

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Nane – Tarehe 13 Septemba, 2018

(Kikao Kilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Mbili, leo ni Kikao cha Nane. Katibu.

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

MHE. ZAINAB A. KATIMBA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE SHERIA NDOGO):

Taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Zainab Katimba. Tunakushukuru sana. Katibu.

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Maswali. Tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, kwa niaba yake, Mheshimiwa Sanga.

Na. 98

Kuboresha Kituo cha Afya cha Ikizu

MHE. DEO K. SANGA (K.n.y. MHE. BONIPHACE M. GETERE) aliluliza:-

Serikali imekuwa na mpango wa kufanya maboresho ya Vituo vya Afya nchini na Kituo cha Afya cha Ikizu ambacho kinahudumia kata zaidi ya 13, majengo yake licha ya kuwa hayatoshelezi hasa wodi ya akina mama wajawazito na watoto, lakini pia yamechakaa sana.

Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu maboresho ya kituo hicho?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, Naibu Waziri, TAMISEMI, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Ikizu ni kati ya vituo viwili vinavyotoa huduma za upasuaji katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda, kituo kingine ni Kasahunga. Katika kukiboresha Kituo cha Afya Ikizu ili kuweza kutoa huduma bora

Serikali imeendelea kufanya maboresho ya miundombinu kwa awamu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali ilifanya ukarabati wa wodi ya wazazi kwa gharama ya shilingi milioni 20. Vilevile katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imepeleka kiasi cha shilingi milioni 33.5 fedha za ufadhili wa *AGPAH* kwa ajili ya ukarabati wa jengo la kutolea huduma na tiba na jengo la stoo. Aidha, Halmashauri imetoa kiasi cha shilingi milioni 5.98 kwa ajili ya kusimika mfumo wa kukusanya mapato na takwimu za afya ili kukiwezesha kudhibiti upotevu wa mapato. Serikali inaendelea kutenga fedha kukikarabati kituo hiki ili kuboresha miundombinu na utoaji wa huduma kwa wananchi.

SPIKA: Mheshimiwa Sanga nilikuona. Swali la nyongeza tafadhali.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali juu ya kituo hiki. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa kituo hiki kilijengwa siku nyingi tangu 1970; na kwa kuwa majengo mengi yamechakaa; na hivi karibuni, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano alipopita katika eneo hilo aliwaahidi Wanabunda wa kituo hiki kwamba kituo hiki kitakarabatiwa haraka; ni lini Serikali itakarabati kituo hiki ili kiweze kuwahudumia wananchi wa Bunda?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Makambako tuna kituo cha afya ambacho kinahudumia wananchi wa Mji wa Makambako; na kwa kuwa mwaka 2017 Serikali ilitupa fedha kwa ajili ya kununua vifaa tiba, hasa vya upasuaji na kwa sababu sasa hivi kituo hakina *x-ray, ultrasound* na vifaa tiba. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha ambazo iliahidi shilingi milioni 500, kwa ajili ya kununua vifaatiba na hela za kujengea wodi ili wananchi hawa wasipate adha ya kwenda kupimwa sehemu nyingine?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Josephat Kandege tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Ikizu ni miongoni mwa vituo bora kabisa katika Wilaya ya Bunda ambayo kinatoa huduma ya upasuaji. Pale wana mpaka *ambulance* na *mortuary* ya kisasa kabisa. Lakini pia naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba azma ya Serikali ya kukarabati vituo vyetu vya afya vilivyochakaa bado iko pale pale. Kutegemeana na upatikanaji wa fedha, tutaendelea kufanya ukarabati na maboresho.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili Mheshimiwa Sanga anataka kujua lini vifaa kama *x-ray* pamoja na *ultrasound* vitapelekwa katika kituo chake cha afya cha Makambako? Naomba nimhakikishie kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI imepeleka fedha *MSD* kwa ajili ya kununulia *x-ray* pamoja na *ultrasound*. Ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba vituo vyote vya afya vinavyokarabatiwa vinatoa huduma ya upasuaji pamoja na vipimo kwa kutumia *x-ray*. Kwa hiyo, nawataka wananchi wa Makambako wahakikishe katika ujenzi unaofanyika, pia na jengo la *x-ray* liwepo. (Makofi)

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Zedi, swali la nyongeza tafadhali.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii.

Kwanza kabisa naipongeza Serikali kwa kutupatia shilingi milioni 800 ambazo maboresho makubwa ya Hospitali ya Wilaya ya Nzega yanaendelea. Sasa nataka kuuliza kwamba Serikali mna mpango gani na Vituo vya Afya vya Itobo na Bukene ambavyo vina tatizo kubwa sana la wodi. Je, baada ya kumaliza maboresho ya Hospitali ya Wilaya, mtakuwa tayari sasa kuelekeza nguvu kwenye Vituo vya Afya vya Itobo na Bukene?

SPIKA: Mtakuwa tayari Mheshimiwa Waziri? Majibu kuhusu Itobo na Bukene.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, kimsingi tutakuwa tayari kama ambavyo tumekuwa tayari siku zote. Hatua kwa hatua tukimaliza vituo hivi ambavyo tumeanza navyo tutakwenda na Vituo vingine vya Afya.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Kapufi.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *Mpanda Town Clinic* ni kituo ambacho kinaisaidia sana Hospitali ya Manispaa ya Mpanda, lakini kwa bahati mbaya kituo hiki ilikuwa kikarabatiwe kwa kupitia fedha za ruzuku kwa maana ya miradi viporo. Naomba kuiuliza Serikali, ni lini watatusaidia fedha hiyo ili tuweze kukisaidia kituo hiki? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, nilipata bahati ya kutembelea Mkoa wa Katavi na Manispaa ya Mpanda nimeitembelea. Pale jirani na *stand*, kuna ujenzi wa Kituo kipyaa cha Afya, lengo ni kuhakikisha kwamba msongamano katika Hospitali ya Wilaya ya Mpanda unapungua.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Kapufi, naye ni shuhuda, tulikuwa wote pamoja; ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba huduma ya afya inasogezwa kwa wananchi.

SPIKA: Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Mwambe, Mbunge wa Ndanda, sasa uliza swali lako.

Na. 99

Gari la Wagonjwa Kituo cha Afya Chiwale

MHE. CECIL D. MWAMBE aliuliza:-

Je, Serikali itapeleka lini gari la wagonjwa kwenye Kituo cha Afya Chiwale kwani ni zaidi ya miaka miwili sasa baada ya gari lililokuwepo kuungua moto?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Chiwale ni moja kati ya vituo vya kutolea huduma za afya 33 vilivyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi. Ni kweli gari la wagonjwa la Kituo cha Afya Chiwale lilichomwa moto na wananchi mwaka 2013, suala hili lilisababisha kituo hicho kukosa gari la wagonjwa kwa muda mrefu na hivyo kusababisha usumbufu mkubwa kwa wagonjwa wanaohitaji huduma za rufaa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi imefanya jitihada za kuhakikisha huduma za dharura kwa wagonjwa wanaohitaji rufaa hazikwami kwa kutoa gari lililokuwa linatumiwa na timu ya Menejimenti ya Afya ya Halmashauri ya Wilaya ya Masasi (*CHMT*). Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi imepewa maelekezo na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kutenga fedha kwenye bajeti kwa ajili ya kununua gari la wagonjwa ili kuwaondolea wananchi usumbufu.

SPIKA: Mheshimiwa Cecil Mwambe.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze tu kuweka taarifa sahihi kadri ya majibu ya Mheshimiwa Waziri hapa, kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ina Vituo vya Afya vinne tu ambapo viwili ni vya Serikali na viwili ni vya *mission* ya Wakatoliki vikiwemo Kituo cha Namombwe na Lukuledi na siyo vituo 33.

Mheshimiwa Spika, suala la gari la wagonjwa la Kituo cha Afya cha Chiwale ambalo liliungua moto mwaka 2010, wananchi waliunguza moto pale na walioliunguza moto gari hilo siyo wananchi wote wa Chiwale isipokuwa ni watu wachache ambao hawakuwa na nia njema wakati huo, lakini Serikali inaonekana kwamba imekuwa ikitumia jambo hili kama adhabu kwa ajili ya watu wa Chiwale.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kupata kauli ya Serikali na tunafahamu kabisa kwamba mapato ya Halmashauri sasa hivi yamechukuliwa na Serikali Kuu, kwa hiyo, isingekuwa rahisi kwa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kuanza kutenga pesa ukizingatia pia ahadi ya Waziri Mkuu wakati tunafanya uzinduzi wa wodi ya akina mama kwenye Hospitali ya Chiwale...

SPIKA: Mheshimiwa Mwambe, *summary* huwa huna kaka yangu.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Spika, sasa swali langu, Serikali, pamoja na hili inalolieleza, vipi, inaweza kutekeleza ile ahadi ya Waziri Mkuu ya kuweza kuleta gari kwenye zahanati ya Chiwale?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kama utakumbuka mwaka 2017 kwenye bajeti iliyopita, Serikali ilitenga shilingi milioni 70 kutoka kwenye *basket fund* kwa ajili ya kudhamini ujenzi wa Kituo cha Afya cha Lukuledi ambapo mpaka sasa hivi naongea hapa, wananchi wako pale wakijitolea pamoja na nguvu ya Ofisi ya Mfuko wa Mbunge. Sasa swali langu ni je, ni lini ahadi ya shilingi milioni 70 ya *basket fund* itapelekwa Lukuledi kwa ajili ya kuwasaidia na kuwaunga mkono wananchi wale? (*Makofi*)

SPIKA: Sasa Mheshimiwa Mwambe, gari mlipewa na Serikali mkachoma wenyewe. Kwa niaba yao, si angalau hata ungekuwa unaomba radhi ili Serikali ikusikie?

Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, katika majibu yangu ya msingi nimesema kuna vituo vya kutolea huduma za afya vitatu, sijasema vituo vya afya. Kwa hiyo, nilikuwa niko sahihi katika jibu nililokuwa nimetoa.

Mheshimiwa Spika, katika maswali yake mawili, kwanza anasema Halmashauri yake haina uwezo wa kutenga fedha kwa ajili ya kununua *ambulance* ambapo lengo la fedha hizo ni kwa ajili ya kusaidia wananchi wanaohitaji huduma ya afya.

Mheshimiwa Spika, ni jana tu nilikuwa naongea na Mkurugenzi wa Halmashauri; uwezo wa Halmashauri wanakusanya jumla ya shilingi bilioni 2.7. Nia ya dhiti ikiwepo wakati inasubiriwa ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kutenga pesa kwa ajili ya kununua gari kwa ajili ya wagonjwa kutoka kwenye shilingi bilioni 2.7 inawezekana kabisa.

Mheshimiwa Spika, ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu itatekelezwa kwa kadri pesa zitakavyopatikana, lakini siyo vibaya kama wakatenga kutoka kwenye bilioni 2.7 kwa ajili ya *ambulance*.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili, anasema kwamba walishaanza ujenzi na tayari kuna ahadi ya shilingi milioni 70 kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa zahanati au kituo cha afya.

Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge; ni azma ya Serikali inayoongozwa na CCM kuhakikisha kwamba huduma za afya zinaboreshwa na kusogezwa kwa wananchi. Kwa hiyo, avute subira. Azma yetu ndani ya miaka mitano ambayo ndiyo ahadi yetu na sisi kwa wananchi, tutatekeleza.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, swali la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile.

Na. 100

Mpango wa Kujitathmini Wenyewe (APRM)

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM aliuliza:-

Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizojiunga na Mpango wa Kujitathmini Wenyewe (*African Peer Review Mechanism*) kisiasa, kiuchumi na kadhalika.

Je, Serikali imejitathmini kwa kiasi gani hali ya uchumi wa Tanzania unaokwenda sanjari na kupungua kwa umaskini?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tanzania ilifanya tathmini ya *APRM* na kutoa ripoti yake ambayo iliwasilishwa kwenye Kikao cha Wakuu wa Nchi mwaka 2013. Tathmini hiyo ilifanyika katika maeneo makuu manne, usimamizi wa uchumi, utendaji wa mashirika ya biashara, siasa na demokrasia na maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la usimamizi wa uchumi, tathmini hiyo ilibainisha masuala mbalimbali yaliyofanywa na Serikali katika kuboresha hali ya kiuchumi ya wananchi wake ikiwa ni pamoja na ushirikishwaji wa wananchi katika kuibua miradi ya maendeleo kwenye maeneo yao; kuimarisha mfumo wa kifedha ikiwa ni pamoja na kutunga Sheria ya Kuzuia Utakatishaji wa Fedha Haramu;

ongezeko la taasisi za kifedha, hivyo kurahisisha upatikanaji wa mikopo kwa wananchi; na kuimarisha ushiriki wa nchi kwenye taasisi za kikanda kama Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*SADC*).

Mheshimiwa Spika, pamoja na tathmini hiyo kubainisha masuala mazuri yaliyofanywa na Serikali, imebainisha pia changamoto mbalimbali za usimamizi wa uchumi. Baadhi ya changamoto zilizobainishwa na Watanzania ni ukuaji wa uchumi usio sanjari na kupungua kwa umaskini na kukosekana kwa mfumo maridhawa wa uwiano wa mapato yanayotokana na mikataba ya kiuchumi ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, tangu ripoti ya *APRM Tanzania* itolewe na kujadiliwa na Wakuu wa Nchi mwaka 2013, hatua mbalimbali zimechukuliwa na Serikali ya Tanzania katika kukuza uchumi kwa lengo la kupunguza umaskini wa wananchi. Hatua hizo ni pamoja na kutekeleza kwa vitendo kauli mbiu ya kujenga uchumi wa viwanda ambao unaendelea kutengeneza ajira na kupunguza umaskini; kuimarisha ukusanyaji, usimamizi na matumizi sahihi ya mapato ya Serikali; kudhibiti ukwepaji kodi; kusambaza umeme vijijini ili kuchochea shughuli za kiuchumi hususan viwanda vidogo vidogo; ujenzi na uboreshaji wa miundombinu; uwekezaji katika kutoa elimu bure na kuongeza bajeti ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi; na kupitia upya sera na sheria mbalimbali kwa lengo la kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji nchini na kuleta uwiano wa mapato yanayoendana na mikataba ya kiuchumi ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ya Awamu ya Tano ni kuhakikisha kwamba inafikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Kwa juhudi hizi za Serikali, ni dhahiri kuwa umaskini utaendelea kupungua hatua kwa hatua ambapo hadi kufikia mwaka 2017 kiwango cha umaskini kimepungua na kufikia asilimia 26.3.

SPIKA: Mheshimiwa Masoud, swali la nyongeza.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imekiri kwamba uchumi unakua lakini na umaskini unaongezeka, ni kwa sababu mmeshindwa kudhibiti mfumuko wa bei. Sasa katika hili tuambiwe hasa Watanzania mtadhibiti vipi mfumuko wa bei wakati huu, wakati hata bei ya sukari yenyewe mmeshindwa kuidhibiti, inaendelea kupanda?

Mheshimiwa Naibu Waziri, awaambie pia Watanzania, mkakati wa kupatikana kwa masoko ya mazao ya uhakika ambapo wakulima wanalalamika kwa muda mrefu. Hilo ni swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, wakati tunaboresha siasa na demokrasia, Wakurugenzi wa Halmashauri wakati wa uchaguzi wanabadilika wanakuwa na wasimamizi wa uchaguzi ambao ni makada watiifu wa Chama cha Mapinduzi, ambao hao ni ma-*referee* katika mfumo wa demokrasia wa vyama vingi. Mtuambie hasa, ni lini Serikali italeta Muswada Bungeni wa kurekebisha mabadiliko haya ili pale tunapoenda kwenye ushindani wa Mfumo wa Vyama Vingi, basi Chama cha Mapinduzi kikishinda, kweli ijulikane kama kimeshinda kulikoni ilivyo sasa wakati Wakurugenzi wa Halmashauri wanapanga mikakati yao kuona kwamba CCM wanashinda? Nashukuru. (*Makofi*)

SPIKA: Maswali yako yote mawili Mheshimiwa Masoud nayakataa. La kwanza la sukari Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji atatoa kauli baada tu ya kipindi cha maswali. Ukiangalia *Order Paper* yako utaona mwisho huko. Kwa hiyo, mambo ya bei ya sukari na kadhalika atasema mwenyewe, atakuja muda siyo mrefu hapa.

Swali la pili la uchaguzi, siyo sehemu kabisa ya swali lako. Swali lako lilikuwa linauliza mambo ya uchumi. Kwa hiyo, la uchaguzi lilete katika utaratibu wake.

Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo,
Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi.

Na. 101

Kuboresha Viwanda vya Michezo

MHE. SILAFU J. MAUFI aliuliza:-

Serikali inafahamu kuwa michezo ni afya na ni ajira pia, lakini mikoa kadhaa hapa nchini ina viwanja visivyokidhi hadhi ya kitaifa na kimataifa na hata kasi ya kuibua vipaji vipya imedorora katika Mikoa ya Rukwa, Tabora, Iringa, Kigoma na kadhalika.

Je, Serikali sasa haioni umuhimu wa kushirikiana na wamiliki wa viwanja hivyo kuvikarabati na kuviboresha kufikia hadhi stahiki?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTHONY P. MAVUNDE K.n.y. WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba ujenzi wa miundombinu ya michezo ni jambo muhimu sana katika kuendeleza vipaji vya wanamichezo na ndiyo sababu ya Serikali kujenga viwanja changamani vikubwa viwili nchini ambavyo ni Kiwanja cha Uhuru na Kiwanja cha Taifa, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya kazi ya ujenzi wa kiwanja kikubwa cha Ngamani cha tatu Jijini Dodoma yanaendelea. Hata hivyo Serikali haiwezi peke yake kujenga miundombinu ya kisasa kwa michezo yote bila mchango wa Halmashauri zetu, taasisi za umma, asasi na kampuni binafsi

na vilevile mashirikisho na vyama husika vya michezo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, pale penye jitihada bayana za kujenga miundombinu ya michezo, Serikali daima imekuwa mstari wa mbele kusaidia juhudi hizo. Utaratibu mkubwa wa viwanja vya Kaitaba - Kagera na Nyamagana - Mwanza, ni matokeo ya mazingira mazuri ya ushirikishaji yaliyowekwa na Serikali kati ya wadau soka, Shirikisho la Soka nchini na Shirikisho la Soka la Dunia.

Aidha, ukarabati mkubwa wa viwanja vya Namfua - Singida; Samora Machel - Iringa na *Majaliwa Stadium* - Ruangwa ni matokeo ya mazingira mazuri ya ushirikiano yaliyowekwa na Serikali kati ya wadau, *TFF* na Wizara yenye dhamana ya michezo. Naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mbunge) kwa kuonesha mfano wa kuhamasisha Halmashauri yake na wananchi wa Ruangwa kuunganisha nguvu na kujenga uwanja wa *Majaliwa Stadium*. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Silafu Maufi, uliza swali.

MHE. SILAFU J. MAUFI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri katika swali langu la msingi, mimi kama Mheshimiwa Mbunge wa Bunge hili la Jamhuri wa Muungano wa Tanzania na bahati nzuri kwa rehema zake Mwenyezi Mungu, jana tu tumepitisha sheria ya kuiwezesha Serikali kuingia ubia na mashirika binafsi katika maendeleo ya wananchi wetu wa Tanzania.

Je, kwa nini Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa wao kuingia ubia na sekta hii binafsi yenye viwanja hivi vinavyomikiwa na hawa watu ambao ni viwanja vyao vya halali? Kwani wamevijenga kwa muda mrefu na wanasuasua katika kuviendeleza viwanja hivi ili waweze kuingia ubia waweze kuvikarabati na watoto wetu wapate afya njema na waweze kupata ajira katika maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali inipatie majibu kwa hilo swali dogo ambalo nimeliuliza kwa wakati huu. (Makofi)

SPIKA: Majibu ya swali hiyo Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Anthony Mavunde.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTHONY P. MAVUNDE K.n.y. WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO): Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba moja kati ya mkakati wa kuendeleza michezo mbalimbali nchini ni pamoja na kuwa na miundombinu rafiki ya kuwafanya washiriki wa mchezo husika kuweza kushiriki kwa ufanisi mkubwa. Ni dhamira ya Serikali kuendeleza viwanja vingi vya michezo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ushauri uliotolewa na Mheshimiwa Mbunge wa kushirikisha sekta binafsi na wadau mbalimbali, sisi kama Serikali tuko tayari. Lengo letu ni kujenga mazingira rafiki ya kufanya michezo mbalimbali iliyo na miundombinu ambayo itatoa fursa kwa washiriki wake kushiriki kikamilifu.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa nakupa nafasi ya swali la nyongeza, tafadhali.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Tatizo la ubovu wa viwanja limekuwa kubwa sana hapa nchini. Sasa Serikali haioni kwamba huu ni wakati sahihi sasa wa kuanzisha Wakala wa Kusimamia Viwanja vya Mpira ili iwe inasimamia ubora wa viwanja vyote vya mpira hapa nchini?

SPIKA: Majibu ya swali hilo fupi, Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna haja ya wakala au hapana?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTHONY P. MAVUNDE K.n.y. WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO): Mheshimiwa Spika, chini ya Wizara pamoja na Shirikisho la Michezo

Tanzania kwa maana *TFF* iko Idara maalum ambayo inasimamia ubora na vigezo vya viwanja ambavyo vitatumiwa katika michezo mbalimbali. Utaratibu uliowekwa ni kwamba iko *international standard* ambayo inavitaka viwanja mbalimba viwe vina sifa zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kwa Kiwanja cha Mpira wa Miguu, kwa mujibu wa *international standard* kinatakiwa kiwe kati ya mita 100 mpaka mita 110 na upana wake uwe ni mita 64 mpaka mita 75. Kwa hiyo, tunayo Idara chini ya *TFF* na kwenye Wizara ambayo kazi yao ni kushughulikia viwanja ambavyo vitakuwa ni bora.

Mheshimiwa Spika, pia kwa wazo ambalo ameleta Mheshimiwa, naamini kazi kubwa ambayo tutafanya kama Serikali ni kuboresha Idara zetu za ndani ili ziendeleo kufanya utaratibu kuhakikisha kwamba tunakuwa tuna viwanja bora zaidi vya watu kuchezea.

SPIKA: Swali la Mheshimiwa Anna Lupembe, kwa niaba yake Mheshimiwa Dkt. Kamala mwulizie.

Na. 102

Usikivu wa *TBC* - Wilaya ya Mlele

MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA (K.n.y. MHE. MHE. ANNA R. LUPEMBE) aliuliza:-

Je, ni lini Redio Tanzania (*TBC*) itasikika katika Kata za Ilela na Ilunde Wilayani Mlele?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTHONY P. MAVUNDE K.n.y. WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TBC* imeendelea na jitihada za kupanua usikivu katika Mikoa na Wilaya ambazo bado hazina usikivu au kuwa na usikivu hafifu wa redio. Katiba bajeti ya mwaka 2016/2017 *TBC* ilitengewa kiasi cha shilingi bilioni moja kwa ajili ya upanuzi wa usikivu katika Wilaya tano za mpakani mwa nchi. Maeneo ambayo mitambo imefungwa na matangazo ya redio kuwashwa ni Rombo, Nyasa, Tarime, Kibondo na Namanga. Serikali inaendelea na utaratibu huo wa kuongeza usikivu kwenye maeneo yasiyo na usikivu mzuri katika Mikoa ya Katavi, Njombe, Simiyu na Songwe.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali ni kujenga mitambo ya redio katika Mikoa hii katika bajeti ya mwaka 2019/2020 na katika bajeti ya mwaka 2018/2019 *TBC* imetengewa kiasi cha shilingi bilioni tano kwa ajili ya ujenzi wa studio za redio na *television* Makao Makuu ya nchi Jijini Dodoma.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Kamala. Kule Nkenge kule inasikika *TBC*? (*Kicheko*)

MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA: Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, haisikiki. Nashukuru sana. Ninayo maswali mawili ya nyongeza. Ukiangalia swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe angependa kujua hasa kwa Kata za llela na Ilunde nini kinafanyika? Sasa pamoja na kwamba Katavi imetajwa na mipango ipi, ni nini hasa kinaandaliwa kufanywa katika maeneo hayo na ni shilingi ngapi zimetengwa?

Swali la pili; kwa kuwa katika Wilaya ya Karagwe, Biharamulo, Ngara pamoja na Misenyi, *TBC* haisikiki na wananchi wangependa kuisikia, ni nini kinafanyika kuwezesha *TBC* kusikika katika maeneo hayo? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali kuhusu usikivu wa *TBC*.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTHONY P. MAVUNDE K.n.y. WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO): Mheshimiwa Spika, nikianza na swali la kwanza; katika majibu yangu ya msingi, nimezungumzia Mkoa wa Katavi kwa ujumla ambao tafsiri yake ni kwamba itajumuisha pia Kata za Ilunde na Ilele ambazo ziko ndani ya Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha bajeti ya mwaka 2017/2018 Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo tumetengewa kiasi cha shilingi bilioni 33.2 ambapo mpango mkakati tulionao hivi sasa ni kuhakikisha kwamba tunaongeza zaidi usikivu kwa sababu ukiangalia katika mwaka 2016 *TBC* ilikuwa ina usikivu wa asilimia 54 tu nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, ndani ya miaka miwili baada ya bajeti hii kuongezeka, tumefikia usikivu wa asilimia 64. Mkakati uliopo ni kuyafikia maeneo mengi zaidi ili wananchi wapate fursa ya kupata habari kupitia *TBC*.

Mheshimiwa Spika, nikienda katika swali la pili la katika maeneo ya Misenyi, jibu langu ni hili hili la kwamba kwa mwaka huu wa fedha ambapo tuna kiasi cha fedha nilichokisema hapo tulichotengewa, kazi yetu kubwa ni kuhakikisha kwamba tunaendelea kufunga mitambo mingi zaidi ili wananchi wapate fursa ya kuweza kusikia *TBC*.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo yale ya pembezoni tumeongeza usikivu kutoka kilowati 200 mpaka kilowati 1000 na ninaamini kabisa kwamba kwa mwaka huu wa fedha tutajipanga vizuri zaidi kuhakikisha kwamba wananchi wengi wanaisikia *TBC*.

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Maliasili na Utalii tafadhali. Mheshimiwa Msigwa, Iringa inasikika *TBC*.

Mheshimiwa Ester Alexander Mahawe, Mbunge wa Viti Maalum, uliza swali lako tafadhali.

Na. 103

Gharama za Kupanda Mlima Kilimanjaro

MHE. ESTER M. MMASI (K.n.y. MHE. ESTER A. MAHAWE)
aliuliza:-

Gharama za kupanda Mlima Kilimanjaro ni mara mbili ya gharama za kupanda Mlima Kenya; hali hii imesababisha kushuka kwa idadi ya watalii na kuinyima Serikali mapato.

Je, ni lini Serikali itafanya marekebicho ya bei hizo?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ester Alexander Mahawe, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mlima Kilimanjaro ni mlima mrefu kuliko yote Barani Afrika ukiwa na urefu wa mita 5,895 kutoka usawa wa bahari. Mlima huu una sifa nyingi za kipekee ikiwemo ya kuwa mlima mrefu duniani uliosimama peke yake (*the only free standing mountain in the world*), asilimia 85 ikiwa ni *vertical*, wenye barafu japo upo katika Ukanda wa Ikweta. Ni moja ya eneo la Urithi wa Dunia na umetunukiwa tuzo ya kuwa kivutio bora (*One of the Africa Wonders*).

Mheshimiwa Spika, aidha, Mlima Kilimanjaro una aina zaidi ya 200 ya ndege na zaidi ya aina *species* 140 za mamalia wakiwemo tembo, pofu, pongo, jamii ya swala, minde, twiga, simba, chui na wengineo, sifa ambazo Mlima Kenya hauna.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kununi za kupanda mlima, Mlima Kilimanjaro hupandwa kwa wastani wa siku sita. Safari ya kupanda mlima huu kwa mtalii kutoka nje ya nchi huipatia Serikali mapato ya dola za Kimarekani 684.4 pamoja na kodi ya VAT. Mtalii anayepanda Mlima Kenya kwa siku sita hulipa dola za Marekani 460. Tofauti ya gharama

kati ya milima hii zinatokana na umuhimu wa kipekee pamoja na sifa ya Mlima Kilimanjaro ambazo haziwezi kulinganishwa na Mlima Kenya.

Mheshimiwa Spika, njia ya kupanda Mlima Kilimanjaro zimetengenezwa vizuri kiasi cha kuwezesha mtu wa kawaida asiye na utaalam kupanda mlima hadi kileleni wakati kwa Mlima Kenya upandaji unahitaji utalaam (*technical climbing*). Tofauti hizi husababisha gharama za utalii kati ya milima hii zisifanane.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2017/2018 Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro ilipokea na kuhudumia watalii 51,825 ambao waliingizia Taifa mapato ya shilingi bilioni 76.16. Kwa sasa Serikali imepanga kukutana na wadau wa Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro ili kukubaliana masuala mbalimbali ikiwemo bei ya kupanda Mlima Kilimanjaro.

SPIKA: Mheshimiwa Ester Mmasi, swali la nyongeza.

MHE. ESTER M. MMASI: Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa *background information* nzuri sana. Kimsingi nioneshe tu masikitiko yangu kwamba ukiangalia muktadha wa swali hili, itoshe tu kusema kwamba bado Mheshimiwa Waziri hakuweza kulitendea haki swali hili.

Mheshimiwa Spika, swali liliuliza; je, ni lini Serikali itafanya marekesho ya bei hizi katika kuimarisha uchumi wa Taifa hili na hususan wakazi wa Mkoa wa Kilimanjaro? Ingekuwa swali linauliza je, Serikali ina mkakati gani? Ndipo jibu lilipaswa kuwa hili. Kwa sababu jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri linasema Serikali imejinga kukutana na wadau. Ni kweli, lakini swali lililenga kujua ni lini hasa?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, ni kweli kwamba moja ya kuinua mapato ya Serikali kupitia kivutio hiki cha Mlima wa Kilimanjaro ni pamoja na kuboresha mpango mkakati wa soko la utalii duniani. Nilipenda Mheshimiwa Naibu Waziri atuambie, je, kupitia uwekezaji wa Shirika la Ndege la Tanzania ni kwa nini Serikali haikuona umuhimu

wa kurudisha nembo ya Mlima wa Kilimanjaro katika ndege hizi za Shirika la Ndege ili basi kwa muktadha huo tuweze kuinua soko la utalii kwa nchi ya Tanzania? Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Tuliwahi kuwa na nembo ya Mlima Kilimanjaro kwenye ndege huko *before*? Mheshimiwa Waziri, sisi tunajua huwa anakuwepo Twiga tu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumpongeza. Najua yeye ni mdau mkubwa sana katika huu mlima na amekuwa akitushauri sana katika masuala mengi. Kuhusu maswali yake yote mawili ambayo ameuliza, suala la kuuliza ni lini? Labda nilitaarifu Bunge lako tukufu kwamba kupitia Kamati ya Kudumu ya Bunge tumeshakutana na wadau mbalimbali katika kuzungumza masuala mbalimbali zikiwemo changamoto pamoja na gharama kubwa ambazo wanatozwa watu mbalimbali wanaopanda Mlima Kilimanjaro. Tumeshakaa tumezungumza, lakini kama Serikali tunataka kujiridhisha. Tunataka tukutane na wadau wengi zaidi kuliko wale wa vyama vyao ili tuone kama kuna haja ya kupunguza au hakuna haja ya kupunguza.

Mheshimiwa Spika, suala la kwamba ni lini? Basi niseme tu kwamba kati ya kipindi cha sasa mpaka mwezi Desemba, hili suala tutakuwa tumeshafikia muafaka kama tupunguze au tuongeze. Kwa hiyo, siyo suala la kupunguza tu.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwamba kulikuwa na nembo kwenye Shirika la Ndege zetu la Kilimanjaro, nadhani tulikuwa na alama kwa ajili kutangaza Mlima wetu Kilimanjaro. Ilikuwemo kwenye nembo hiyo na bado itaendelea kuwemo. Mpaka sasa hivi tumeweka zaidi, lakini siyo tu kutangaza Mlima Kilimanjaro, bali tunaangalia na vivutio vingine vingi ambavo vipo, ndiyo maana ndege zetu sasa hivi tunaweka vitu vingi na alama nyingi zaidi ambazo zinaendelea kulitambulisha Taifa letu. Bado tutakaa na wadau mbalimbali kuona kama kuna haja ya kurudisha ile alama iwepo pale kama alama ya utambulisho. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri gharama za hawa watalii wanaokuja siyo lazima iwe ni *get fee* peke yake ambayo ndiyo inaingia Serikalini, hata hao *operators* nao wana gharama zao. Kwa hiyo, lazima iwe *both sides, private sectors* nao wapunguze kama ikibidi kuelekea huko. Mheshimiwa, nilikuona.

MHE. NURU A. BAFADHILI: Ahsante Mheshimiwa... aah!

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Aah, ni mimi bwana.

Nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Nakubaliana na Mheshimiwa Waziri kwamba gharama za kupanda Mlima Kenya haziwezi kulingana na Mlima Kilimanjaro kwa sababu ya *unique* tuliyonayo katika mlima wetu. Tumezungumza na *tour guides* ambao wanafanya hiyo kazi, wanasema hiyo siyo sababu; sababu ni kuongezeka kwa *18 percent* ya *VAT* katika gharama ambayo inamgusa moja kwa moja mtalii.

Je, Serikali lini sasa itakaa kuona kwamba hili ni tatizo na kuonda *18 percent* kwa wageni wanaokuja ili waje kwa wingi na tukusanye kwa wingi? (*Makoff*)

SPIKA: Kuondoa *VAT* kwenye masuala ya utalii, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, ni kweli kabisa kwamba Serikali ilianzisha *VAT* katika huduma mbalimbali za kitalii ambazo zinatolewa, ni karibu takribani miaka miwili sasa imepita toka kuanzishwa kwa *VAT*.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tuliagizwa tufanye utafiti mpana zaidi tuone kama kweli hii *VAT* imeleta athari. Sasa katika kipindi kifupi ni vigumu sana kuweza kujua kama *VAT* imeleta athari au haijaleta athari. Kwa hiyo, sasa hivi ambacho tunakifanya, tunataka tufanye *study* kubwa, lakini pia tuone ni maeneo gani ambayo tunaweza kuyatumia

ambayo tunaweza kupanua wigo wa kupata mapato mengi zaidi badala ya kutegemea tu suala la VAT.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili tutalifanyia kazi na tunaomba tuendelee kupata maoni zaidi na mawazo namna ya kuboresha huduma zetu hizi za utalii.

SPIKA: Ahsante sana. Tunaelekea kwenye Wizara ya Katiba na Sheria, swali la Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mbunge wa Kavuu, kwa niaba yake Mheshimiwa Chenge tafadhali.

Na.104

Sheria Zilizopitwa na Wakati

MHE. ANDREW J. CHENGE (K.n.y. MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE) aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta baadhi ya sheria zilizopitwa na wakati Bungeni ili ziweze kupitiwa upya zierendane na wakati uliopo hasa zikiwemo Sheria za Usalama Barabarani?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (MHE. ANTHONY P. MAVUNDE K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mbunge wa Kavuu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa sheria za nchi zinakidhi mahitaji ya wakati, Serikali imekuwa ikifanya mapitio ya sheria ya kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania iliyopo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, Tume hii imekuwa ikifanya mapitio na tafiti mbalimbali ambazo zimekuwa ni msingi wa

marekebisho ya sheria au kutungwa kwa sheria mpya hapa nchini. Kazi ya mapitio ya sheria ni endelevu na Serikali itaendelea kuwasilisha Bungeni miswada ya sheria ambayo inalenga kurekebisha sheria za nchi au kutunga sheria mpya ili kukidhi mataakwa ya wakati.

SPIKA: Swali la nyongeza, Mheshimiwa Andrew Chengé, tafadhali.

MHE. ANDREW J. CHENGÉ: Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali kwa majibu yake. Nina maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza, muuliza swali alilenga hasa katika Sheria ya Usalama Barabarani. Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya marekebisho katika sheria hiyo?

Swali la pili; natambua kazi nzuri inayofanywa na Tume ya Kurekebisha Sheria; je, Serikali inaweza kwa wakati muafaka ikatoa *report* za kazi ambazo zimefanywa na Tume hiyo kama mapendekezo kwa Bunge lako tukufu? Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (MHE. ANTHONY P. MAVUNDE K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA): Mheshimiwa Spika, nikianza na swali la kwanza, ni kweli kwa mujibu wa sheria iliyoanzisha Tume ya Kurekebisha Sheria Sura Na. 171 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002, moja kati ya kazi ya Tume ni kuandaa *report* ambayo hupelekea mabadiliko ya sheria au kutungwa kwa sheria mpya.

Mheshimiwa Spika, katika Sheria za Usalama Barabarani tayari Tume imeshafanya kazi yake na tunayo *report* ya Tume ya mwaka 2004 ambayo imeshawasilishwa kwa Mheshimiwa Waziri. Pindi pale itakapoonekana kuna mahitaji ya kufanya marekebisho katika sheria husika, sheria

hii itawasilishwa hapa Bungeni kwa ajili ya kuweza kufanyiwa marekebisho kama ambavyo Mheshimiwa muuliza swali amesema.

Mheshimiwa Spika, la pili, kuhusiana na *report* za Tume kuwasilishwa katika Bunge; kwa mujibu wa sheria Tume hii inapaswa kutoa taarifa yake ya kila mwaka ya namna ambavyo imezipitia sheria. Tunao mpango mkakati wa kuanzia mwaka 2013 mpaka mwaka 2018 wa marekebisho hayo ya sheria.

Mheshimiwa Spika, suala la uwasilishwaji wa taarifa hii, itakuwa ni kati ya Serikali na Bunge kuona namna bora ya kuwasilisha, lakini kwa hivi sasa taarifa zetu zinapatikana katika mitandao yetu mbalimbali na utaratibu mwingine wa Kiserikali kuhakikisha kwamba wananchi wengi wanazipata.

Mheshimiwa Spika, kwa maombi ya Mheshimiwa Mbunge, kama Serikali tumesikia na tutaona namna bora ya kuweza kulifanyia kazi jambo hilo.

SPIKA: Mheshimiwa Magdalena Sakaya nilikuona, swali fupi.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, zipo sheria nyingine ambazo kuchelewa kuletwa Bungeni zina-*cost* maisha ya watu moja kwa moja. Kwa mfano, Sheria hii ya Usalama Barabarani, suala la sasa hivi Bodaboda ku-*overtake* kushoto linasababisha ajali nyingi sana na watu wengi wanapoteza maisha. Sheria inasema *overtake* kulia, lakini wewe una-*overtake* kushoto na ajali nyingi zinatokea kwa utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa maisha ya watu yanapotea kila siku, Serikali haioni haja ya kuleta sheria hii kwa *fast-track* Bungeni ili kuokoa maisha ya watu wanaoteketea kila siku kwa sababu ya Sheria ya Barabarani kuwa imepitwa na wakati?

SPIKA: Hapa nafikiri kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi yupo hapa, akohoe kidogo. Karibu Mheshimiwa. *(Kicheko)*

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama ndani ya Bunge hili tukufu nikiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, nichukue fursa hii kuendelea kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuniamini kwamba ninatoshia na ninaweza kumsaidia kazi hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Pia nakushukuru wewe kwa ushirikiano ambao unanipatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nampongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Mavunde namna ambavyo amejibu swali la msingi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa katika kupambana na ajali za barabarani, na sisi tunajua kabisa bodaboda kama alivyosema Mheshimiwa Sakaya limekuwa ni tatizo kubwa. Tayari hivi tunavyozungumza, majibu mazuri kabisa ya Mheshimiwa Mavunde ni kwamba marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani yako katika hatua za mwisho. Aiamini Serikali kwamba tutaiteta hapa Bungeni kwa ajili ya Bunge hili kuweza kuipitisha. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nilipokuwa naangalia swali la Mheshimiwa Dkt. Kikwembe ikabidi niangalie na takwimu nyingine kidogo hapa, nikaangalia humu Bungeni hivi tuna *Doctorate* ngapi hapa? *Ph.D* ziko ngapi? Sasa nilipoangalia nikaona kwa ujumla ziko 20. Katika 20, 19 CCM; lakini kesho nitajipanga vizuri zaidi nitakuja na takwimu nyingine. *(Makofi)*

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, swali la Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Buhigwe.

Na. 105

Ujenzi wa Kituo cha Polisi Buhigwe

MHE. ALBERT O. NTABALIBA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi katika Wilaya mpya ya Buhigwe na kutoa vitendea kazi kwa Jeshi la Polisi?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Buhigwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto za miundombinu Kijiografia pamoja na nyinginezo zinazoikabili pamoja na mikoa mipya hapa nchini. Changamoto hizi ni pamoja na uhaba wa Ofisi na nyumba za kuishi watumishi. Hata hivyo, Jeshi la Polisi katika Wilaya mpya ya Buhigwe limeshatenga eneo kwa ajili ya Ofisi ya Mkuu wa Polisi wa Wilaya na Kituo cha Polisi cha Wilaya chenye ukubwa wa ekari tano. Pia zimetengwa ekari 20 kwa ajili ya nyumba za makazi ya Askari Polisi. Aidha, kwa sasa huduma za kipolisi katika maeneo ya Buhigwe hutolewa kupitia kituo kidogo cha Polisi cha Buhigwe na Manyovu.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya vituo vya polisi pamoja na nyumba za makazi ya askari nchini ni makubwa na yanahitaji fedha nyingi. Haya hivyo, Jeshi la Polisi limeweka vipaumbele katika Mikoa na Wilaya mpya, Miji inayokuwa kwa kasi pamoja na maeneo yenye viashiria na matishio ya kiusalama ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

SPIKA: Mheshimiwa Ntabaliba swali la nyongeza.

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nashukuru majibu ya Serikali. Ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, tunacho Kituo cha Mlyama ambacho kimejengwa kwa muda mrefu sasa hakijamalizika na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani analijua hilo na pale Wilayani tuna kituo ambacho kinatumiwa kwenye nyumba ambayo siyo nzuri na haitoshi; na kwa majibu haya kwamba wametenga eneo; swali linauliza kwamba ni lini wanaanza kujenga? Hayo maeneo tunashukuru wanayo, lakini swali, wanaanza kujenga lini?

Mheshimiwa Spika, la pili; tuna matukio makubwa sana ya ujambazi yanayotokea hasa baada ya Wakimbizi kurudishwa kwenda Burundi na Jimbo langu linavamiwa kila siku iendayo kwa Mungu na juzi mwanajeshi mmoja ameuawa baada ya kuwa wameenda ku-*intervene* mashambulio hayo na vitendea kazi ni hafifu.

Je, ni lini sasa vitendea kazi vya magari na pikipiki vitaongezwa kwenye Wilaya ile? Yeye mwenyewe anayo taarifa kwamba ujambazi ni kila siku. Nakushukuru.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa *Engineer* Masauni tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na lini kituo hiki kitajengwa; nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa kutambua changamoto ya *location* ya Jimbo lake, pale ambapo tutapata fedha ni katika vituo ambavyo tutavipa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, sambamba na kujibu swali lake la pili ambalo lithatusha vilevile pamoja na upelekaji wa vitendea kazi ili tuweze kukabiliana na changamoto ambayo ameizungumza ambayo tunaitambua na tumeshaanza kushughulika nayo.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Nuru Bafadhili, swali la nyongeza tafadhali.

MHE. NURU A. BAFADHILI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Katika Kata za Jiji la Tanga miaka ya 1990, kata zilihamasishwa kujenga vituo mbalimbali vya Polisi ambavyo vilisaidia kupunguza uhalifu, matokeo yake sasa hivi vituo vile vimetelekezwa, vimekuwa ni nyumba za vibaka.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuvifufua vituo hivyo ili kuweza kuweza kuzuia uhalifu?

SPIKA: Majibu ya swali hilo kuhusu Vituo vya Polisi vya Tanga.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, mara zote tumekuwa tukihamaisha Waheshimiwa Wabunge na wananchi kushirikiana na Serikali katika kukabiliana na upungufu wa Vituo vya Polisi nchini. Kwa hiyo, ni jambo la ajabu sana kama Serikali tutakubali kuona kwamba jitihada hizi za wananchi wanavunjwa moyo.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba siyo dhamira ya Serikali kuvitelekeza vituo hivyo ambavyo vina umuhimu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Mheshimiwa Mbunge hakutaja kituo gani ambacho kimetelekezwa, kwa hiyo, ni vigumu kumpa sababu ya kituo hicho ambacho amekusudia kwamba hakitumiki mpaka sasa hivi kwa sababu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, baada ya Bunge hili nitakuwa tayari kukutana naye ili aweze kunipa taarifa za kina tufuatilie na kuchukua hatua za haraka. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Mattar Ali Salum, Mbunge wa Shaurimoyo. Bado tuko Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mattar. *(Makofi)*

Na.106

Kumweka Ndani Mtuhumiwa kwa Saa 24

MHE. MATTAR ALI SALUM aliuliza:-

Polisi wanapowakamata watuhumiwa baadhi wanawaweka ndani kwa saa 24 na wengine zaidi ya saa 24.

(a) Je, ni makosa yapi mtuhumiwa anaweza kuwekwa ndani zaidi ya masaa 24?

(b) Je, ni makosa yapi ambayo mtuhumiwa anaweza kuwekwa ndani chini ya saa 24?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mattar Ali Salum, Mbunge wa Shaurimoyo lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20, kifungu cha 148(5)(a) mpaka (e) kinaeleza makosa mabaya mtuhumiwa anaweza kuwekwa kizuizini zaidi ya saa 24. Makosa hayo ni kama vile uhaini, mauaji, ujambazi wa kutumia silaha, kujihusisha na biashara ya dawa za kulevya, ugaidi, usafirishaji wa fedha haramu, mtuhumiwa aliyewahi kuhukumiwa kifungo kinachozidi miaka mitatu ama aliwahi kuruka dhamana na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, makosa ambayo mtuhumiwa anaweza kuwekwa ndani chini ya saa 24 ni makosa yote isipokuwa yaliyoainishwa katika kifungu cha 148(5)(a) mpaka (f).

SPIKA: Mheshimiwa Mattar, swali la nyongeza tafadhali.

MHE. MATTAR ALI SALUM: Mheshimiwa Spika, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Alhaji Masauni.

Mheshimiwa Spika, wapo askari wanaowaweka ndani watuhumiwa zaidi ya saa 24 wakati hawana makosa ya kuwekwa ndani zaidi ya saa 24. Serikali inawachukulia hatua gani askari hawa wakibainika wanakiuka Sheria za Jeshi la Polisi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Watanzania wengi hawana elimu ya Sheria ya Jeshi la Polisi. Serikali ina mkakati gani wa kutoa elimu ili Watanzania wakafahamu haki yao ya kimsingi ili waweze kujua taratibu za kuwekwa ndani zaidi ya saa 24 na sheria ambazo haziwahusu kuwekwa ndani zaidi ya saa 24? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo ya Mbunge wa Shaurimoyo, Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, nataka nimjibu Mheshimiwa Mattar kwamba sheria niliyoizungumza inahusisha watu wenye makosa ya aina ambayo nimeyataja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama kutakuwa kuna Askari Polisi ambaye amemweka mtu ndani na hakufanya makosa ambayo nimeyataja, naye Mheshimiwa Mattar anamfahamu, basi ni wajibu wake kuweza kuwasilisha taarifa hiyo ili tuweze kuchukua hatua kama ambavyo tumefanya kwa askari wengine wenye makosa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, katika kipindi cha miezi sita ya mwaka huu, takriban askari 15 ambao walifanya makosa ya kukiuka maadili ya utendaji wao wa kazi ambao tumeweza kupokea taarifa zao na kati ya hao mpaka sasa hivi tayari askari wawili wameshachukuliwa hatua. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mattar kama ana taarifa hizo aziwasilishe katika mamlaka husika ili hatua ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, suala la elimu linaendelea kutolewa na ni wajibu wa kila mtu akiwemo yeye Mheshimiwa Mbunge kuweza kutusaidia kutoa elimu kwa wananchi wake, ingawa kutokufahamu sheria hakuhalalishi juu ya uvunjifu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi kwamba tutaendelea kujitahidi kadri itakavyowezekana watusaidie Waheshimiwa Wabunge akiwemo Mheshimiwa Mattar kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na ufahamu wa sheria mbalimbali katika nchi yetu. *(Makofi)*

SPIKA: Majibu ya nyongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, tafadhali Mheshimiwa Kangi Lugola.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba niongezee majibu ya nyongeza kwenye majibu mazuri ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ameyasema.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kulikuwa na malalamiko kwa wananchi kwa kuwekwa ndani na baadhi ya askari ambao sio waaminifu, siyo waadilifu kwenye makosa ambayo hayastahili, lakini pia wamekuwa wakiwaweka ndani baadhi ya wananchi kwenye makosa ambayo pia hayahitajiki hata kuwekwa ndani, hata nusu dakika au sekunde.

Mheshimiwa Spika, tayari nimeshatoa maelekezo kwamba Makamanda wote wa Polisi wa Mikoa na Wakuu wa Polisi wa Wilaya, kituo chochote ambacho kitaonekana na malalamiko ya kukiuka utaratibu huu wa kuweka wananchi ndani, viongozi hao watawajibika. Hivi karibuni nitaanza ziara kwenye mikoa yote ya Tanzania pale ambapo nitakuta vituo, askari bado wanalalamikiwa, askari hao hawatakuwa na nafasi ya kuendelea kulichafua Jeshi zuri la Polisi ya nchi yetu. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa nahitaji watu ambao wamewahi kuwekwa ndani saa 24, sasa mnasimama watu hamjawahi hata kukaa ndani. Haya nitatoa nafasi tatu Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa John Heche na Mheshimiwa Susan Kiwanga. Mheshimiwa Esther Matiko. *(Kicheko)*

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amejibu kwamba ikigundulika askari wanaowaweka kituoni wananchi kwa muda watachukuliwa hatua. Wakati nachangia bajeti iliyopita ya Wizara ya Mambo ya Ndani nilieleza bayana kabisa kwamba kuna baadhi ya mahabusu kituo cha Kawe waliwekwa ndani kwa zaidi ya miezi mitatu na nikasema kabisa na nikamtaja na askari aliyehusika mpaka leo hajachukuliwa hatua.

Je, ni kwa nini Mawaziri wanatumika kwenye Bunge Tukufu kuwadanganya watanzania bila kuchukua hatua?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kuhusiana na hii hoja ya mahabusu Kituo cha Kawe, tulishawahi kutoa maelekezo, uchunguzi ufanyike ili hatua ziweze kuchukuliwa, lakini kama Mheshimiwa Mbunge atataka kulithibitishia Bunge hili tukufu mpaka kama

hatua hazijachukuliwa, basi nimuahidi kwamba nitakapotoka hapa nitafuatilia nijue ni kwa nini hatua kama hazijachukuliwa ama pengine wanastahili kuendelea kukaa ndani kwa mujibu wa sheria.

SPIKA: Mheshimiwa Heche nimeshakutaja.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, ninafikiri kwamba ni vema Mawaziri wetu wanapokuja kutoa majibu hapa wajue Watanzania wanawaangalia na Watanzania wanasikitika sana pale wanapokuwa wanatoa taarifa ambazo siyo za kweli. Kwa mfano, juzi amekamatwa Mwenyekiti wa Kijiji anaitwa Tanzania Omutima, Kijiji cha Kewanja kwa tuhuma tu, amekaa siku nne hajafikishwa Mahakamani na wala hajapelekwa polisi. Pia amekamatwa kijana anaitwa Mudude Nyagali, amewekwa ndani zaidi ya siku 30.

Mheshimiwa Spika, ninachoomba Waziri atoe tamko kwamba ni marufuku kuanzia sasa watu wa *abide* na sheria, kukamata mtu na kukaa naye zaidi ya yale masaa ambayo sheria inaruhusu kama mtu amefanya hivyo afikishwe kwenye utaratibu, ashitakiwe kwa kukiuka sheria ambayo tunayo mpaka sasa.

SPIKA: Lakini Mheshimiwa Heche, lakini huko unakoulizia unajua ni Kanda Maalum kule. Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwanza napingana kabisa na kauli yake kwamba Mawaziri hapa tunatoa majibu ambayo siyo sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, majibu ambayo tunayotoa hapa ni majibu ambayo tumeyafanyia utafiti wa kina na tunajiamini kwamba tunachokizungumza hapa ni kitu ambacho ni sahihi kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anataka tutoe tamko, matamko tumekuwa tukitoa kila siku na siyo lazima atoe matamko kwa sababu sheria zinajulikana, tunachokifanya ni kusimamia sheria ambazo tumezitunga humu Bungeni na Mheshimiwa Heche anazifahamu. Kwa hiyo, iko wazi kwamba yeyote ambaye hafuati sheria na hakuna ambaye yuko juu ya sheria, ikiwemo Wasimamizi wa Sheria ambao ni Vyombo ya dola.

Mheshimiwa Spika, tunasema kila siku kwamba kama kuna Askari yeyote ambaye anatumia nafasi yake vibaya kinyume na maadili yake ya kazi, tutamchukulia hatua na tumekuwa tukifanya hivyo, tukiwachukulia na tutaendelea kufanya hivyo. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Susan Kiwanga.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante mimi siko mbali...

SPIKA: Sahamani kidogo Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani anataka kuongezea kidogo, tafadhali. Samahani Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri juu ya swali ambalo limeulizwa na Mheshimiwa Heche.

Mheshimiwa Spika, pengine nitoe fursa ya kuelimisha kidogo hii dhana ya saa 24 kukaa mahabusu. Kwenye Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, unapomkamata kwa mara ya kwanza mtuhumiwa na kumuweka mahabusu, kwa maana ya matakwa ya saa 24. Saa 24 yale yanaendana na upelelezi wa awali. Kuna mazingira ambapo uliyemweka ndani hata kabla ya saa 24 hayajafika mtamtoa ndani katika upelelezi ama kuna mahala anaenda kuonesha silaha, ama kuna mahala anaenda kuonesha ushahidi fulani kutokana na maelezo yake. Mnapotoa atakaporudi mahabusu huyo mtuhumiwa anaanza kuhesabiwa masaa yake upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya wananchi wanahesabu tangu alipokamatwa, lakini kisheria tunahesabu tofauti. Kwa hiyo, nimuelimisha Mheshimiwa Heche, huyo anayemsema Mwenyekiti wa Kijiji ambaye aliyekamatwa pale Nata, kulikuwa na masuala ya vielelezo vya *documents* kwa sababu fedha za kijiji zaidi ya shilingi milioni 300, vilevile ilikuwa inahusisha na Kampuni ya Uwekezaji wa *Grument*. Kwa hiyo, aliyekuwa amekamatwa tulitoa maelekezo. Mheshimiwa Heche dhana hii muifahamu vizuri ya masaa 24.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naona wananchi waelewe dhana ya saa 24 inaanza wakati gani na inaisha wakati gani. Siyo nia ya Serikali kuwatesa wananchi wake, na ndiyo maana majibu niliyoyatoa mwanzo nilisema wale askari ambao watakiuka sheria hiyo ya kuwaweka ndani tunachukua hatua, hakuna yeyote ambaye tunamfumbia macho. Kwa hiyo, Mheshimiwa Heche uwe na amani huyo mtu unayemsema tumeshatoa maelekezo na tunajua *concern* yako. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Tunapotetea watuhumiwa waliokula zaidi ya shilingi milioni 300 za wananchi napo inabidi tuwe makini kidogo. Mheshimiwa Susan Kiwanga.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Waziri Kangi Lugola ni awamu yake ya kwanza ya kuwa katika nafasi hii, na kwa kuwa mara nyingi nikimsikia na hata ndani ya Bunge amethibitisha ya kwamba atakomesha hiyo hali ya wananchi kuonewa, kuwekwa mahabusu muda mrefu bila utaratibu wowote.

Mheshimiwa Spika, je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari sasa kwenda kwenye mahabusu ya Wilaya ya Ifakara na Mlimba kwenda kuangalia hali halisi, mahabusu wanavyowekwa ndani muda mrefu lakini hata chakula hawapewi, mara nyingi nimeenda kuwanunulia chakula na kuwapa mahabusu haki zao zinavunjwa kabisa za kibinadamu, hilo wa kutowapa mahabusu chakula unalizingumziaje?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi tafadhali, jukumu la nani kumpa mahabusu chakula.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwanza wananchi wa Tanzania nataka niwahakikishie kwamba siyo nia wala lengo la Jeshi la Polisi kuwatesa mahabusu wanapokuwa wamekamatwa na wako ndani. Mahabusu wote wanapata chakula na wapo watu ambao wanapewa *tender* hizi za kuleta vyakula kwa mahabusu, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, pili kumekuwa na wananchi pia ambao wana vyakula wanavyohitaji kuwaletea wananchi mahabusu wao. Vyakula hivyo pia tumekuwa tukiwaruhusu kuwapatia mahabusu na kwa kuwa amelenga Mlimba, kwamba kuna matatizo nimeishasema kwamba kutokana na tatizo la baadhi ya askari wachache ama kuwabambikiza kesi wananchi ama kuwatesa nimesema jambo hilo halitakuwa na nafasi na litakomeshwa. Nimesema nitaanza ziara mikoa yote hivi karibuni na hizo kero nitazishughulikia. (*Makofi*)

SPIKA: Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ulikuwa hujaja muda mrefu hapa, sasa maswali inabidi yaongezeke kidogo. Mheshimiwa Khatib umesimama sana, swali la mwisho la nyongeza kwenye Wizara hiyo.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, katika siku za karibuni kumejitokeza tabia chafu, mbaya na ovu kabisa ya mahabusu kufia kwenye Vituo vya Polisi. Mahabusu anapelekwa, wanashikiliwa, wanapata mateso ambayo yanapelekea vifo vyao. Hivi karibuni tu kuna baadhi ya jamii zimekataa kupokea maiti kwenda kuzika kutokana na kufia ndani ya Vituo vya Polisi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri anatoa kauli gani kali ya kukemea tabia hii ambayo inatia aibu nchi yetu ambayo ni ya haki na demokrasia?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Kangi Lugola, tafadhali.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa mwananchi kufa, anakufa wakati wowote, mahali popote na ndiyo maana sijui kwenye Qurani, ila kwenye Biblia ukisoma Muhubiri 9:12 ni kwamba kifo ni mtego, kifo humnasa mtu wakati wowote, mahali popote. Kwa hiyo, mwananchi anaweza akafa akiwa polisi, anaweza akafa akiwa anafanya mapenzi, anaweza akafa akiwa kwenye gari anasafiri, anaweza akafia hata humu ndani ya Bunge. Kwa hiyo, isije ikachukuliwa kwamba anayefia kwenye Kituo cha Polisi ni kwamba ameteswa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ninakiri kwamba kumekuwa na matukio ambapo wananchi wanafia mikononi mwa polisi na pale ambapo matukio hayo yanajitokeza tumekuwa tukifanya uchunguzi na pale inapobainika kwamba polisi wamehusika tumekuwa tukichukua hatua, ndiyo maana tunazuia wananchi wasichukue sheria mikononi za kuanza kuvamia vituo kwa sababu mtu amefia mikononi mwa polisi. Nimekuwa nikihoji huyu anayekufa akifanya mapenzi mbona hawaendi kuchoma kitanda na nyumba kwamba amefia mikononi mwa kitanda? Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

SPIKA: Mheshimiwa Khatib umeyataka mwenyewe.

Tunaenda Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, swali la Mheshimiwa Mary Deo Muro.

Na. 107

Ujenzi wa Barabara ya Kibaha Kupitia Vikawe na Bagamoyo

MHE. MARY D. MURO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya *TAMCO* Kibaha kupitia Vikawe kuunganisha na barabara ya Bagamoyo ili

kupunguza msongamano wa magari yanayoenda Mbezi Boko na Bagamoyo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mary Deo Muro, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya *TAMCO* kupitia Vikawe hadi Mapinga yenye urefu wa kilometa 23 ni barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) ambapo kilometa 22 zimejengwa kwa kiwango cha changarawe na kilometa moja imejengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina pamoja na tathmini ya fidia katika barabara hii ilikamilika katika mwaka wa fedha 2012/2013. Utekelezaji wa ujenzi wa kiwango cha lami umeanza kwa awamu ambapo kilometa moja imekamilika kujengwa. Vilevile taratibu za ununuzi kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa kipande cha kilometa 2.5 zimekamilika ambapo Mkandarasi *Skol Building Contractors* amepatikana na anategemewa kusaini mkataba mwishoni mwa mwezi huu wa Septemba, 2018.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 kiasi cha shilingi bilioni 1.5 kimetengwa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Aidha, taratibu za ununuzi wa mkandarasi wa ujenzi kwa kiwango cha lami kwa kipande kingine cha kilometa 1.5 zimeanza. Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) Mkoa wa Pwani anaendelea kufanya matengenezo mbalimbali barabara hii ili iweze kupitika majira yote ya

mwaka ambapo shilingi bilioni 1.789 zimetengwa katika mwaka huu wa fedha kutoka Mfuko wa Barabara.

SPIKA: Mheshimiwa Mary Deo Muro tafadhali.

MHE. MARY D. MURO: Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kwenye jibu lake la msingi amekiri kwamba tathmini ilifanyika 2012/2013; swali sasa watu hawa wamekatazwa wasiendeleze na nyumba zao zimebomoka na tathmini hairudiwi na anasema kwamba mkandarasi anaanza ujenzi; je, anaanzaje ujenzi wakati wananchi hawa hawajalipwa fidia yao?

Swali la pili, kwa kuwa tathmini ilifanyika 2012/2013 na sasa hivi ni miaka mitano imepita, je, Serikali ina jibu gani kuhusu kurudiwa kwa tathmini au malipo yao itakuwa vipi kwa sababu nyumba nyingine zimebomoka na nyingine zimeanguka. Ni mkakati gani ambao wataufanya ili wananchi wale waweze kupata malipo yao kwa tathmini mpya?

SPIKA: Majibu ya swali hilo la Mheshimiwa Mary Deo Muro, Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Eliasi Kwandikwa.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Spika, eneo hili la barabara ya kutoka *TAMCO* kwenda Mapinga ni barabara muhimu sana, hivi ninavyoongea tunaendelea na utaratibu wa kuhakikisha ujenzi unafanyika ili kuweza kukamilisha kilometa tano za eneo hili. Eneo hili ni muhimu sana kwa sababu barabara hii sehemu ambayo tunayoanza kujenga ndiyo maeneo ambayo ndiyo kitovu cha Mji wa Kibaha kwa maana ya kwamba maendeleo yanafanyika katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa eneo hili ujenzi unaanza, lakini kuhusu fidia ni kwamba kumbukumbu muhimu za fidia katika eneo hili

zimeshachukuliwa na kumbukumbu muhimu zimekubaliwa na wananchi ambao wamepisha eneo la ujenzi, kwa sababu hiyo haitaathiri malipo yao wakati ujenzi unaendelea.

Kwa hiyo, kikubwa tu niwapongeze na kuwashukuru wananchi wa eneo hili kwa uzalendo na kwa kweli nao wanahitaji hii barabara iweze kuwepo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge usiwe na wasiwasi tumeweka kumbukumbu vizuri na wananchi wameshasaini kukubali malipo ya kwao na pia upo utaratibu kama tukichelewa kulipa kuna viwango huwa vinabadilika kutokana na utaratibu uliopo.

Mheshimiwa Spika, pia kwa eneo hili ambalo ujenzi utaanza, utaratibu wa kuwalipa wananchi fidia upo mbioni, kwa hiyo niwatoe hofu wananchi kwamba wakati ujenzi unaendelea kufanyika na malipo yao yatafanyika hususani kwa kilometa hizo tano ambazo tumetathmini kwa sababu eneo lote hili la barabara wanastahili kulipwa kama shilingi bilioni 8.9 hivi. Kwa hawa wa kilometa tano, kama shilingi bilioni moja hivi itatumika kulipa fidia. Niwatoe wananchi wa maeneo haya watalipwa fedha zao kulingana na taratibu ili kupisha barabara hii muhimu kwa ajili ya maendeleo yao wao wenyewe.

SPIKA: Ahsante sana. Swali la nyongeza nilikuona Mheshimiwa Salma Kikwete, tafadhali.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana naomba niulize swali langu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa upatikanaji wa kivuko baina ya Kata ya Msinjahili na Kitumbikwera ulikuwa uende sambamba na ujenzi wa sehemu za kusubiria abiria; na kwa kuwa takribani mwaka mmoja umeshapita tangu kivuko kipatikane.

Je, lini Serikali itajenga sehemu za kusubiria abiria baina ya Kitumbikwera na Msinjahili ili kuwaondolea adha wananchi hawa? *(Makofi)*

SPIKA: Majibu ya swali hilo muhimu Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie nafasi hii nimpungeze sana Mheshimiwa, kwa sababu suala hili amekuwa akilifuatilia sana ni muda mrefu na mimi nilifika eneo hili la kivuko na hali niliyoikuta pia nilitoa maelekezo ili tuweze kupata kibanda cha abiria na pia ujenzi wa huduma zingine.

Mheshimiwa Spika, ni furaha yangu tu kumueleza Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Lindi kwamba tumeshapata mkandarasi, ameshasaini Mkataba kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya abiria ya kusubiria usafiri, maeneo yote ya pande mbili za vivuko tutaweka pia huduma zingine kama vyoo vya kisasa na tumetoa maelekezo kwamba ujenzi uanze haraka kabla ya msimu wa mvua.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nikupe tu taarifa kwamba tutasimamia kuhakikisha huduma muhimu katika maeneo haya yanapatikana haraka kabla ya mvua. *(Makofi)*

SPIKA: Swali la mwisho kwa siku ya leo twende Wizara ya Maji ya Umwagiliaji litaulizwa na Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mheshimiwa Mbunge wa Mpanda Vijijini.

Na. 108

Kukarabati Visima Vilivyochimbwa na UNHCR – Mpanda

MHE. MOSHI S. KAKOSO aliuliza:-

Tatizo la maji katika vijiji vya Mlibansi, Mazwe, Mgamsamansi, Ilangu, Kapemba na Busongola ni kubwa sana.

Je, ni lini Serikali itakarabati visima vilivyochimbwa na *UNHCR* ili viweze kutatua tatizo la maji katika vijiji hivyo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo yatajiibiwa na Mheshimiwa Waziri mwenyewe wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Profesa Mbarawa tafadhali.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza awamu ya pili ya programu ya maendeleo ya sekta ya maji nchini kote. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 1.302 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maji vijijini inayohusisha ujenzi, upanuzi na ukarabati wa miundombinu ya maji. Kupitia fedha hizo zilizotengwa Serikali itakarabati miradi mbalimbali ya maji katika Halmashauri ya Mpanda ikiwemo visima vilivyochimbwa na *UNHCR* vilivyopo katika Vijiji vya Mlimbasi, Mazwe, Mgamsamansi, Ilangu, Kapemba na Busongola.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa Halmashauri wa miaka mitano yaani kuanzia mwaka 2015 mpaka 2020 wa usambazaji wa maji safi na usafi wa mazingira, Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda imepanga kufanya upembuzi yakinifu kwa miradi mikubwa ya usambazaji maji katika kijiji cha Busongola. Aidha, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kukarabati na kujenga miradi ya maji nchini kulingana na upatikanaji wa fedha ili iweze kutatua kero ya upatikanaji wa huduma kwa wananchi.

SPIKA: Mheshimiwa Kakoso tafadhali.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Spika, nishukuru sana kunipa nafasi hii, nishukuru majibu ya Mheshimiwa Waziri ambayo yanatia matumaini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vijiji 16 ambavyo vipo katika eneo la Mishamo ni vya muda mrefu na miundombinu yake ilishakuwa chakavu. Serikali haioni sasa ni wakati

muhimu wa kupeleka miradi mikubwa ambayo itawasaidia hawa wananchi kupata maji yenye uhakika?

Swali la pili, ipo Miradi ya Maji ya Mwese, Kabungu, Kamjera yenye thamani ya shilingi bilioni 2.4 na tayari wakandarasi walishafanya kazi kwa kuanza na fedha zao; je, ni lini Serikali itapeleka fedha hizi ili waweze kukamilisha hiyo miradi?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Profesa Mbarawa, Waziri wa Maji na Umwagiliaji tafadhali.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali kwanza ni kujenga miundombinu mikubwa kwa ajili ya maji ili yaweze kuwafikia wananchi mbalimbali na katika hivyo vijiji 16 vya Mishamo ambavyo amevisema Mheshimiwa Mbunge, tutahakikisha kwamba tunajenga miundombinu mikubwa ambayo itaweza kuwafikia wananchi wote kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Mheshimiwa Kakoso tunazo takribani kandarasi tano. Tuna makandarasi watano ambao wanafanya kazi na kazi hiyo ina gharama takribani ya shilingi bilioni 2.78. Mpaka sasa hivi makandarasi wawili bado hawaja-*rise certificate* yoyote, mkandarasi mmoja tumeshamlipa *advance payment* na makandarasi wawili ambao ni Dar Huduma na *DDSA* tayari wameleta *certificate* na hivi sasa tunaendelea na kuzichambua ili tuweze kuwalipa makandarasi hao.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda tuishie hapo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya mimi kutaja kidogo takwimu zile nimepata maandishi mengi sana ya Waheshimiwa Wabunge wengine wakiwa rafiki zangu kutoka upande huu, wakisema Mzee basi kesho usije ukataja takwimu ziishie hapo hapo, sasa sijui niendeleo nazo kesho au niache? Maana alipokuwa anajibu hapa Profesa Mbarawa nikakumbuka kwamba chama pekee chenye

maprofesa humu Bungeni ni CCM. Kwa hiyo, ngoja nikajipange halafu kesho nitakuja ndio mtaona kwamba CCM imejipanga vipi. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Jukwaa la Spika ni wageni wangu watatu ambao ni Balozi wa Ujerumani nchini Tanzania Mheshimiwa Dkt. Deflef Weachter, *German Ambassador to Tanzania* karibu Mheshimiwa Balozi na ameambatana na Maafisa Ubalози wawili Dkt. Richard Shaba na Ndugu Pamela Kanora, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia ninaye mgeni maalum kabisa Waheshimiwa Wabunge naye si mwingine bali ni Mkurugenzi Mkuu mpya kabisa wa TAKUKURU, Kamishina wa Polisi Diwani Athumani. Mheshimiwa Mkurugenzi Mkuu Bunge tunakupongeza sana, tunakutakia kila la kheri na taasisi hii itakupa kila aina ya ushirikiano. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni wangu wengine ni Wajumbe wa Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar ambao Mwenyekiti wake Ndugu Idrissa Kheir Juma, karibu, Ndugu Jokha Khamis Makame -Mjumbe, Ndugu Ussi Jecha Simai - Mjumbe, Ndugu Hamida Mussa Khamis - Mjumbe, Ndugu Haidar Haji Abdulla - Mjumbe, Ndugu Zahor Juma Khamis – Mjumbe, huyu Zahor siyo yule aliwahi kuwa Mbunge hapa? Nahisi. Pia Katibu wa Tume Ndugu Ali Ali Haji na Maafisa wawili Ndugu Khamis Silima Juma na Ndugu Omar Abdalla Ameir. *(Makofi)*

Tume ya Huduma za Bunge kwa upande wa Baraza la Wawakilishi inaitwa Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi yenyewe Wajumbe wake hawatokani na Wabunge wanatoka nje ya taasisi. Kwa hiyo, ndiyo hawa wageni waliotutembelea karibuni sana na mtakutana na Wajumbe wenzenu muda siyo mrefu. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tunae mgeni wa Mheshimiwa Stella Alex Ikupa - Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Watu wenye Ulemavu ambaye ni Mchungaji Gibson Gondwe kutoka Mkoani

Mwanza, Mchungaji ahsante yuko kule. Mgeni wa Mheshimiwa Elias Kwandikwa - Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, mgeni huyo ni kutoka Chuo Kikuu cha T/A cha Mkoani Mbeya ambaye Ndugu Pius Wilbard Sambamba yuko pale karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni 14 wa Mheshimiwa Oscar Mukasa ni wanakikundi kinachoshughulika kuwakinga watoto wadogo wasipate maambukizi ya UKIMWI (AGPAHI) wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mheshimiwa John Mongella na Mheshimiwa Seif Shekalaghe Mkuu wa Wilaya ya Maswa, karibuni sana Mkuu wa Mkoa yupo pia? Karibuni sana, jambo mnalolishughulikia ni jambo muhimu kweli katika maisha ya watoto wetu. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji ambao ni watoto wake kutoka Zanzibar, Ndugu Sumaya Abdallah na Ndugu Farahati Abdallah, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Susan Kiwanga ambao ni watoto wake kutoka Mkoani Morogoro wakiongozwa na Ndugu Diana Kiwanga. Mheshimiwa Susan watoto watano si haba! *(Kicheko)*

Mgeni wa Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein ambaye ni mdogo wake kutoka Arusha Ndugu Farhad Saleh Khamis, ahsante Farhad yule kule. Pia kuna wageni wa Mheshimiwa Oran Njeza kutoka nchini Afrika Kusini Ndugu Dennis Cooke - *General Manager Panda Hill Tanzania Limited* na Ndugu Pierre Joubert - *Investment Advisor Tremont Investment Limited*, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunae mgeni wa Mheshimiwa Fatma Toufiq ambaye ni Mganga Mfawidhi - Ndugu Ngoyeji Yusuph Nkinga kutoka Zahanati ya Nzasa Dodoma, yule pale karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa George Lubeleje ambao ni Mchungaji Ashery Magomba na Mama Mchungaji

Helena Elenei kutoka Mwapwa karibuni sana, Mheshimiwa George Lubeleje amefiwa na mdogo wake jana, kwa hiyo tunampa pole sana Mheshimiwa Lubeleje na tuko naye katika wakati huu mgumu.

Wageni wawili wa Kamati ya Uchangishaji Fedha kwa ajili ya kuboresha mazingira ya mtoto wa kike mashuleni kutoka kampuni ya *The Network* (TatuMzuka) karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, upande wa wanafunzi tunao wanafunzi 55 na walimu sita wa shule ya sekondari Magole kutoka Kilosa Mkoani Morogoro, wakiongozwa na Mwalimu Abdiel Mtui. Wanafunzi wa Magole naomba msimame karibuni sana wanangu nitakutana na ninyi baadae kidogo. *(Makofi)*

Pia kuna wanafunzi 120 na Walimu 19 kutoka shule ya msingi Nyamata ya Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Mwalimu Mkuu wao Mwalimu Geoffrey Yungu. Wanafunzi kutoka Dar es Salaam, ahsanteni na karibuni sana watoto wetu, karibuni mjifunze kuhusu Bunge. *(Makofi)*

Katibu tuendele. *(Makofi)*

MWONGOZO WA SPIKA

SPIKA: Haya miongozo hiyo miwili anza Mheshimiwa Mwambe.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuomba mwongozo wa meza yako ili iweze kuelekeza jambo ambalo limekuwa likiendelea sasa hivi. Wizara ya Mambo ya Ndani kupitia Jeshi la Mageza kwenye Gereza la Wilaya ya Masasi, Kijiji cha Namajani kumekuwa na mgogoro wa muda mrefu sana wa masuala la ardhi ambayo yamesababisha uvunjifu wa amani katika maeneo hayo na tulikuwa tukiripoti kila mara. Hivi juzi Wizara ilituandikia barua ikisema kwamba itawaleta wathamini ili kuja kufanya upya *valuation* kwa maana ya

kutaka kuona namna ya kuwalipa wale wananchi waweze kuondoka sasa.

SPIKA: Sasa Mheshimiwa Mwambe hilo limetokea leo wakati gani hilo?

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Spika, linaendelea huku ndani ya Bunge.

SPIKA: Utuhalalishie tu ili uendelee vizuri. Ahsante sana Mheshimiwa Gekul.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) juu ya usimamizi wa taasisi za fedha na mashirika ya kibiashara ambayo wakati Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje alizungumzia kwamba hili wao wanafanya.

Naomba mwongozo wako kuhusu hizi taasisi za fedha hususani *microfinance* ambazo hazijafanya vizuri na nitolee mfano wa *PRIDE Tanzania* ambapo sasa *network* ya matawi 72 nchi nzima yamefungwa *portfolio* zaidi ya shilingi bilioni 80 hazijulikani zilipo.

Mheshimiwa Spika, inasemekana *top management* wamekimbilia nje ya nchi, kwa hali halisi wafanyakazi zaidi ya 500 nchi nzima na wateja zaidi ya 150,000 hawajui akiba zao ziko wapi, wafanyakazi wengine wako pemba kwao ni Kigoma wamekwama, miezi tisa hawajalipwa mishahara na malalamiko jameshatoka kwenye vyombo vya habari, Mheshimiwa Rais ameshaandikiwa, Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Waziri Mkuu na hakuna majibu na hili linagusa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, ninakuomba kwa nini Serikali isitoe kauli hapa Bungeni kutuambia hali halisi ya kinachoendelea katika *PRIDE Tanzania* na Serikali ilishawahi kuwa na hisa na kwa kinachoendelea sasa...

SPIKA: Mheshimiwa hilo umeli-*link* na swali gani?

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, nimeli-*link* na swali namba 100 wakati anajibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

SPIKA: Mbona hilo halina uhusiana kabisa.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, lina uhusiano kwa sababu alizungumzia kuhusu taasisi za kifedha na mashirika ya kibiashara na usimamizi wake, masuala ya kiuchumi na hili limekuwa likigusa wananchi wetu kwa nchi nzima sasa.

SPIKA: Hapana, halina uhusiano Mheshimiwa Mbunge. Swali lilikuwa linahusu mambo ya *Peer Review Mechanism* na hali ya uchumi wa nchi kwa ujumla wake, lakini la kwako ni *very specific*, lakini wamesikia. Katibu tuendeleo.

NDG. LINA KITOSI - KATIBU MEZANI:

KAULI ZA MAWAZIRI

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Kauli za Mawaziri naomba sasa nimuite Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, nadhani ungekuja mbele.

Sasa naomba Waheshimiwa Wabunge tumsikilize Mheshimiwa Waziri tafadhali, karibu sana.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Spika, taarifa ya hali ya sukari nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na taarifa hii ninayoisoma ambayo inasambazwa kuna viambatisho viwili vyenye kutoa takwimu zenye ufafanuzi wa kina.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya sukari nchini yanakadiriwa kuwa tani 670,000 ambapo tani 515,000 ni kwa matumizi ya kawaida na tani 155,000 kwa matumizi ya viwandani (*industrial sugar*). Uzalishaji wa sukari kwa viwanda vyetu vitano vya ndani kwa mwakwa 2018/2019 unakadiriwa

kuwa tani 353,651 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na hakuna kiwanda kinachozalisha sukari kwa ajili ya matumizi ya viwandani. Hivyo naksi ya sukari nchini ni takribani tani 316,349 ikihusisha tani 161,349 kwa maana ya matumizi ya kawaida na tani 155,000 kwa ajili ya matumizi ya viwandani ambazo itabidi kuagizwa kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, viwanda vyote vitano vilivyopo nchini vinaendelea na uzalishaji wasukari tangu mwezi Mei na Juni 2018. Kiwanda cha Kilombero kilianza uzalishaji tarehe 22/5/2018 na kufuatiwa na Viwanda vya Manyara tarehe Mosi Juni, Kagera tarehe 13 Juni, TPC tarehe 13 Juni na Mtibwa tarehe 20 Juni. Hadi kufikia tarehe 05 Septemba, 2018 jumla ya kiasi cha tani 119,671.19 zilikuwa zimezalishwa. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 33.84 ya malengo ya uzalishaji wa viwanda vyote vitano kwa mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 5 Septemba, 2018 kiasi cha sukari ya matumizi ya kawaida kilichopo katika maghala ya wenye viwanda na wasambazaji/wafanyabiashara wakubwa ni tani 118,130.22. Kiasi hiki kinahusisha tani 65,089 kilichozalishwa na viwanda vya ndani; Kilombero tani 37,694, TPC tani 7,340, Kagera tani 12,800, Mtibwa tani 7,155 na Manyara tani 100 na tani 38,119 zilizoagizwa na viwanda hivyo kutoka nje ili kuziba pengo la sukari (*gap sugar*).

Mheshimiwa Spika, sukari iliyopo kwenye maghara ilyoagizwa kutoka nje ya nchi, Kilombelo wanazo tani 6,954, TPC tani 15,026, Kagera tani 3,070 na Mtibwa tani 13,069. Kiasi cha sukari kilichopo nchini kinatosheleza mahitaji ya sukari kwa kipindi cha miezi mitatu mbali na uzalishaji unaoendelea.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya tasnia ya sukari kwa kipindi cha miezi sita kuanzia mwezi Machi hadi Agasti, 2018 kuhusu hali ya upatikanaji wa sukari Tanzania inaonesha kuwa bidhaa hiyo inapatikana bila matatizo katika maeneo yote nchini. Aidha, takwimu za bei hadi kufikia tarehe 5 Septemba zinaonesha kuwa wastani wa bei ya viwanda (*ex -factory price*) ni kati ya shilingi 1,746 na shilingi 2,160.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mauzo ya reja reja mwezi Mei ndiyo ulikuwa una bei ya juu nchini, ambapo kilo moja ya sukari iliuzwa shilingi 2,900 Mkoa wa Kigoma. Bei ya chini ilikuwa mwezi Agosti, 2018 ambapo kilo moja ya sukari imeuzwa shilingi 2,300 kwa rejareja Mkoa wa Morogoro. Ni muhimu kuzingatia kuwa bei za bidhaa hii zilianza kupungua taratibu baada ya msimu wa uzalishaji kuanza mwezi Mei.

Mheshimiwa Spika, kwa wastani wa bei za rejareja nchini bei za wastani wa juu ilikuwa ni shilingi 2,669 mwezi Mei, bei ya wastani wa chini ilikuwa shilingi 2,595 kwa mwezi Agosti, 2018. Kwa bei za juu kimkoa, Mkoa wa Kigoma kilo moja ya sukari iliuzwa 2,900 kwa mwezi Mei, 2018 na mwezi huo huo bei ya chini kimkoa bei ilikuwa ni 2,400 Mkoa wa Kagera. Kwa mwezi wenye unafuu wa bei Mkoa wa Kigoma kilo moja ya sukari iliuzwa shilingi 2,850 mwezi Agosti na mwezi huo huo bei ya chini ilikuwa ni shilingi 2,300 kwa Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya bei za sukari kimkoa inaonesha mapungufu ya usambazaji ambao Mkoa wa Kigoma ulinunua sukari kwa shilingi 2,900, Mkoa wa Ruvuma shilingi 2,850, Mkoa wa Rukwa shilingi 2,850, Mkoa wa Katavi shilingi 2,800, Mkoa wa Mtwara shilingi 2,800 na Mkoa wa Njombe 2,850. Kwa kipindi chote cha mwaka kwa bei ya juu sana kuliko Mkoa mingine.

Mheshimiwa Spika, kama nitakavyoeleza kwenye hitimisho taarifa hii, Serikali imewaagiza wenye viwanda kuboresha mfumo wa usambazaji sukari nchini kwa lengo la makusudi la kupunguza makali ya bei kwenye mikoa hiyo ukilinganisha na Mikoa mingine nchini.

Mheshimiwa Spika, utafiti uliofanywa na Kampuni ya *LMC International* ya Uingereza mwaka 2014 kuhusu gharama za kuzalisha tani moja ya sukari katika tasnia ya sukari nchini ulibaini kuwa inagharimu wastani wa USD 705 kuzalisha tani moja. Kwa kutumia kiwango cha kubadilisha dola kwa shilingi kwa sasa hii ni sawa na shilingi 1,607 kwa kilo moja.

Utaona hapa kuwa gharama na hatimaye bei ya sukari inategemea kuimarika kwa dola ya Kimarekani dhidi ya shilingi ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, viwanda vya sukari vinatumia mafuta, mitambo na vipuli bidhaa ambazo bei zake hupanda pindi dola ya Kimarekani inapoimarika dhidi ya shilingi ya Tanzania. Hii ni moja ya sababu inayochangia bei ya sukari kuwa kubwa au kubadilika mara kwa mara. Sababu nyingine ni mashamba mengi ya miwa kulimwa kwa kutumia mtindo wa zamani ambao hauna tija kubwa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo juu tathmini inaonesha kuwa hakuna ongezeko kubwa la bei ya sukari kati ya mwezi Machi na Septemba, 2018. Tofauti kati ya bei ya wastani wa juu na chini ni shilingi 75, ambapo bei ya wastani wa juu ni shilingi 2,669 mwezi Mei, 2018 na bei ya chini ni shilingi 2,594 mwezi Agosti, 2018. Kwa bei ya rejareja Mkoa wa Kigoma ambao mwezi wa Mei wananchi wake walinunua sukari kwa shilingi 2,900; mwezi Agosti bei ilipoanza kushuka walinunua sukari kwa shilingi 2,850.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako tukufu kuwa haukuwepo upandaji wa bei mkubwa sana ila mabadiliko ya kati shilingi 50 mpaka shilingi 150 hutegemea Mkoa na Mkoa.

Mheshimiwa Spika, kufuatia matokeo ya tathmini hii Serikali inaendelea kuhakikisha wananchi wanapata sukari wakati wote na kwa bei stahiki. Aidha, Serikali imetoa maelekezo kwa viwanda vyote kuwasilisha mapendekezo mapya juu ya mfumo wa kusambaza sukari nchini. Kama nilivyoeleza hapo juu na ukirejea bei za sukari viwandani (*ex-factory prices*) ikilinganishwa na bei ya bidhaa hiyo Mkoa kwa Mkoa na kwa mauzo ya rejareja tutaweza kumpatia mradi nafuu kidogo ya bei tukiondoa madhaifu katika mfumo wa sasa wa usambazaji sukari.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye aya ya tatu hapo juu mpaka tarehe 5 Septemba, tani 12,800 za sukari

zilikwa zimerundikana Kiwandani Kagera ikilinganishwa na tani 1,000 ambacho ndizo kiwango cha juu kinachopaswa kutunzwa kiwandani wakati wa uzalishaji wa kawaida. Hali hiyo si kwa Kiwanda cha Kagera tu bali ni kwa viwanda vyote hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, suluhisho la tatizo hili ambalo ni tishio kwa maendeleo ya viwanda vya sukari ni kubuni utaratibu mpya wa kusimamia uagizaji wa kiasi cha upungufu wa sukari (*gap sugar*) Kazi hii itakamilika kabla ya mwisho wa mwezi Oktoba, 2018. Aidha, ushauri wa kusambaza sukari nchini ili kusaidia kushusha bei ya sukari wazo hilo haliwezi kuleta matokeo chanya, hii ni kutokana na ukweli kuwa Mikoa yote ya nchi hii sasa ina sukari ya kutosha, lakini pia bei ya sukari inategemea gharama za usafirishaji, kodi na gharama ya utunzaji vigezo ambavyo siyo rahisi kuviepuka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu gharama ya kuzalisha tani moja ya sukari, Serikali inafatilia mpango wa viwanda wakuongeza tija katika mashamba ya miwa hali ambayo itapelekea gharama za uzalishaji kushuka. Aidha, wawekezaji wapya wanaoanza kuwekeza katika uzalishaji wa sukari wanapewa maelekezo ya ulimaji na utunzaji wa miwa kwa njia zinazooongeza tija kubwa kwa lengo la kupunguza gharama ya uzalishaji na hatimaye kumpatia mlaji wa mwisho bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, noamba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji Mheshimiwa Charles Mwijage kwa taarifa hiyo. Natumaini Waheshimiwa Wabunge tayari mnazo nakala za hiyo kauli, kama hamna basi muda siyo mrefu mtapata nakala za taarifa hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, basi kwa hatua hii naomba nimpishe Mheshimiwa Najma Giga aweze kuendelea.

Hapa Mwenyekiti(Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Katibu tuendelee.

NDG. LINA KITOSI – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA KAMATI

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Kumi na Moja wa Bunge

MWENYEKITI: Namkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo Mheshimiwa Chenge. (*Makofi*)

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu Bunge Sheria Ndogo, nakushukuru kwa kutoa idhini kwa Kamati yangu iweze kutoa taarifa kuhusu uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa mezani na Serikali katika Mkutano wa Kumi na Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumaini kuwa taarifa hii itawezesha Waheshimiwa Wabunge kutoa ushauri zaidi kuhusu Sheria Ndogo zilichambuliwa na Kamati pamoja na Sheria Ndogo nyingine ambazo zinatumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati inaamini kuwa Serikali itayafanyia kazi mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii na maoni yatakayotolewa na Wabunge ili kuondoa dosari zilizobainika kutokana na uchambuzi uliofanywa na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madaraka ya kutunga sheria; Ibara ya 64 ya Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, imelipa Bunge la Jamhuri wa Muungano wa Tanzania mamlaka ya kuchunga sheria juu mambo yote ya Muungano na yasiyo ya Muungano yahusuyo Tanzania Bara. Aidha, Ibara ya 97 ya Katiba imeweka utaratibu ambao unapaswa kuzingatiwa na Bunge katika kutekeleza madaraka yake ya kutunga sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mamlaka iliyonayo Bunge ya kutunga sheria, kiuhalisia Bunge halina muda wa kutosha wa kutunga sheria kuhusu masuala yote ambayo utekelezaji wake unahitaji uwepo wa sheria. Kutokana na hali hiyo ndiyo maana Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 97, Ibara Ndogo ya Katiba inalipa Bunge uwezo wa kukasimu madaraka yake ya kutunga sheria kwa mtu yoyote au Idara yoyote ya Serikali. Sheria zinazotungwa kwa utaratibu huo zinaitwa sheria ndogo (*subsidiary legislation* au *delegated legislation*), ambazo hujumuisha Kanuni mbalimbali (*rules and regulations*) pamoja na Sheria Ndogo za Halmashauri (*by laws*) kama inavyoainishwa na sheria Kifungu cha Nne cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura Na. 1 ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa Kibunge wa Sheria Ndogo (*Parliament Control by Subsidiary Legislation*) ni utaratibu wa kawaida katika Mabunge ya nchi za Jumuiya ya Madola. Katika jukumu lake la udhibiti, Bunge huzingatia masharti ya sheria mama yaliyoruhusu kutungwa na sheria ndogo husika misingi mingine iliyowekwa na sheria zilizotungwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la udhibiti wa sheria ndogo pia imewekwa katika Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura Na. 1, *Interpretation of Laws Act* ya sheria za nchi ambayo imeweka mashariti maalum yanayolipa Bunge la Tanzania Mamlaka ya Udhibiti wa Sheria Ndogo zinazotungwa na Serikali pamoja na vyombo vyake.

Hata hivyo, udhibiti huo siyo wa moja kwa moja kwa sababu Bunge halina mamlaka ya kuingilia mchakato wa kutungwa kwa sheria ndogo yoyote, mpaka Shsheria ndogo inapotangazwa katika Gazeti la Serikali na kuwasilishwa humu Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge lako tukufu kufatilia ipasavyo utekelezaji wa madaraka yake ya kutunga sheria yaliyokasimiwa kwa mamlaka mbalimbali, naomba kubainisha mambo sita

yanayozingatiwa na Kamati wakati wa uchambuzi wa sheria ndogo na zinazowasilishwa mezani. Mambo hayo lengo lake ni kujiridhisha:

(i) Iwapo sheria ndogo husika inakiuka Katiba ya nchi;

(ii) Iwapo sheria ndogo husika inavuka mpaka au kwenda kinyume na masharti ya sheria inayotoa mamlaka ya kutunga sheria ndogo au sheria nyingine;

(iii) Iwapo sheria ndogo husika imezingatia misingi bora ya uandishi wa sheria;

(iv) Iwapo sheria ndogo husika inakiuka misingi ya haki za bianadam;

(v) Iwapo sheria ndogo inaendana na uhalisia wa mambo ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake, hali ya uchumi wa walengwa na viwango vya adhabu na faini; na

(vi) Kujiridhisha kuhusu maudhui ya jumla ya sheria ndogo pamoja na makosa ya uandishi au uchapaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya amelezo hayo napenda nilijulisha Bunge lako tukufu kuwa taarifa hii inahusisha uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa mezani na Serikali katika Mkutano wa Kumi na Kumi na Moja. Mifano na maelezo ya dosari mbalimbali zilizojitokeza katika sheria hizo inaonyeshwa katika sehemu zinazofuata ya taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi wa Bunge; katika Mkutano wa Kumi wa Bunge Serikali iliwasilisha mezani sheria ndogo 70, sheria ndogo hizo ziligawanyika katika mchanganuo ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja; kanuni za Wizara (*regulations*) zilikuwa kumi, matangazo (*notices*) yalikuwa 26,

amri (*orders*) zilikuwa 27, kanuni (*rules*) zilikuwa tatu, *instrument* zilikuwa mbili, na sheria ndogo za Halmashauri zilikuwa mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchangauo wa sheria ndogo ulioainishwa Kamati ilichambua na kubaini dosari mbalimbali katika kanuni tano za Wizara. Baada ya uchambuzi wa kanuni hizo, Kamati imetoa maoni na ushauri kwa lengo la kuboresha maudhui ya kanuni hizo kama inavyoonesha katika jedwali la uchambuzi ambalo limeambatishwa na taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ndogo kwenda kinyume na sheria mama au sheria nyingine za nchi. Kamati ilibaini kuwa baadhi ya kanuni zilizotungwa na Wizara (*regulations*) zinakwenda kinyume na masharti yaliyowekwa na sheria mama au sheria zingine za nchi. Kifungu cha 36(1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, kinabainisha kwamba sheria ndogo yoyote inapaswa kutokiuka masharti ya Sheria ya Bunge inayotoa mamlaka ya kutungwa kwake au sheria nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ndogo iliyobainika kuwa na dosari ya kwenda kinyume na sheria mama au sheria nyingine za nchi ni *The Oil and Gas, Revenues Management (Regulations) 2017* ambazo zimetungwa chini ya Sheria ya *The Oil and Gas, Revenues Management Act*, Sura ya 328. Uchambuzi umebaini kwa kanuni 4 (2)(b) inampa Waziri wa Fedha kujumu la kushiriki katika majadiliano ya mikataba ya kugawana mapato (*production sharing agreement*) katika sekta ndogo ya mafuta na gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaona kuwa Kanuni hii imemuongezea Waziri wa Fedha majukumu mapya ambayo hayatajwi katika kifungu cha 4 cha Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi (*The Oil and Gas Revenues and Management Act*, Sura ya 328). Kwa mujibu wa kifungu cha 5 na kifungu cha 47 cha Sheria ya Petroli ya mwaka 2015 majukumu yanayoainishwa na kanuni husika yanapaswa kutekelezwa kwa niaba ya Serikali na Waziri wa Nishati pamoja na vyombo vya Serikali vya *TPDC* na Mamlaka

ya Udhhibiti wa Shughuli wa Petroli katika Mkondo wa Juu (*PURA*). Majukumu haya hayaingiliani na yale ya Waziri wa Fedha chini ya Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na gesi (*The Oil and Gas Revenues and Management Act*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kanuni ya 4(2)(b) ya Kanuni hizi inaenda kinyume ya masharti yaliyowekwa na kifungu cha 36(1) cha Sheria ya Tafsiri, ambacho kinaelekeza kwamba sheria ndogo haipaswi kwenda kinyume na vifungu vya Sheria Mama vinavyoianzisha au sheria yoyote ya nchi. Hivyo, mantiki ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria, kanuni hiyo ya 4(2) (b) ni batili kwa kiwango inachokidhana na Sheria ya Petroli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Sheria Ndogo (*The Mining Local Content Regulations 2016*) ambayo imetungwa chini ya Sheria ya *Mining Act*, Sura ya 123 na kubaini kuwa ina vifungu vinavyokwenda kinyume na Sheria Mama (Sheria ya Madini 2010) kama ilivyorekebisha mwaka 2017. Kamati ilibaini dosari katika kanuni ya 3 inayotoa tafsiri ya neno kampuni ya mzawa au wazawa (*Indigenous Tanzanian Company*) kuwa ni ile inayomilikiwa na kwa asilimia 51 na Watanzania au Mtanzania, na ina asilimia 80 ya Watanzania katika nafasi ya utendaji wa juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri inayotolewa katika kanuni hii haipo katika Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na kama ilivyorekebisha na ni kinyume na kifungu cha 39(1) cha Sheria ya Tafsiri, Sura namba 1, kinachoelekeza kuwa, maneno yanayotumika katika sheria ndogo yanapaswa kuwa na maana sawa na yale yaliyotumika katika sheria mama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, tafsiri hiyo haipo katika Sheria ya Makampuni Sura ya 212 ambayo ndiyo sheria mama inayosimamia masuala ya makampuni nchini. Utaratibu wa kuanzisha tafsiri mpya ya maneno ni vema ukaanzia katika sheria mama au sheria nyingine za nchi ambazo ni mahsus kwa jambo fulani. Hii itasaidia kuondoa uwezekano wa kuwa na mkanganyiko katika tafsiri za maneno mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili sheria ndogo kuwa na makosa ya uandishi katika majedwali yaani kutorejea kanuni sahihi, kurejea kanuni ambazo hazipo, kutorejea kabisa kanuni na maudhui ya jedwali kutofautiana na vifungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makosa ya uandishi yamebainika katika sheria ndogo ya *The Mining Local Content Regulations* ya mwaka 2018, ambayo imetungwa chini ya Sheria ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama zilivyo sheria nyingine sheria hii pia ina majedwali ambayo yanaweka ufafanuzi wa kanuni mbalimbali katika ya sheria ndogo hii. Hata hivyo, Kamati imebaini dosari katika rejea za Kanuni zinazoanzisha majedwali hayo. Kwa mfano, jedwali la kwanza la kanuni hizi zimerejea kuanzishwa chini ya kanuni ya 10(1) ambayo maudhui yake ni tofauti kabisa na yale yanayoainishwa katika jedwali hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba rejea sahihi iliyopaswa kuwekwa katika jedwali hili ni kanuni ya 11(1) ambayo ndiyo yenye maudhui sahihi ya jedwali la kwanza la Kanuni hii na si Kanuni ya 10(1).

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati ulibaini pia Sheria Ndogo ya *The Mining (Mineral Beneficiation) Regulations, 2018* ambazo zimetungwa chini *The Mining Act* nayo ina mapungufu ya katika uandishi wa jedwali ambayo yote haya ni kinyume cha kifungu cha 25(2) cha Sheria ya Tafsiri ambacho kinatambua majedwali kuwa ni sehemu ya sheria. Tusipoweza kuyaweka vizuri kwa rejea hizo inakuwa inaleta mkanganyiko katika utumiaji wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kuchambua kanuni kuhusu *Local Content* kwenye Sekta ya Madini, hususani *The Mining (Local Content) Regulations, 2018 (GN. 3/2018)*, Kamati ilibaini kwamba tafsiri ya maneno *Indigenous Tanzanian Company* na *Indigenous Tanzanian Bank, i.e. a bank that has one hundred percent Tanzanian or majority*

Tanzanian shareholding, iliyotumika katika kanuni hizo ina ukakasi. Pamoja na nia njema ya Waziri wa Madini ya kuweka tafsiri hizo, utekelezaji wake una changamoto na unaweza kuwa na matokeo hasi kwa kampuni kama *PUMA Energy Tanzania*, ambapo Serikali inamiliki asilimia 50 ya hisa zote na kwa benki ya *NBC Limited* ambapo Serikali inamiliki asilimia 15 ya hisa zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa tafsiri *Indigenous Tanzanian Company or Indigenous Tanzanian Bank* tafsiri hiyo inaziangua taasisi hizo katika shabaha iliyokusudiwa na Kanuni hizo. Sheria ndogo hiyo haitambui umiliki wa Serikali wa hisa katika benki ya *NBC* na katika kampuni ya *PUMA* kuwa ni umiliki wa Serikali kwa niaba ya Watanzania na hivyo upo uwezekano mkubwa wa kuzikosesha kampuni hizo fursa ya kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi zinazolengwa na Sheria Ndogo hiyo. Halikadhalika benki na taasisi za fedha nyingi zilizosajiliwa hapa nchini ambazo hazimilikiwi na Watanzania ama kwa asilimia 100 au kwa hisa nyingi zitakosa fursa ya kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za kiuchumi katika sekta ya madini. Kamati haiamini kwamba haya ndio yalikuwa madhumuni ya kutungwa kwa sheria ndogo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge; katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge Serikali iliwasilisha mezani sheria ndogo 121 ambazo zimegawanyika katika makundi yafuatayo:-

Kanuni za Wizara zilikuwa 50; matangazo yalikuwa 36; *orders* zilikuwa 12, *rules* tatu na sheria ndogo za Halmashauri zilikuwa 20.

Baada ya uchambuzi uliofanywa na Kamati imebainika zipo dosari mbalimbali katika sheria ndogo kumi na imetoa mapendekezo ya kufanyiwa marekebisho na kuziboresha sheria ndogo hizo. Mtaona jedwali lililoambatanishwa na taarifa hii kama inavyopendekezwa na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo uchambuzi wa sheria ndogo za Baraza la Sanaa la Taifa, 2018 haukuingizwa katika taarifa hii baada ya Kamati kubaini dosari nyingi sana za kimsingi katika Kanuni hizo. Tarehe 11 Septemba, 2018 Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe (Mbunge), alipokutana na Kamati kujibu hoja za uchambuzi katika Kanuni za Baraza la Sanaa la Taifa, 2018 (*GN No.43/2018*), alikiri uwepo wa dosari hizo. Hivyo aliomba muda wa kuzipitia upya kanuni hizo ili kurekebisha dosari zilizobainika na kuahidi kuwasilisha tena kwenye Kamati wakati wa vikao vya Kamati mwezi Oktoba, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa madhumuni ya kulitaarifu Bunge kuhusu uchambuzi uliofanyika, baadhi ya dosari zilizobainika katika kanuni hizo zinafafanuliwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ndogo kwenda kinyume na masharti ya Katiba (kama ilivyorekebisha); Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiyo sheria mama na ndiyo msingi mkuu wa sheria zote za nchi zinazopaswa kutungwa pasipo kuwa na maudhui yanayokinzana nayo. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa sheria ndogo ya *The Urban Planning (Appeals), Regulations, 2018* ambayo imetungwa chini ya Sheria ya *The Urban Planning Act*, Sura ya 355 ina maudhui yanayoingilia mhimili wa Mahakama. Dosari hiyo imebainika katika kanuni ya 5(2) ambayo inaweka sharti la lazima kwa Mahakama mara baada ya kutoa uamuzi, kuwasilisha nakala tatu za hukumu kwa Mamlaka ya Mipango Miji zinazoainisha sababu za kufikia uamuzi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu uliowekwa na kanuni hii unaingilia mamlaka ya Mahakama ambayo ni kinyume kabisa na Ibara ya 107(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na taratibu za kimahakama zilizoanzishwa kwa mujibu wa sheria za nchi. Ikumbukwe kuwa chombo kinachoweza kuamuru Mahakama kufanya jambo

lolote kwa uamuzi iliyotoa ni Mahakama iliyo juu yake na si chombo au taasisi nyingine nje ya mfumo wa mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 36(1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, kinaelekeza kwamba sheria ndogo haipaswi kuwa na vifungu vinavyokinzana na sheria mama iliyolanzisha au sheria nyingine yoyote ya nchi; na ikitokea kuwa sheria ndogo ina vifungu vinavyokinzana, vifungu hivyo kinzani vitahesabiwa kuwa ni batili kwa kiwango ambacho vifungu hivyo vinakinzana na sheria mama au sheria nyingine yoyote ya nchi. Hivyo kutokana na kanuni ya 5(2) kuweka masharti yanayovuka mipaka ya sheria inayotoa mamlaka ya kutungwa kwake, kanuni hiyo inahesabika kuwa ni batili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema vyombo vinavyokasimiwa mamlaka ya kutunga sheria ndogo vikazingatia misingi ya mgawanyo wa madaraka katika mihimili ya nchi wakati wa utungaji wa sheria ndogo. Hii itasaidia kuondoa migongano na hatimaye kuwezesha mihimili ya nchi kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, sheria ndogo kwenda kinyume na sheria mama au sheria nyingine za nchi. Kamati imebaini pia kanuni za *The Urban Planning (Appeals), Regulations, 2018* zilizoanzishwa chini ya Sheria ya *Urban Planning Act*, Sura ya 355 ina masharti yanayokinzana na yale yaliyowekwa na sheria nyingine za nchi. Kanuni hiyo ya 4(b)(ii) na (iii) za kanuni hii inaweka sharti kwamba mtu anayetaka kukata rufaa dhidi ya Mamlaka ya Mipango Miji, anapaswa kuwasilisha kwa Mamlaka ya Mipango Miji, orodha ya nyaraka anazotarajia kutumia katika rufaa yake pamoja na nyaraka ambazo hakuwahi kuziwasilisha kwa Mamlaka ya Mipango Miji katika hatua ya usikilizaji wa shauri la awali dhidi ya mamlaka hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeona utaratibu huu si sahihi kwa kuwa katika hatua hii mrufani hapaswi kuwasilisha ushahidi wa aina yoyote kwa mrufaniwa mpaka pale ambapo kesi yake itakapokuwa imefikishwa

Mahakamani. Aidha, katika hatua ya rufaa mrufani hapaswi kuwasilisha ushahidi mpya mpaka pale tu Mahakama itakapoonna kuna haja ya kufanya hivyo ili kufikia uamuzi sahihi. Hayo ndiyo matakwa ya sheria ya mwenendo wa kesi za madai, Sura ya 33 (*The Civil Procedure Code, Cap. 33*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukinzana kwa kanuni na sheria mama au sheria nyingine za nchi kama nilivyowaeleza ni kinyume na masharti ya kifungu cha 36(1) cha Sheria ya Tafsiri. Nisingependa niyarudie hayo, kwa hiyo kuna utata katika sehemu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo limebainishwa na Kamati, masharti ambayo yanakinzana na sheria mama ni kanuni ya *The Urban Planning Building Regulations, 2018* ambayo imetungwa chini ya sheria ya *Urban Planning Act*, Sura ya 355.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini dosari katika kanuni ya 3 ambayo inatoa tafsiri ya neno *vehicle* ikihusisha vitu kama mkokoteni wa kuvutwa na ng'ombe, baiskeli ya matairi mawili, baiskeli ya matairi matatu. Tafsiri hii ni kinyume na ile iliyotolewa na Sheria ya Usalama Barabarani kuhusiana na neno *vehicle* ambayo haijabainisha vifaa hivyo kuwa ni sehemu ya vyombo vya moto. Halikadhalika masuala ya vyombo vya moto kwa namna yoyote ile hayahusiani na maudhui ya kanuni hii inayohusu masuala ya mipango miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni hiyo ya 3 inakinzana na kifungu cha 36(1) na kifungu cha 39(1) cha Sheria ya Tafsiri za Sheria ambavyo vinaeleza kwamba maneno yatakayotumika katika sheria ndogo yanapaswa kuwa na maana sawa na yale ambayo yanatumika katika sheria mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dosari ya kwenda kinyume na masharti ya sheria mama pia iligundulika katika sheria ndogo ya *The Urban Planning (Building) Regulations, 2018* ambazo zimetungwa chini ya sheria hiyo hiyo ya *The Urban*

Planning Act, Sura ya 355. Kamati ilifanya uchambuzi wa Kanuni hii na kubaini kuwa Kanuni ya 3 inatoa tafsiri ya neno jengo (*building*) kuwa inahusisha pia mabango ya matangazo na minara ya simu kinyume na tafsiri iliyotolewa na sheria mama chini ya kifungu cha 2 ambacho pamoja na masuala mengine hakijafanua masuala ya mabango ya matangazo na minara ya simu. Kwa msingi huo huo wa kukiuka kifungu cha 36(1) na kifungu cha 39(1) cha Sheria ya Tafsiri Kanuni hiyo ni batili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria Ndogo kuwa na makosa ya uandishi katika majedwali (kutorejea kanuni sahihi, kurejea kanuni ambazo hazipo, kutorejea kabisa kanuni na maudhui ya jedwali kutofautiana na vifungu vya kanuni). Katika uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge, Kamati ilibaini dosari mbalimbali za uandishi katika majedwali ikiwa ni pamoja na kutorejea kanuni sahihi zilizoanzisha majedwali husika kurejea kanuni ambazo hazipo na maudhui ya jedwali kuwa tofauti na vifungu vya kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dosari za uandishi wa majedwali zilibainika pia sheria ndogo za *The Urban Planning (Building) Regulations*, zilizotungwa chini ya Sheria ya *The Urban Planning Act*. Kamati ilibaini dosari katika Fomu Na. 18 na Na. 19 katika jedwali la nne. Fomu hizo zinarejea kuanzishwa chini ya kanuni ya 77(1)(r) ambayo haipo katika sheria hii.

Kwa mujibu wa kifungu cha 25 (2) cha Sheria ya Tafsiri majedwali yote ni sehemu ya sheria husika, na lengo lake husaidia kufanua zaidi maudhui ya kifungu husika katika sheria. Hivyo kwa kanuni hizo zilizobainika kutoweka rejea sahihi ya vifungu katika majedwali husika, si tu italeta changamoto ya usomaji bali pia itafanya majedwali hayo kukosa uhalali wake wa kuwepo katika kanuni kwa kuwa hayajaanzishwa na vifungu sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sheria ndogo kutozingatia misingi ya uandishi wa sheria; Kamati ilifanya

uchambuzi wa sheria ndogo za *The Urban Planning (Urban Farming) Regulations, 2018* zilizoanzishwa chini ya Sheria ya *The Urban Planning Act*. Katika uchambuzi huo Kamati imebaini dosari za uandishi wa sheria, ambazo mwishoni mwa sheria ndogo hii kumewekwa ufafanuzi wa maneno mbalimbali pasipo kuyaweka katika kanuni ya 2 ambayo ni mahsusi kwa ajili ya kutoa tafsiri ya maneno mbalimbali yanayotumika katika kanuni zenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ndogo nyingine iliyobainika kuwa na dosari za uandishi ni *The Electronic and Postal Communications (Sim Card Registration) Regulations, 2018* ambazo zinaanzishwa chini ya Sheria ya *The Electronic and Postal Communications Act* Sura 306 ya sheria za nchi. Sheria ndogo hii pia imebainika kuweka maelezo ya ziada kuhusu sifa za picha zinazopigwa, mashine za kielektroniki zinazotumika katika usajili wakati wa kusajili laini za simu pasipo kuyaweka maelezo hayo katika kifungu chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huu ni kinyume na uandishi wa sheria, kwa kuwa maneno yote yanayotolewa tafsiri yanapaswa kuwa katika kifungu cha tafsiri au katika kifungu chochote kinachoelezea jambo mahsusi na si kuandikwa peke yake pasipo kuwa na rejea ya kanuni husika. Aina hii ya uandishi inaweza kuleta changamoto pale ambapo mtu anahitaji kufanya rejea ya maneno hayo kwa kuwa hayana kifungu kinachoyapa nguvu ya sheria ndogo kuwepo katika kanuni hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya jumla; Kamati inazishauri mamlaka zote ambazo zimekasimiwa na Bunge madaraka ya kutunga sheria ndogo, kuzingatia kikamilifu ushirikishwaji wa wadau wanaolengwa na sheria ndogo yoyote ili kupunguza changamoto mbalimbali zinazoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa sheria ndogo hizo. Kamati inashauri Serikali iongeze idadi ya rasilimali watu katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu hasa upande wa Mwandishi Mkuu wa Sheria na vitengo vingine ambavyo vinahusika na upitishaji wa sheria ndogo hizi ili kuhakikisha makosa yanayojitokeza mara kwa mara

katika sheria ndogo yanarekebishwa kabla ya sheria ndogo hizo kuchapishwa katika Gazeti la Serikali na kuanza kutumika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri mamlaka zinazopewa jukumu la kutunga sheria ndogo kufanya kazi kwa karibu sana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakati wa utungaji wa sheria ndogo kwa lengo la kuondoa dosari mbalimbali zinazojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kuzifanyia marekebisho sheria ndogo zote zenye dosari. Baada ya marekebisho hayo kufanyika na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali, Sheria Ndogo hizo ziwasilishwe tena Bungeni kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sheria ndogo ya *The Mining (Local Content) Regulations, 2018 (GN No. 3/2018)*, Kamati inashauri tafsiri ya maneno *Indigenous Tanzanian Company* na *Indigenous Tanzania Bank* ifanyiwe marekebisho ili kuondoa masharti hasi kwenye kampuni ambazo Serikali inamiliki hisa chini ya asilimia 51. Kwa upande wa maudhui ya huduma za kifedha, mabadiliko hayo yakifanyika yatawezesha kupanua wigo wa ushiriki wa benki na taasisi za fedha zilizosajiliwa hapa nchini na hivyo kuweza kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja; dosari ya uandishi wa majedwali ikilinganishwa na vifungu vya sheria;

KWA KUWA katika uchambuzi wa Kamati imebainika kuwa baadhi ya sheria ndogo zina dosari mbalimbali katika majedwali kuhusu vifungu vinavyoanzisha majedwali husika.

NA KWA KUWA kwa mujibu wa kifungu cha 25(2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinabainisha kwamba majedwali ni sehemu ya sheria.

KWA HIYO BASI Bunge linaazimia kwamba Wizara ambazo sheria ndogo zake zimebainika kuwa na dosari

katika majedwali zifanyiwe marekebisho ili kuondoa dosari hizo.

Kukinzana na masharti ya sheria mama au sheria nyingine za nchi:-

KWA KUWA baadhi ya sheria ndogo zilizofanyiwa uchambuzi na Kamati zilibainika kuwa na vifungu vinavyokinzana na masharti ya sheria mama au sheria nyingine za nchi.

NA KWA KUWA kukinzana huko ni kwenda kinyume na masharti ya kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinachotoa sharti kwa sheria ndogo zinazokwenda kinyume na masharti ya sheria zinakataza kutokwenda kinyume na sheria mama.

NA KWA KUWA kukinzana huko kunaifanya kanuni husika kuwa batili kwa kiwango kinachokinzana.

KWA HIYO BASI Bunge linaazimia kwamba, Wizara zinazohusika kufanya marekebisho katika sheria ndogo hizo, ili kuondoa vifungu vinavyokwenda kinyume na masharti ya sheria mama au sheria nyingine ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na Bunge lako tukufu kwa kuweka utaratibu unaowezesha Kamati hii kuwasilisha taarifa zake mara mbili kwa mwaka, maana ni sheria hizi zinagusa wananchi katika maisha yao ya siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Jenista Mhagama (Mbunge), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana na Wenye Ulemavu kwa kuendelea kuweka utaratibu mzuri ambao uliwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, ninawashukuru Mawaziri, Naibu Mawaziri wa sekta mbalimbali kwa kufika mbele ya kamati na kujibu hoja zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati. Kwa heshima na

taadhima naomba niwatambue kwa jinsi walivyofika mbele ya kamati; Mheshimiwa Dkt. Harison Mwakyembe (Mbunge) - Waziri wa Habari na Utamaduni, Mheshimiwa William Lukuvi(Mbunge) - Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji (Mbunge)- Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Atashasta Nditiye(Mbunge) - Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya(Mbunge) - Naibu Waziri Viwanda, Bisahara na Uwekezaji na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo (Mbunge) - Naibu Waziri wa Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee niwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri wanayochambua sheria hizi zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na wa Kumi na Moja na hatimaye kufanikisha kazi hii. Kwa heshima naomba Kumbukumbu Rasmi ya *Hansard* iyachukue majina yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Ndugu Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge, kwa ushirikiano wanaoupatia Kamati hii ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Aidha, nimshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Athuman Hussein akisaidiwa na Bi. Angelina Sanga, Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Kamati za Bunge kwa usimamizi mzuri wa shughuli za Kamati.

Mwisho, lakini si kwa umuhimu. Niwashukuru Makatibu wa Kamati ya Sheria Ndogo, Ndugu Yona Kirumbi, Ndugu Angela Shekifu, Ndugu Stanslaus Kagisa na Ndugu Mkuta Masoli, wakisaidiwa na Ndugu Paul Chima kwa kuratibu vyema Shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO TAARIFA
KUHUSU UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA
KATIKA MKUTANO WA KUMI NA KUMI NA MOJA WA BUNGE
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI

1.1 Maelezo ya Awali

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, nakushukuru kwa kutoa idhini kwa Kamati yangu iweze kuwasilisha **Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo** kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Mezani na Serikali katika Mkutano wa Kumi na Kumi na Moja wa Bunge.

1.1.1 **Mheshimiwa Spika**, natumaini kuwa Taarifa hii itawezesha Waheshimiwa Wabunge kutoa ushauri zaidi kuhusu Sheria Ndogo zilizochambuliwa na Kamati pamoja na Sheria Ndogo nyingine ambazo zinatumika. Pia, Kamati inaamini kuwa Serikali itayafanyia kazi mapendelezo yaliyomo katika Taarifa hii na maoni yatakayotolewa na Wabunge ili kuondoa dosari zilizobainika kutokana na uchambuzi wa Kamati.

1.2 Madaraka ya Kutunga Sheria

1.2.1 **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 64 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, imelipa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mamlaka yote ya kutunga Sheria juu ya mambo yote ya Muungano na yasiyo ya Muungano yahusuyo Tanzania bara. Aidha, Ibara ya 97 ya Katiba imeweka utaratibu ambao unapaswa kuzingatiwa na Bunge katika kutekeleza madaraka yake ya kutunga Sheria.

1.2.2 **Mheshimiwa Spika**, pamoja na mamlaka lililonayo Bunge la kutunga Sheria, kwa hali halisi Bunge halina muda wa kutosha wa kutunga Sheria kuhusu masuala yote ambayo utekelezaji wake unahitaji uwepo wa Sheria. Kutokana na hali hiyo ndiyo maana Ibara ya 97 (5) ya Katiba inalipa Bunge

uwezo wa kukasimu madaraka yake ya kutunga Sheria kwa mtu yeyote au idara yoyote ya Serikali. Sheria zinazotungwa kwa utaratibu huo zinaitwa Sheria Ndogo (*subsidiary legislation/delegated legislation*) ambazo hujumuisha Kanuni mbalimbali (*rules and regulations*) pamoja na Sheria Ndogo za Halmashauri (*By-Laws*) kama zinavyotafsiriwa chini ya Kifungu cha 4 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura 1

1.3 Udhhibiti wa Kibunge wa Sheria Ndogo

1.3.1 **Mheshimiwa Spika**, Udhhibiti wa Kibunge wa Sheria Ndogo (*Parliamentary Control Over Subsidiary Legislation*) ni utaratibu wa kawaida katika Mabunge ya nchi za Jumuiya ya Madola. Utaratibu huu unalenga kuliwezesha Bunge kujiridhisha kikamilifu kuhusu utekelezaji wa madaraka ya kutunga sheria lililoyakasimu kwa mamlaka nyingine. Katika jukumu lake la udhibiti, Bunge huzingatia masharti ya Sheria Mama iliyoruhusu utungwaji wa Sheria Ndogo husika na misingi mingine iliyowekwa na Sheria zilizotungwa na Bunge.

1.3.2 **Mheshimiwa Spika**, utaratibu huu umezungumziwa na waandishi wengi wakiwemo Jain and Jain katika kitabu chao kiitwacho *The Principles of Administrative law* (2007) ukurasa wa 175 wanaposema;

Naomba kunuku; *".....Since it is the legislature which grants legislative power to the administration, it is primarily its responsibility to ensure the proper exercise of delegated legislative power, to supervise and control the actual exercise of this power and ensure against the danger of its objectionable, abusive and unwarranted use by the administration."* **Mwisho wa kunukuu**

Kwa tafsiri isiyo rasmi tunaweza kusema, kwa kuwa Bunge limetoa madaraka ya utungaji sheria kwa vyombo vingine, wajibu wake mkubwa ni kuhakikisha kunakuwepo matumizi sahihi ya madaraka yaliyo kasimiwa ya kutunga sheria, kusimamia na kudhibiti matumizi ya mamlaka hayo ili kuondoa uwezekano wa vyombo hivyo kutumia vibaya madaraka yaliyokasimiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo utaratibu wa kuchambua Sheria Ndogo na kutoa Taarifa Bungeni kunaliwezesha Bunge kujiridhisha na namna madaraka yake yaliyo kasimiwa kwa Taasisi za Serikali yanavyotumika.

1.3.3 **Mheshimiwa Spika**, suala la udhibiti wa Sheria ndogo pia limewekwa katika Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 (*The Interpretation of Laws Act, Cap 1 R.E. 2002*) ambayo imeweka masharti maalum yanayolipa Bunge la Tanzania mamlaka ya udhibiti wa Sheria Ndogo zinazotungwa na Serikali pamoja na vyombo vyake. Hata hivyo udhibiti huo siyo wa moja kwa moja kwa sababu Bunge halina mamlaka ya kuingilia mchakato wa kutungwa kwa Sheria Ndogo yoyote mpaka Sheria Ndogo inapotangazwa katika Gazeti la Serikali na kuwasilishwa Bungeni.

1.3.4 **Mheshimiwa Spika**, kutokana na umuhimu wa kufanya Udhibiti wa Utungaji wa Sheria Ndogo, Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge ikisomwa kwa pamoja na Nyongeza ya Nane ya Kanuni hizo imeanzisha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kama ilivyo kwa Mabunge mengine katika Nchi za Jumuiya ya Madola. Kamati hii imepewa majukumu kwa mujibu wa Kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 ambayo ni, kuchambua Sheria Ndogo ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi.

1.4 **Namna ambavyo Kamati inatekeleza majukumu yake**

1.4.1 **Mheshimiwa Spika**, wajibu wa msingi wa Kamati kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, kama ambavyo imeelezwa awali, ni kufanya uchambuzi wa Sheria Ndogo ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi. Sheria Ndogo hutungwa kwa lengo la kuwezesha utekelezaji wa Sheria Mama katika masuala mbalimbali. Kwa mujibu wa Kifungu cha 4 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria¹, Sheria Ndogo zinajumuisha:-

¹Toleo la 2002

- a) Amri (*Orders*)
- b) Matamko (*Proclamations*)
- c) Kanuni za Taasisi (*Rules*)
- d) Kanuni za Mahakama (*Rules of Court*)
- e) Kanuni za Wizara (*Regulations*)
- f) Taarifa (*Notices*)
- g) Sheria Ndogo za Halmashauri (*By – Laws*)
- h) Hati (*Instruments*)

1.4.2 Kufanya Uchambuzi wa Sheria Ndogo zote zilizowasilishwa Mezani katika Mkutano wa Bunge uliotangulia

1.4.2.1 **Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 38 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, kinaweka sharti kwamba, Sheria Ndogo yoyote iliyotungwa na mamlaka nyingine nje ya Bunge ni lazima iwasilishwe Bungeni ndani ya siku sita (6) ya vikao (*six sitting days*) vya Mkutano wa Bunge unaofuata baada ya Sheria kutangazwa katika Gazeti la Serikali. Baada ya Bunge kupokea Sheria Ndogo hiyo, Kamati hufanya uchambuzi wake na baadae kutoa maoni na ushauri kuhusu yaliyomo katika Sheria Ndogo husika. Kifungu hicho kimeainisha hatua zinazoweza kuchukuliwa na Bunge. Hatua hizo ni:-

i) Kutoa Azimio la kuzuia kutumika kwa Sheria Ndogo husika (*disallowance resolution*)

Kifungu cha 38 (2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, kinaruhusu Bunge kupitisha Azimio la kuzuia kutumika kwa Sheria Ndogo endapo litajiridhisha na maoni ya Kamati kwamba, Sheria Ndogo haikidhi masharti na matakwa ya Katiba, Sheria Mama au Sheria nyingine ya nchi. Aidha, Bunge linaweza kuchukua hatua hii endapo litajiridhisha kuwa Sheria Ndogo fulani haikuwasilishwa Bungeni ndani ya siku sita (6) ya vikao (*six sitting days*) vya Bunge baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali kwa kuwa kutofanya hivyo ni kinyume na Kifungu cha 38 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria.

ii) **Kufanya marekebisho au kuibadili Sheria Ndogo yoyote kufuatia Azimio la kuzuia kutumika kupitishwa na Bunge (*amendment and substitution*)**

Kifungu cha cha 38 (4) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, kinaliruhusu Bunge kupitisha Azimio muda wowote ili kurekebisha au kubadili Sheria Ndogo yoyote iliyozuiwa kutumika kwa masharti yanayopatikana katika Kifungu cha 38 (2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria.

1.4.3 Kufanya Uchambuzi wa Sheria Ndogo yoyote ambayo inatumika

1.4.3.1 **Mheshimiwa Spika**, kwa madhumuni ya utekelezaji mpana wa Kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati inaweza kufanya uchambuzi wa Sheria Ndogo yoyote kwa kuzingatia vipaumbele inavyojiweka.

1.4.3.2 **Mheshimiwa Spika**, kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge lako tukufu kufuatilia ipasavyo utekelezaji wa madaraka yake ya kutunga sheria yaliyokasimiwa kwa mamlaka mbalimbali, naomba kubainisha mambo sita yanayozingatiwa na Kamati wakati wa uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowekwa Mezani. Mambo hayo ni:-

a) Iwapo Sheria Ndogo husika inakiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

b) Iwapo Sheria Ndogo husika inavuka mipaka au kwenda kinyume na masharti ya Sheria inayotoa mamlaka ya kutunga Sheria Ndogo au Sheria nyingine yoyote;

c) Iwapo Sheria Ndogo husika imezingatia misingi bora ya uandishi wa Sheria (*drafting principles*);

d) Iwapo Sheria Ndogo husika inakiuka misingi ya haki za binadamu;

e) Iwapo Sheria Ndogo inaendana na uhalisia wa mambo ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake, hali ya uchumi wa walengwa na viwango vya adhabu na faini; na

f) Maudhui ya jumla ya Sheria Ndogo pamoja na makosa ya uandishi na uchapaji.

1.4.3.3 **Mheshimiwa Spika**, baada ya kukamilisha uchambuzi wake kwa kuzingatia masuala yaliyotajwa, Kamati hubaini hoja mbalimbali zinazolenga kupata ufafanuzi katika maeneo ya Sheria Ndogo zenye dosari. Hoja hizo huwasilishwa Serikalini kwa lengo la kupendekeza marekebisho au kufutwa kwa kifungu chochote ambacho kina dosari zilizobainishwa na Kamati. Kila Wizara inayoguswa na hoja zinazoibuliwa na Kamati, huwajibika kufika mbele ya Kamati na kutoa maelezo kuhusiana na Sheria Ndogo ambayo inaisimamia.

1.4.3.4 **Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo napenda nilijulishe Bunge lako Tukufu kuwa Taarifa hii inahusisha uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mikutano miwili ya Bunge yaani, Mkutano wa Kumi na ule wa Kumi na Moja wa Bunge. Mifano na maelezo ya dosari mbalimbali zilizojitokeza katika Sheria ndogo hizo inaonyeshwa katika sehemu zinazofuata katika Taarifa hii.

2.0 UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA KATIKA MKUTANO WA KUMI WA BUNGE

2.1 **Mheshimiwa Spika**, Katika Mkutano wa Kumi wa Bunge Serikali iliwasilisha Mezani Sheria Ndogo Sabini (70). Sheria Ndogo hizo ziligawanyika katika mchanganuo ufuatao:-

- a) Kanuni za Wizara (*Regulations*) – 10
- b) Matangazo (*Notices*) – 26
- c) Amri (*Orders*) – 27
- d) Kanuni (*Rules*) - 3
- e) Hati (*Instruments*) - 2
- f) Sheria Ndogo za Halmashauri (*By – Laws*) – 2

2.2 **Mheshimiwa Spika**, katika mchanganuo wa Sheria Ndogo ulioainishwa, Kamati ilichambua na kubaini dosari mbalimbali katika Kanuni Tano (5) za Wizara. Baada ya Uchambuzi wa Kanuni hizo Kamati imetoa maoni na ushauri kwa lengo la kuboresha maudhui ya Kanuni hizo kama inaonekana katika **JEDWALI LA UCHAMBUZI** lililoambatishwa. Kwa minajili ya kulitaarifu Bunge kuhusu uchambuzi uliofanyika, baadhi ya dosari zilizobainika katika Kanuni hizo ni kama ifuatavyo:-

2.2.1 **Sheria Ndogo kwenda kinyume na Sheria Mama au Sheria nyingine za Nchi.**

2.2.1.1 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa, baadhi ya Kanuni zilizotungwa na Wizara (*Regulations*) zinakwenda kinyume na masharti yaliyowekwa na Sheria Mama au na Sheria Nyingine za Nchi. Kifungu cha 36 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria ambacho kinabainisha kwamba, Sheria Ndogo yoyote inapaswa kutokiuka masharti ya Sheria ya Bunge inayotoa mamlaka ya kutungwa kwake au Sheria nyingine yoyote.²

2.2.1.2 **Mheshimiwa Spika**, Sheria Ndogo iliyobainika kuwa na dosari ya kwenda kinyume na Sheria Mama na Sheria nyingine za Nchi ni *The Oil and Gas (Revenues Management) Regulations, 2017* ambazo zimetungwa chini Sheria ya *The Oil and Gas Revenues Management Act*, Sura ya 328. Uchambuzi umebaini kuwa **Kanuni ya 4(2) (b)** ya Kanuni hizi inampa Waziri wa Fedha jukumu la kushiriki katika majadiliano ya Mikataba ya Kugawana Mapato (*Production Sharing Agreements*) katika Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia nchini.

2.2.1.3 **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona kuwa Kanuni hii imemuongezea Waziri wa Fedha Majukumu mapya ambayo hayatajwi katika **Kifungu cha 4** cha Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi (*The Oil and Gas Revenues Management Act*), Sura ya 328. Kwa mujibu wa **Kifungu cha**

²Sura ya 1 Toleo la 2002

5 na 47 vya Sheria ya Petroli ya mwaka 2015 majukumu yanayoainishwa na Kanuni husika yanapaswa kutekelezwa na Waziri wa Nishati, TPDC na PURA kwa niaba ya Serikali. Majukumu haya hayaingiliani na yale ya Waziri wa Fedha chini ya Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi (*The Oil and Gas Revenues Management Act*).

2.2.1.4 **Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa, **Kanuni ya 4(2) (b)** ya Kanuni hizi inaenda kinyume na masharti yaliyowekwa katika **Kifungu cha 36(1)** cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria (*Interpretation of Laws Act*) Sura ya 1 ambacho kinaelekeza kwamba, Sheria Ndogo haipaswi kwenda kinyume na vifungu vya Sheria Mama vinavyoanzisha au Sheria yoyote ya Nchi.

Hivyo kwa mantiki ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Kanuni hiyo ya **Kanuni ya 4(2) (b)** ni batili kwa kiwango inachokinzana na Sheria ya Petroli ya mwaka 2015 na Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi Sura 328.

2.2.1.5 **Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Sheria Ndogo ya *The Mining (Local Content) Regulations, 2018*, ambayo imetungwa chini Sheria ya *The Mining Act*, Sura ya 123 na kubaini kuwa ina vifungu vinavyokwenda kinyume na Sheria Mama. Kamati ilibaini dosari katika **Kanuni ya 3** inayotoa tafsiri ya neno Kampuni ya mzawa/wazawa (***Indigenous Tanzanian Company***) kuwa ni ile inayomilikiwa kwa asilimia 51 na Mtanzania/Watanzania na ina asilimia 80 ya watanzania katika nafasi za watendaji wa juu.

2.2.1.6 **Mheshimiwa Spika**, tafsiri inayotolewa katika Kanuni hii haipo katika katika Sheria ya Makampuni Sura, 212 ambayo ndiyo Sheria Mama inayosimamia masuala yote ya Makampuni Nchini. Utaratibu wa kuanzisha tafsiri mpya ya maneno ni vema ukaanzia katika Sheria Mama au Sheria nyingine ya nchi ambayo ni mahususi kwa jambo fulani, hii itasaidia kuondoa uwezekano wa kuwa mchanganyiko wa tafsiri za maneno mbalimbali.

2.2.2 Sheria Ndogo kuwa na makosa ya uandishi katika Majedwali (Kutorejea Kanuni sahihi, kurejea Kanuni ambazo hazipo, kutorejea kabisa Kanuni na Maudhui ya Jedwali tofautiana na Vifungu)

2.2.2.1 Mheshimiwa Spika, Makosa ya uandishi yamebainika katika Sheria Ndogo ya *The Mining (Local Content) Regulations, 2018*, ambayo imetungwa chini Sheria ya *The Mining Act*, Sura ya 123. Kama zilivyo sheria nyingine, sheria hii pia ina Majedwali ambayo yanaweka ufafanuzi wa Kanuni mbalimbali katika Sheria Ndogo hii. Hata hivyo Kamati imebaini dosari katika rejea za Kanuni zinazoanzisha majedwali. Kwa mfano, **Jedwali la Kwanza** la Kanuni hizi limereja kuanzishwa chini ya **Kanuni ya 10 (1)** ambayo maudhui yake ni tofauti kabisa na yale yale yanayoainishwa katika Jedwali hili. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba rejea sahihi iliyopaswa kuwekwa katika Jedwali hili ni **Kanuni ya 11 (1)** ambayo ndiyo yenye maudhui ya sahihi ya Jedwali la kwanza la Kanuni hizi.

2.2.2.2 Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati pia ulibaini pia Sheria Ndogo ya *The Mining (Mineral Beneficiation) Regulations, 2018* ambazo zimetungwa chini Sheria ya *The Mining Act*, Sura ya 123 ina mapungufu ya katika uandishi wa Jedwali. Katika Sheria Ndogo hii, Kanuni ya 11(1) inataja kuanzisha Jedwali la Tatu, hata hivyo uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Jedwali hilo halipo katika Kanuni hizi.

2.2.2.3 Mheshimiwa Spika, ni vema uandishi wa majedwali katika sheria uzingatie kurejea Kanuni sahihi zinazoanzisha majedwali husika, kwa kuwa majedwali hufafanua zaidi masharti ya utekelezaji wa Kanuni husika katika Sheria Ndogo. Hivyo kwa kutorejea vifungu sahihi sio tu inaondoa maana ya masharti ya **Kifungu cha 25 (2)** cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria ambacho kinatambua majedwali kuwa ni sehemu ya sheria, bali pia inaleta changamoto katika usomaji mzuri wa sheria husika.

2.2.2.4 Mheshimiwa Spika, wakati inachambua Kanuni kuhusu *Local Content* katika sekta ya Madini, hususani *The*

Mining (Local Content) Regulations, 2018 (GN. 3/2018), Kamati ilibaini kwamba tafsiri ya maneno "***Indigenous Tanzania Company***" na "***Indigenous Tanzanian Bank***" – ie. "***a bank that has one hundred percent Tanzanian or majority Tanzanian shareholding***" iliyotumika katika Kanuni hizo ina ukakasi. Pamoja na nia njema ya Wizara ya Madini ya kuweka tafsiri hizo, utekelezaji wake una changamoto na unaweza ukawa na matokeo hasi kwa kampuni kama Puma Energy Tanzania ambapo Serikali inamiliki asilimia hamsini (50%) ya hisa zote na kwa benki ya NBC *Limited* ambapo Serikali inamiliki asilimia kumi na tano (15%) ya hisa zote.

2.2.2.5 Sheria Ndogo hiyo haitambui umiliki wa Serikali wa hisa katika benki ya NBC na katika kampuni ya Puma kuwa ni umiliki wa watanzania na hivyo kuzikosesha kampuni hizo fursa ya kushiriki kiuchumi katika sekta ya madini. Halikadhalika benki na taasisi za fedha nyingi zilizosajiliwa hapa nchini ambazo hazimilikiwi na watanzania kwa asilimia mia moja au kwa hisa nyingi zitakosa fursa ya kushiriki kwenye sekta ya madini. Kamati haiamini kwamba haya ndio yalikuwa madhumuni ya kutungwa kwa Sheria Ndogo hiyo.

3.0 UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA KATIKA MKUTANO WA KUMI NA MOJA WA BUNGE

3.1 **Mheshimiwa Spika**, katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge mnamo tarehe 9 Aprili, 2018 Serikali iliwasilisha mezani Sheria Ndogo Mia Moja Ishirini na Moja (121), ambazo zimegawanyika katika makundi yafuatayo:-

- a) Kanuni za Wizara (*Regulations*) – 50
- b) Matangazo (*Notices*) – 36
- c) Amri (*Orders*) – 12
- d) Kanuni (*Rules*) - 3
- e) Sheria Ndogo za Halmashauri (*By-Laws*) – 20 (**Marekebisho mbalimbali yaliyofanyika**)

Mara baada ya kuwasilishwa kwa Sheria Ndogo hizo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo ilifanya uchambuzi na kubaini dosari mbalimbali katika Sheria Ndogo 10 kwa lengo

la kufanya marekebisho yanayolenga kuboresha Sheria Ndogo hizo kama inavyoonyeshwa katika **JEDWALI LA UCHAMBUZI** lililoambatishwa.

3.2 **Mheshimiwa Spika**, hata hivyo uchambuzi wa Kanuni ya Baraza la Sanaa la Taifa, 2018 hautaoneshwa katika Taarifa baada ya Kamati kubaini dosari nyingi katika Kanuni hii, hivyo mnamo tarehe 11 Septemba, 2018 Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Dkt. Harrison Mwakyembe (Mb) - alipokutana na Kamati kujibu hoja za kiuchambuzi katika **Kanuni za Baraza la Sanaa la Taifa, 2018 (GN Na. 43/2018)**, alikiri uwepo wa dosari hizo. Hivyo aliomba muda wa kuzipitia upya ili kurekebisha dosari zilizobainika na kuwasilisha kwenye Kamati wakati wa vikao vya mwezi Oktoba, 2018.

3.3 **Mheshimiwa Spika**, Kwa madhumuni ya kulitaarifu Bunge kuhusu uchambuzi uliofanyika, baadhi dosari zilizobainika katika Kanuni hizo zinafafanuliwa kama ifuatavyo:-

3.3.1 **Sheria ndogo kwenda Kinyume na Masharti ya Katiba (kama ilivyorekebisha)**

3.3.1.1 **Mheshimiwa Spika**, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 ndio Sheria Mama na kwa msingi huo Sheria zote za nchi zinapaswa kutungwa pasipo kuwa na maudhui yanayokinzana nayo. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Sheria Ndogo ya *The Urban Planning (Appeals), Regulations, 2018* ambayo imetungwa chini *The Urban Planning Act*, Sura ya 355, ina maudhui yanayokiuka Katiba ya Nchi. Dosari hiyo imebainika katika **Kanuni ya 5(2)** ambayo inaweka sharti la lazima kwa Mahakama mara baada ya kutoa uamuzi, kuwasilisha nakala tatu za hukumu kwa Mamlaka ya Mipango Miji zinazoainisha sababu za kufikia maamuzi yake.

3.3.1.2 **Mheshimiwa Spika**, utaratibu uliowekwa na Kanuni hii unaingilia mamlaka ya Mahakama ambayo inajiendesha kwa mujibu wa **Ibara ya 107B** ya **Katiba ya Jamhuri ya**

Muungano wa Tanzania na taratibu za Kimahakama zilizoanzishwa kwa mujibu wa Sheria za nchi. Ikumbukwe kuwa chombo kinachoweza kuamuru Mahakama kufanya jambo lolote kwa uamuzi iliyotoa ni Mahakama iliyo juu yake na si chombo au taasisi nyingine nje ya Mfumo wa Mahakama (*Judicial Hierarchy*).

3.3.1.3 **Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 36(1) cha Sheria ya Tafsihi ya Sheria, Sura 1 kinaeleza kwamba, Sheria Ndogo haipaswi kuwa na vifungu vinavyokinzana na Sheria Mama iliyoanzisha au Sheria nyingine yoyote ya Nchi na ikitokea inakuwa na Vifungu vinavyokinzana, vifungu hivyo vitahesabika kuwa ni batili kwa kiwango ilichokinzana na Sheria Mama au Sheria nyingine yoyote ya nchi. Hivyo kutokana na Kanuni ya 5(2) kuweka masharti yanayoonekana kukikua ya Katiba ya Nchi inahesabika kuwa ni batili.

3.3.1.4 **Mheshimiwa Spika**, ni vema vyombo vilivyokasimiwa mamlaka ya kutunga Sheria Ndogo vikazingatia misingi ya mgawanyo wa madaraka katika Mihimili ya nchi wakati wa utungaji wa Sheria Ndogo. Hii itasaidia kuondoa migongano na hatimaye kuwezesha Mihimili ya nchi kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria za Nchi.

3.3.2 **Sheria Ndogo kwenda kinyume na Sheria Mama au Sheria nyingine za Nchi.**

3.3.2.1 **Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini pia Kanuni ya *The Urban Planning (Appeals), Regulations, 2018* zinazoanzishwa chini ya Sheria ya *The Urban Planning Act*, Sura ya 355 ina masharti yanayokinzana na yale yaliyowekwa na Sheria nyingine ya nchi. **Kanuni ya 4(b) (ii) (iii)** ya Kanuni hii, inaweka sharti kwamba mtu anayetaka kukata rufaa dhidi ya Mamlaka ya Mipango Miji, atapaswa kuwasilisha kwa Mamlaka ya Mipango Miji, orodha ya nyaraka anazotarajia kutumia katika rufaa yake pamoja na nyaraka ambazo hakuwahi kuziwasilisha kwa Mamlaka ya Mipango Miji katika hatua ya usikilizaji wa shauri la awali dhidi ya Mamlaka hiyo.

3.3.2.2 **Mheshimiwa Spika**, Kamati imeona utaratibu huu si sahihi kwa kuwa, katika hatua hii mrufani hapaswi kuwasilisha ushahidi wa aina yoyote kwa mrufaniwa mpaka pale ambapo kesi yake itakapokuwa imefikishwa mahakamani. Aidha katika hatua ya rufaa mrufani hapaswi kuwasilisha ushahidi mpya mpaka pale tu mahakama itakapoonona kuna haja ya kufanya hivyo ili kufikia maamuzi kama inavyoonyeshwa katika **O. XXXIX R. 27** ya Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Madai, Sura 33 (*The Civil Procedure Code, Cap 33*).

3.3.2.3 **Mheshimiwa Spika**, kukinzana kwa Kanuni na Sheria Mama au Sheria nyingine za nchi kama inavyoonekana katika Kanuni za *The Urban Planning (Appeals), Regulations, 2018* ni kinyume na masharti ya **Kifungu cha 36 (1)** cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1, ambacho kinazitaka Sheria Ndogo kutokinzana na Sheria Mama, Katiba na Sheria nyingine za nchi. Halikadhalika ni kinyume na **Kifungu cha 39(1)** cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 kinachoelekeza kuwa maneno yatakayotumika katika Sheria Ndogo yanapaswa kuwa na maana sawa na yale yaliyotumika katika Sheria Mama.

3.3.2.4 **Mheshimiwa Spika**, kwa msingi huo uliowekwa kwa mujibu wa Sheria ya Tafsiri ya Sheria, kunaifanya Kanuni ya **Kanuni ya 4 (b) (ii) (iii)** ya *The Urban Planning (Appeals) Regulations, 2018* kuhesabika kuwa ni batili kutokana na kukinzana na masharti yaliyowekwa kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Madai, Sura 33 (*The Civil Procedure Code, Cap 33*).

3.3.2.5 **Mheshimiwa Spika**, Sheria Ndogo nyingine iliyobainika na Kamati kuweka masharti yanayokinzana na Sheria Mama ni *The Urban Planning (Building) Regulations, 2018* ambayo imetungwa chini *The Urban Planning Act, Sura ya 355*. Uchambuzi wa Kamati umebaini dosari katika **Kanuni ya 3** ambayo inatoa tafsiri ya neno " *Vehicle*" ikihusisha vitu kama mkokoteni wa kuvutwa na ng'ombe, baiskeli ya matairi mawili, baiskeli ya matairi matatu. Tafsiri hii ni kinyume na ile inayotolewa na Sheria ya Usalama Barabarani, Sura 168 ambayo haijabainisha vifaa hivyo kuwa ni sehemu ya

vyombo vya moto. Halikadhalika masuala ya vyombo vya moto kwa namna yoyote ile hayahusiani na maudhui ya Kanuni hii inayohusu masuala ya mipango miji.

3.3.2.6 **Mheshimiwa Spika**, kuweka katika Sheria Ndogo maneno tofauti na yale yaliyotumika katika Sheria nyingine za nchi ni kinyume na **Kifungu cha 36(1)** na **Kifungu cha 39 (1)** cha Sheria ya Tafsiri za Sheria ambacho kinaeleza kwamba, maneno yatakayotumika katika Sheria Ndogo yanapaswa kuwa na maana sawa na yale yaliyotumika katika Sheria Mama.

3.3.2.7 **Mheshimiwa Spika**, dosari ya kwenda kinyume na masharti ya Sheria Mama pia iligundulika katika Sheria Ndogo ya *The Urban Planning (Building) Regulations, 2018* ambazo zimetungwa chini *The Urban Planning Act*, Sura ya 355. Kamati ilifanya uchambuzi wa Kanuni hii na kubaini kuwa **Kanuni ya 3** inatoa tafsiri ya neno Jengo (*Building*) kuwa inahusisha pia mabango ya matangazo na minara ya simu kinyume na tafsiri inayotolewa na Sheria Mama chini ya **Kifungu cha 2** ambayo pamoja na masuala mengine haijafafanua masuala ya Mabango ya Matangazo na Minara ya simu.

3.3.2.8 **Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa tafsiri tofauti ya neno Jengo (*Building*) iliyotolewa na Kanuni hii inakwenda kinyume na **Kifungu cha 36 (1)** na **Kifungu cha 39 (1)** cha Sheria ya Tafsiri za Sheria, Sura ya Kwanza vinavyoeleza bayana kuwa, vifungu vya Sheria Ndogo havipaswi kutofautiana na vile vya Sheria Mama au Sheria nyingie za nchi. Halikadhalika maneno yatakayotumika katika Sheria Ndogo yanapaswa kubeba maana ile ile iliyotumika katika Sheria Mama iliyoianzisha Sheria Ndogo husika.

3.3.3 **Sheria Ndogo kuwa na makosa ya uandishi katika Majedwali (Kutorejea Kanuni sahihi, kurejea Kanuni ambazo hazipo, kutorejea kabisa Kanuni na Maudhui ya Jedwali tofautiana na Vifungu)**

3.3.3.1 **Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Moja wa

Bunge, Kamati ilibaini dosari mbalimbali za uandishi katika Majedwali ikiwa ni pamoja na kutorejea Kanuni sahihi zinazoanzisha Majedwali husika kurejea Kanuni ambazo hazipo na Maudhui ya Jedwali kuwa tofauti na vifungu vya Kanuni.

3.3.3.2 **Mheshimiwa Spika**, dosari za uandishi wa Majedwali zilibainika pia Sheria Ndogo za *The Urban Planning (Building) Regulations, 2018* zilizotungwa chini ya Sheria ya *The Urban Planning Act, Sura ya 355*. Kamati ilibaini dosari katika **Fomu Na 18 na Na. 19** katika **Jedwali la Nne**. Fomu hizo zinarejea kuanzishwa chini ya **Kanuni ya 77(1) (r)** ambayo haipo katika Sheria Ndogo hii.

3.3.3.3 **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kifungu cha 25 (2)** cha *Sheria ya Tafsiri za Sheria, Sura ya 1*, majedwali ni sehemu ya Sheria na husaidia kufafanua zaidi maudhui ya kifungu husika katika Sheria. Hivyo kwa Kanuni hizo zilizoobainika kutoweka rejea sahihi ya vifungu katika Majedwali husika, si tu italeta changamoto ya usomaji bali pia inafanya Majedwali hayo kukosa uhalali wa kuwepo katika Kanuni kwa kuwa hayajaanzishwa na vifungu sahihi.

3.3.4 **Sheria Ndogo kutozingatia misingi ya uandishi wa Sheria (Drafting Principles)**

3.3.4.1 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi wa Sheria Ndogo za *The Urban Planning (Urban Farming) Regulations, 2018* zilizoanzishwa chini ya Sheria ya *The Urban Planning Act, Sura 355*. Katika uchambuzi huo Kamati imebaini dosari za uandishi wa sheria, ambapo mwishoni mwa Sheria Ndogo hii kumewekwa ufafanuzi wa maneno mbalimbali pasipo kuyaweka katika Kanuni ya 2 ambayo ni mahsusni kwa ajili ya kutoa tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika katika Kanuni zenyewe.

3.3.4.2 **Mheshimiwa Spika**, Sheria Ndogo nyingine iliyobainika kuwa na dosari za uandishi ni *The Electronic and Postal Communications (Sim Card Registration) Regulations, 2018* ambazo zinaanzishwa chini ya Sheria ya *The Electronic and*

Postal Communications Sura 306. Sheria Ndogo hii pia imebainika kuweka maelezo ya ziada kuhusu sifa za picha zitakazopigwa, mashine za kielektroniki zitakazotumika katika usajili wakati wa kusajili laini za simu pasipo kuyaweka maelezo hayo katika Kifungu chochote.

3.3.4.3 **Mheshimiwa Spika**, utaratibu huu ni kinyume na uandishi wa Sheria, kwa kuwa maneno yote yanayotolewa tafsiri yanapaswa kuwa katika Kifungu cha Tafsiri au katika Kifungu chochote kinachoelezea jambo mahsusi na si kuandikwa pekee pasipo kuwa na rejea ya Kanuni husika. Aina hii ya uandishi inaweza kuleta changamoto pale ambapo mtu anahitaji kufanya rejea ya maneno hayo kwa kuwa hayana Kifungu kinachoyapa nguvu ya Sheria Ndogo kuwepo katika Kanuni hii.

4.0 MAPENDEKEZO YA JUMLA

4.1 **Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri mamlaka zote ambazo zimekasimiwa na Bunge madaraka ya kutunga Sheria Ndogo, kuzingatia kikamilifu ushirikishwaji wa wadau wanaolengwa na Sheria Ndogo yoyote ili kupunguza changamoto mbalimbali zinazoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa Sheria Ndogo hizo.

4.2 **Mheshimiwa Spika**, kamati inashauri Serikali iongeza idadi ya Rasilimali watu katika Ofisi ya Rais (TAMISEMI) na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali hasa vitengo vinavyohusika na upitiaji wa Sheria Ndogo ili kuhakikisha makosa yanayojitokezamara kwa mara katika Sheria Ndogo yanarekebishwa kabla ya Sheria Ndogo hizo kuchapishwa katika Gazeti la Serikali na kuanza kutumika.

4.3 **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Mamlaka zilizopewa jukumu la kutunga Sheria Ndogo kufanya kazi kwa karibu na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakati wa utungaji wa Sheria Ndogo kwa lengo la kuondoa dosari mbalimbali zinazojitokeza.

4.4 **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kuzifanyia marekebisho Sheria Ndogo zote zenye dosari. Baada ya marekebisho hayo kufanyika na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali, Sheria Ndogo hizo ziwasilishwe Bungeni kwa mujibu wa Sheria.

4.5 **Mheshimiwa Spika**, kuhusu, Sheria Ndogo ya *The Mining (Local Content) Regulations, 2018 (GN Na. 3/2018)*, tafsiri ya meneno "*Indigenous Tanzanian Company*" na "*Indigenous Tanzania Bank*" ifanyiwe marekebisho ili kuondoa masharti hasi kwenye makampuni ambapo Serikali inamiliki chini ya asilimia hamsini na moja (51%) ya hisa zote. Aidha, Mabadiliko hayo yatawezesha kupanua wigo wa ushiriki wa benki na taasisi za fedha zilizosajiliwa hapa nchini katika fursa za kiuchumi katika sekta ya madini.

5.0 HOJA

5.1 Dosari ya Uandishi wa Majedwali ikilinganishwa na Vifungu vya Sheria

KWA KUWA, katika uchambuzi wa Kamati imebainika kuwa baadhi ya Sheria Ndogo zina dosari mbalimbali katika majedwali kuhusu vifungu vinavyoanzisha majedwali husika.

NA KWA KUWA, kwa mujibu wa Kifungu cha 25 (2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinabainisha kwamba Majedwali ni sehemu ya Sheria.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Wizara ambazo Sheria Ndogo zake zimebainika kuwa na dosari katika Majedwali zifanyiwe marekebisho ili kuondoa dosari hizo.

5.2 Kukinzana na masharti ya Sheria Mama au Sheria nyingine za nchi.

KWA KUWA, baadhi ya Sheria Ndogo zilizofanyiwa uchambuzi na Kamati zilibainika kuwa na vifungu vinavyokinzana na masharti ya Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi.

NA KWA KUWA, kukinzana huko ni kwenda Kinyume na masharti ya Kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri za Sheria kinachotoa sharti kwa Sheria Ndogo kutokwenda kinyume na masharti ya Sheria Mama.

NA KWA KUWA, kukinzana huko kunaifanya Kanuni husika kuwa ni batili kwa kiwango ilichokinzana.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Wizara zinazohusika, kufanya marekebisho katika Sheria Ndogo hizo ili kuondoa vifungu vinavyokwenda kinyume na masharti ya Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi.

6.0 HITIMISHO

6.1 **Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dharti kwako binafsi na Bunge lako tukufu kwa kuweka utaratibu wa taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuwasilishwa katika Bunge lako tukufu. Ni matumaini yangu kwamba, utaratibu huu utakuwa endelevu na umuhimu wa Kamati hii katika maendeleo ya nchi yetu utaonekana kwa kuwa kwa kiasi kikubwa Sheria Ndogo ndizo zinagusa maisha ya kila siku ya wananchi wengi.

6.2 **Mheshimiwa Spika**, kipekee kabisa naomba nimshukuru Mhe. Jenista Mhagama (MB) – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu) kwa kuendelea kuweka uratibu mzuri ambao uliwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, niwashukuru Mawaziri na Naibu Mawaziri wa sekta mbalimbali kwa kufika mbele ya Kamati na kujibu hoja zilizobuliwa na Wajumbe wa Kamati. Kwa heshima na taadhima naomba niwatambue kwa jinsi walivyofika mbele ya Kamati kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dkt Harrison Mwakyembe (Mb) – **Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**
2. Mhe. William Lukuvi (Mb) – **Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.**

3. Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb) – **Naibu Waziri wa Fedha na Mipango.**
4. Mhe. Atashasta Nditiye (Mb) – **Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.**
5. Mhe. Eng. Stella Manyanya (Mb) – **Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.**
6. Mhe. Stanslaus Nyongo (Mb) – **Naibu Waziri wa Madini.**

6.3 **Mheshimiwa Spika**, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi Bunge na Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge na hatimaye kufanikisha kazi hii. Kwa heshima kubwa naomba majina yao yaingie katika kumbukumbu rasmi za Bunge (*Hansard*) :-

1. Mhe. Andrew John Chenge, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. William Mganga Ngeleja, Mb - **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Aida Joseph Khenani, Mb
4. Mhe. Khamis Mtumwa Ali, Mb
5. Mhe. Rashid Ali Abdallah, Mb
6. Mhe. Mlinga Goodluck Asaph, Mb
7. Mhe. John John Mnyika, Mb
8. Mhe. Halima James Mdee, Mb
9. Mhe. Elibariki Emmanuel Kingu, Mb
10. Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mb
11. Mhe. Sabreena Hamza Sungura, Mb
12. Mhe. Sadifa Juma Khamis, Mb
13. Mhe. Anne Kilango Malecela, Mb
14. Mhe. Zainab Athman Katimba, Mb
15. Mhe. Salome Wycliffe Makamba, Mb
16. Mhe. Twahir Awesu Mohammed, Mb
17. Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb
18. Mhe. Mary Deo Muro, Mb
19. Mhe. Easter Lukago Midimu, Mb

6.4 **Mheshimiwa Spika**, aidha napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Ndg. Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati hii ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, nimshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein akisaidiwa na Bi. Angelina Sanga, Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati wa Idara ya Kamati za Bunge kwa usimamizi mzuri wa Shughuli za Kamati.

Mwisho lakini si kwa umuhimu, niwashukuru Makatibu wa Kamati ya Sheria Ndogo Ndg. Yona Kirumbi, Ndg. Angela Shekifu, Ndg. Stanslaus Kagisa, Ndg. Mkuta Masoli wakisaidiwa na Ndg. Paul Chima kwa kuratibu vyema Shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Andrew J. Chenge, Mb

MWENYEKITI

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO

13 Septemba, 2018

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Ahsante sana Mheshimiwa Mtemi Andrew Chenge kwa Taarifa hiyo ya Kamati ya Sheria Ndogo. *(Makofi)*

Tunaendelea sasa na mjadala wa jumla. Tunaanza na Mheshimiwa Rashid Abdallah Salim; hayupo tunaendelea na Mheshimiwa Hawa Ghasia. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, yupo Mheshimiwa Rashid.

MWENYEKITI: Yupo! Haya, Mheshimiwa Rashid anaanza, halafu atakuja Mheshimiwa Hawa Ghasia.

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, jina langu lilikuwa ni Rashid Ali Abdallah.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pia, nishukuru kwa wasilisho lililotolewa na Mwenyekiti wangu na kufahamika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge ndicho chombo pekee cha kutunga sheria na mara baada ya kutunga sheria, sheria hii lazima iende ikatekelezwe, na utekelezaji wa sheria hii kunahitajika kuandaliwa kwa kanuni chini ya Ibara ya 97(5) ya Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikia jinsi uchambuzi ulivyotolewa na hiyo ndiyo hali halisi ya baadhi tu ya sheria, kanuni ambazo zimeletwa katika Bunge hili. Kwa utaratibu sheria zinatungwa huko zinakotungwa, aidha, Waziri au Wizara yake, lakini zinapitia kwa Mwanasheria Mkuu halafu baaday ndipo zinatangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali na kupewa *GN. number*. Sheria hizi baada ya hapo zinaendelea kutumika kabla ya kupita kwenye Kamati hii ya Sheria Ndogo. Kwa hiyo, tutaona hapa sheria chache tu ambazo zimewasilishwa kwenye Bunge zina makosa ambayo yamekwenda kinyume na Katiba ya nchi, zimekwenda kinyume na sheria na hata zimekwenda kinyume na haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utaona *trend* ilivyo, kwamba sheria ngapi zimepita hapa na sheria ngapi ziko nje zinatumika kimakosa na kwa maana hiyo, tunasema kwamba, sheria hizi nyingi ambazo zinatungwa watungaji hawana uangalifu wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kama ni Halmashauri basi tunao Wanasheria wa Halmashauri, zikitoka kwenye Halmashauri zinakwenda kwa Waziri, zikitoka kwa Waziri zinakwenda kwa Mwanasheria Mkuu, lakini bado makosa yanakuwa makubwa, yanakuwa kinyume na Katiba. Kwa hiyo, tunaona ni jinsi gani kazi inavyofanyika na jinsi gani wananchi wanaumia huko vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba kama tunabadilisha sheria, Kamati imependekeza sheria ibadilishwe, lakini bado sheria inatumika huko, kwa hiyo huu ni mzunguko. Kwanza uende ukabadilisha sheria, sheria inaendelea kutumika, kwa hiyo haileti maana halisi. Mimi nadhani huu ni mfumo wa Serikali kuweza kutumika sheria kabla ya kupita kwenye Kamati, lakini kuna haja sasa ya mfumo huu kutazama upya kwa sababu, sheria inaumiza wananchi, lakini inatumika na baadaye ndipo sheria inakuja kwenye Bunge na hiyo sio sheria zote ni baadhi tu ya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia hizo sheria ambazo ziko huko ni kiasi gani zinakandamiza wananchi hawa? Kuna mazao, ulipaji wa kodi ya mazao, kuna masuala ya uendeshaji wa shughuli mbalimbali za biashara zao, kuna kanuni hizo zinaendelea kutumika, basi wanyonge huko ndio wanaoumia zaidi. Sheria hizi ni za nchi nzima, kila unapokwenda ziko sheria hizi ndogo zinaendelea kutumika na zinaendelea kwa sababu kuna sheria mama inatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina wazo kwamba kwa mujibu wa Katiba Bunge limekasimu madaraka kutunga hizi kanuni, lakini hao ambao wanatunga hawako *serious*, na makosa haya yataendelea kuwepo.

Mimi nilisema kuna haja ya kubadilisha mfumo huu, sheria zile ambazo ni *very serious* au ni *emergency majesty*, ni haraka sana, zinaweza zikaenda, lakini zile sheria ambazo hazina umuhimu sana kabisa, basi ni lazima zipitie kwenye Kamati ya Sheria Ndogo, ili kuhakikisha kwamba, ziko sahihi; lakini tukiendelea na mfumo huu bado Wananchi wataendelea kukandamizwa na hakuna mtu wa kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano hata Serikali nayo inapata matatizo, kuna uendeshaji wa shughuli za petroli. Kama unaendesha shughuli za petroli lazima uwe na kibali, na sheria inasema kama huna kibali basi ni faini isiyopungua shilingi milioni 20. Hata hivyo kanuni inasema kama utaendesha shughuli hizi za petroli bila kibali ni faini ya

shilingi milioni tano. Kwa hivyo, hapo tunaona Serikali imepeta hasara kiasi cha shilingi milioni 15 zimeondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kanuni inasema milioni tano; na hiyo, sijui kama imeletwa wakati gani kwenye Bunge. Kwa hiyo, ni kusema kwamba Serikali pia inakosa mapato, lakini pia wananchi nao pia wanakandamizwa na sheria hizi kwa sababu zinakuwa ni kinyume na Katiba na hata pengine wakaenda Mahakamani sheria hizi hazina *support* yoyote, zinafutwa na kwa maana hiyo ni kupoteza nguvu ya Serikali, kupoteza nguvu ya Wananchi wenyewe walioshitakiwa na halleti tija yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pendekezo langu ni kwamba, sheria hizi zinagusa Wabunge wote katika majimbo yao na Halmashauri zao. Kuna haja ya kubadili mfumo ili kuhakikisha sheria kwanza zinathitishwa ziko sahihi, lakini pia, ninachokisema mimi na kinachonisikitisha kabisa ni kwamba, kwa nini sheria inapita kwa Mwanasheria Mkuu? Kwa nini sheria inapita kwa Mheshimiwa Waziri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri anakuja kwenye Kamati basi haelewi ni sheria ipi anakuja kui-*defend*. Sasa sijui hizi sheria zinakwendaje, hawaeleweki; Waziri unamwambia funua ni sheria gani, anamuuliza Katibu Mkuu, haelewi. Kwa hiyo Mawaziri hawako *serious* na masuala haya, Mwanasheria Mkuu pia katika ofisi yake hawako *serious* na katika Halmashauri, Wanasheria wa Halmashauri hawako *serious*. Kwa hiyo, hii mamlaka waliyopewa hawaietendei haki ni vizuri turudie katika mfumo ambao ni sahihi. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa, tunaendelea na Mheshimiwa Hawa Ghasia na baadae Mheshimiwa Zainab Katimba ajiandae.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenijalia uhai na kuweza kusimama mbele ya Bunge lako tukufu na kuweza kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu.

Pia nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Spika kwa kuanzisha Kamati hii, lakini pia utaratibu wa kuwasilisha taarifa hii mara mbili kwa mwaka, kwa sababu imekuwa na mchango mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu kwamba sheria ndizo ambazo Bunge tunashiriki kwa kiasi kikubwa katika kuzitunga, lakini kanuni zinatungwa na Mawaziri na zinaanza kutumika sisi tunakuja baadae kuziona. Kwa hiyo, ukiangalia kwa kiasi kikubwa sheria nyingi kwa kuwa, zinakuwa zimepitia kwa wadau wengi unaweza ukakuta hata kama kunakuwa na mapungufu yanakuwa ni machache sana. Kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Mawaziri wakati wa kuandaa kanuni si vibaya tukashirikisha wadau mbalimbali, ili na wenyewe wakatia mchango wao na wakaweza kutusaidia katika kuziboresha kanuni zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo Sheria yetu ya Madini ambayo tuliipitisha mwaka jana na pia tukawa na kanuni zake; Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi. Sasa katika kanuni ukiangalia suala la *local content* na suala zima la *indigineous bank* na *ndigineous company*, ukiangalia pale unakuta kunakuwa na matatizo makubwa sana. Nia ya sheria ni nzuri, lakini inavyokuja kanuni unakuta sasa ile nia nzuri inapotea. Lengo la kuhakikisha kwamba, tunakuwa na *local content* siyo kwa vile ambavyo imetafsiriwa katika kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaposema kwamba, kampuni ya madini itawekeza akaunti zake katika *indigenous bank* na ukatoa tafsiri ya *indigenous bank* ambayo inaitoa CRDB, inaitoa NMB na naitoa NBC, benki zinazobaki kwa kweli, hazina uwezo hata hizo kampuni zikisema yanataka kukopa, lakini hata uwezo wake ule wa kuhimili kwa sababu baada ya hapo zitabaki labda *Mwanga Community Bank*, *Mufindi Community Bank* au labda Azania, ndizo ambazo utazikuta zinaendana na yale masharti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa kanuni ikitoka inachukua muda mrefu sana kuja kurekebisha, mimi

nadhani ni vizuri sana Waheshimiwa Mawaziri wanapozitunga zile kanuni hata wakaishirikisha Kamati ya Sheria Ndogo wakazipitia kabla ya kuzitangaza katika Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina uhakika kabisa kwamba zitakuwa ni kanuni nzuri sana kwa sababu hatutegemei kanuni izizidi sheria, lazima sheria iwe juu ya kanuni. Kwa hiyo, hilo lilikuwa ni pendekezo langu la kwanza, kwamba Waheshimiwa Mawaziri wanapotunga kanuni, wala sio vibaya waka-*share* na Kamati Ndogo, lakini pia wakawashirikisha wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiachia suala la benki, mfano *indigenous company*, Shirika kama PUMA Serikali ina hisa 50%. Ndiyo kusema PUMA ikinufaika na Serikali imenufaika na wananchi wananufaika, kwa sababu Serikali inasimama kwa niaba ya Watanzania. Sasa kwa kanuni ile sasa inaitoa PUMA kufanya kazi na migodi ya dhahabu au na migodi mingine, kwa sababu PUMA sasa inakuwa sio *indigenous company* kwa sababu *share* za Serikali au *share* za Watanzania kupitia Serikali ni 50% tu. Kwa hiyo, niombe wakati tunavyotunga kanuni, nia ni nzuri, lakini tuwe tunaangalia hivi tunavyosema *indigenous company* au *indigenous bank* ni zipi tunazozikusudia na kama sisi tutanufaikaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kwa kiasi kikubwa kampuni zetu, sekta binafsi katika nchi yetu ni change, kwa hiyo tunategemea pale ambapo Serikali ipo, imeingia ubia, ndio wananchi wapo, Serikali ikinufaika Wananchi tumenufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo pia nilitaka nilichangie, tumesikia kwamba kumekuwa na matatizo ya uandishi katika baadhi ya kanuni na wakati mwingine hata sheria ndogo zinazotungwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hata hivyo wakati mwingine makosa yale yanajitokeza kutokana na uchache wa rasilimali watu katika ofisi zetu na wakati mwingine na wingi wa kazi uliopo. Mfano kama sasa hivi unakuta tuna Halmashauri 185, useme tu nusu

yake wamepeleka Sheria zao Ndogo TAMISEMI na zinahitajika kwa haraka, umepeleka Sheria Ndogo 80 au 90, watumishi waliopo je, wanaendana na kazi iliyopo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali nayo tuhakishe kwamba, tunajengea uwezo kwa maana ya kwamba, watumishi, rasilmali watu, lakini pia na kuziwezesha kwa sababu tunazo sekta zinazoibukia, masuala ya gesi na *oil*. Wengi wa wanasheria wetu wamesoma, lakini wanasoma mambo hayo hayakuwepo, lazima tuwajengee uwezo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Hawa Ghasia, tunaendelea na Mheshimiwa Zainab Katimba na baadae Mheshimiwa Elibariki Kingu ajiandae.

MHE. ZAINAB A. KATIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii na mimi kuweza kuchangia taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa *the Interpretation of Laws Act, Cap. 1*, imeweka masharti maalum ambayo yanalipa Bunge mamlaka ya kuweza kuzisimamia au kufanya udhibiti wa Sheria Ndogo ambazo zinatungwa na Serikali pamoja na taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge linafanya udhibiti huo baada ya sheria zile ndogo kuwa zimetungwa na Serikali na zimetangazwa katika Gazeti la Serikali, lakini pia zimewasilishwa Bungeni. Katika uchambuzi wa sheria ndogo vitu ambavyo tunajiridhisha ni kwamba, kama sheria ndogo hizo zilizotungwa zinaendana na zinakidhi matakwa na masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini pia zinakidhi matakwa na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sheria ndogo ya *The Mining Local Content Regulation* katika kanuni ya 3, kanuni hii inaonekana kwamba ni *ultra vires* kwa maana ya kwamba, inakwenda kinyume na masharti ya sheria mama, kivipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, ukiangalia kanuni hii yenyewe inatoa tafsiri ya neno kampuni zawa ambayo katika tafsiri yake imeweka kwamba, kampuni zawa itakuwa ni ile kampuni ambayo katika *share holders* wake au wanahisa 51% ya wenye hisa wawe ni Watanzania. Si hivyo tu, pia 80% katika utendaji wa juu wa kampuni hiyo pia, wawe ni Watanzania. Sasa ukiangalia Sheria ya Makampuni ambayo ndio sheria mahususi kwa masuala ya makampuni kwa Tanzania hii, haijatoa tafsiri hiyo, ambayo imetolewa katika kanuni hii kwa hiyo, maana yake nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kunakuwa na mkanganyiko wa tafsiri na utaratibu wa kutunga kanuni au kutunga sheria ndogo ni lazima sheria mama zizingatiwe. Pale kunapokuwa na mkanganyiko kati ya sheria mama pamoja na kanuni hiyo inaleta changamoto na ninaomba sana marekebisho yaweze kufanywa ili kuondoa mkanganyiko huo kwa sababu ukiangalia kwenye Sheria ya Makampuni yenyewe inatafsiri kampuni zawa ni kampuni ile ambayo imesajiliwa chini ya *BRELA*. Kwa hiyo matakwa ya *shareholding structure* hayajawekwa kwenye Sheria ya Makampuni.

Kwa hiyo, ni vizuri Sheria ya Makampuni ifanyiwe mabadiliko ili kuweza kuendana na matakwa ya mabadiliko na kuzuia mkanganyiko wa sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda pia kwenye *The Urban Planning (Appeals), Regulations, 2018* ambayo imetungwa chini ya Sheria ya *The Urban Planning Act*, Sura ya 355, utaona kwamba kanuni hii imeweka sharti kwamba mahakama mara baada ya kutoa uamuzi, kuwasilisha nakala tatu za hukumu kwa Mamlaka ya Mipango Miji zinazoainisha sababu ya kufikia maamuzi yake. Sasa ukiangalia kanuni hii, utaona kwamba utaratibu uliowekwa na kanuni hii si sawa,

kwa nini, kwa sababu hamna chombo au taasisi yoyote ya Serikali...

T A A R I F A

MWENYEKITI: Taarifa, Mheshimiwa Mwakasaka.

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba tu nimpe taarifa mwongaji Mheshimiwa Zainab Katimba kwamba nikiangalia kule mbele anaongea kitu ambacho ni muhimu sana lakini sioni upande wa Serikali anaye-*note down* pale hili suala la kisheria. Naona haijakaa sawa sawa. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Mwakasaka, Mheshimiwa Zainab wenyewe wameshakusikia, Mheshimiwa Zainab tuendele.

MHE. ZAINAB A. KATIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nashukuru kwa taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mahakama ni mhimili unaojitegemea na unaoendeshwa chini ya Ibara 107(b) lakini unapooni kwamba kuna kanuni ambayo inatoa sharti ya kuamuru Mahakama tofauti na utaratibu basi hii kanuni inakuwa ni batili na inakinzana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana gani kwamba Mahakama haiwezi kuamuriwa na Serikali au chombo chochote cha Serikali, bali mahakama inaamuriwa na mahakama iliyo juu yake, si tofauti na hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hii kanuni ambayo inayotoa masharti kwa Mahakama kuleta maelezo na kuleta nakala tatu za hukumu kwa Mipango Miji na kuainisha sababu ya kufikia maamuzi yake ina changamoto na sio sahihi na kuna haja ya kufanya marekebisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo hivyo tu, ukiangalia kwenye hii *The Urban Planning (Appeals), Regulations*, 2018 kanuni ya 4(b) kanuni ya ndogo ya pili na ya tatu utaona kwamba inaweka sharti kwa mtu anayekata rufaa dhidi ya maamuzi ya Mamlaka ya Mipango Miji kutoa nyaraka zote pamoja na zile ambazo hakuwa amezitoa katika uskilizaji wa shauri la awali dhidi ya mamlaka hiyo kuzipeleka kwa Mamlaka ya Mipango Miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika utaratibu mtu anayetoa rufaa hatakiwi wala hapaswi kisheria kupeleka nyaraka zozote kwa yule mrufaniwa, tofauti na hapo inabidi tu asubiri mashtaka yaanze na atakabidhi nyaraka kwa Mahakama na si kumpelekea yule ambaye yeye anaenda kukata rufaa dhidi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sio hivyo tu hata katika ngazi ya rufaa, rufaa haichukui ushahidi mpya, rufaa inafanya uamuzi kutokana na nyaraka zilizokuwepo kuanzia mwanzo katika mashtaka, lakini kusema kwamba kuletwe nyaraka mpya si utarabu sawa na ni kinyume na tofauti na kanuni hizi zinavyoelekeza. Kwa hiyo, kuna haja ya kufanya marekebisho ili kuendana na sheria zilizowekwa ambazo zinaongoza utaratibu wa kimahakama wa kukata rufaa na wa kimashtaka kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kujielekeza kwenye baadhi ya hizi sheria ndogo, naomba sasa kuishauri Serikali kwamba wakati wa utungaji wa sheria ndogo kwanza wawashirikishe wadau mbalimbali ili hizi sheria ndogo zinapokuja kutungwa kusiwe kuna changamoto wakati wa utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo hivyo tu, Serikali pia iongeze rasilimali watu katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali hasa katika vitengo vinavyojihusisha na kupitia sheria ndogo hizi ili kuondoa zile dosari ambazo zinaonekana ambazo hatimaye zinaleta changamoto katika utekelezaji wa sheria husika. Pia wakati wa utunzi wa sheria ndogo mamlaka au Serikali pia ihakikishe

kwamba uchambuzi na utunzi wa zile Sheria Ndogo unazingatia misingi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sheria ndogo na sheria zingine za nchi ili sheria ndogo tunazozitunga zisije zikaleta *conflict of Laws* na sheria ziwe zinaweza kutekelezeka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Zainab Katiba. Tunaendelea na Mheshimiwa Elibariki Kingu baadae Mheshimiwa Aida Khenani na Mheshimiwa Halima Mdee wajiandae.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza kabisa ni wazi inajulikana kabisa ya kwamba jukumu la kutunga sheria ni jukumu la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Katiba. Kinachofanyika kitendo cha ku-*delegate* mamlaka ya utunzi wa sheria kwenda kwenye mhimili wa *executive* ni kutokana na ukweli kwamba Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haliwezi kukaa kila siku na kutunga hizi *regulations* ambazo zinatumika kwenye mamlaka za Serikali na Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi tukiri ya kwamba mimi nikiwa kama moja ya wajumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo tumeshuhudia kwa kiwango kikubwa ukosefu wa umakini mkubwa sana sana sana kwa upande wa *executive* katika utunzi wa sheria na hasa *regulation* ambazo kimsingi ndizo zinagusa maisha ya wananchi ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umakini huu umesababisha sisi kutilia mashaka ni kwa kiwango cha namna gani wananchi wetu wanaweza wakawa *vulnerable* kuathirika kutokana na matumizi ya *regulation* ambazo tunaweza tukazipitisha na wakati mwingine kwa kiwango kikubwa zinaletwa hapa zikiwa tayari zimeshakuwa *gazetted* na ziko kwenye *operation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia kanuni nyingi zinatungwa, kanuni inasema hivi lakini ukienda kwenye sheria unakuta ni kitu tofauti hakiendani na kitu hata kimoja kuhusiana na sheria husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mdogo, ukienda kuangalia *GN. 80* ambayo inaongelea habari za *Urban Planning Building Regulation* ya mwaka 2018; ukienda kusoma kanuni ya tatu inatoa tafsiri ya neno *vehicle* ambayo kimsingi ukiangalia tafsiri hiyo iko kabisa kinyume na Sheria ya Usalama Barabarani kifungu cha 168.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizingatia hilo, ukiachilia mbali kanuni hiyo kutoa tafsiri ya neno *vehicle* tofauti, lakini bado *regulation* yenyewe inaongelea habari za *Urban Planning Building Regulation*, sasa mambo ya *vehicle* kwenye mambo ya *urban* yanaingiliana wapi? Hii inaonesha kwa kweli kuna ukosefu wa umakini mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niombe Serikali, *regulations* hizi ndizo zinazotumika ku-*govern* maisha ya kila siku ya wapiga kura na wananchi wetu. Kama mhimili wa Serikali hautachukulia suala la utungaji wa *regulation* ni kuwa ni suala *serious* kama alivyosema dada yangu Mheshimiwa Katimba, kuhakikisha kwamba mnapata *manpower* na *skilled labour* ambayo itaweza kusaidia Ofisi ya Mwanasheria na watu wa TAMISEMI katika kuhakikisha kwamba *regulation* zinazokuja ziweze ku-*reflect* misingi ya uandishi wa sheria katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hilo halitoshi, bado ukienda katika masuala ya uandishi wa majedwali, katika taratibu za uandishi wa sheria majedwali ni sehemu ya sheria, lakini unaweza ukakuta jambo limezungumzwa ukienda kwenye jedwali halipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo kwa namna moja ama nyingine yasipoangaliwa kwa umakini na kwa *trend* tuliyonayo ya ku-*gazette regulation* na kuzifanya zitumike na zinakuja baadae kwa sababu ya wingi italet

madhara makubwa sana kwa wananchi wetu. Nina imani ninayasema haya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ananisikiliza ili kusudi yaweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia pamekuwa na makosa makubwa ambayo yamekuwa yakifanyika. Misingi ya uandishi wa sheria imekuwa ikikiukwa sana, nikiwa na maana ya *drafting principles* katika uandishi wa *regulations*. Mfano mdogo unaweza ukaenda kwenye *GN. 90*, ukienda katika *GN. No. 90* utakuta kwenye ile sheria nyuma ya sheria kuna maelezo ambayo ndani ukiangalia hayana *explanation* yoyote. Ili maelezo yoyote katika sheria yaweze kupata nguvu ya kisheria, lazima yawe na kifungu kinachotoa *support* ambacho kinayapa maelezo hayo nguvu ya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukienda katika hiyo sheria niliyoisema katika *GN. 90* ambayo kimsingi inaongelea *The Urban Planning (Urban Farming) Regulations, 2018* ambayo inayotoka na sheria mama *The Urban Planning Act* Sura ya 355, ameizungumzia Mheshimiwa Katimba, lakini nyuma ya sheria nenda kasome utakuta kuna maelezo, hakuna kifungu chochote kinachoyapa maelezo hayo nguvu ya kisheria, huu ni udhaifu mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nitoe ushauri kwa Serikali. Kwa sababu sisi katika Kamati tume-*observe* makosa ya kimsingi ambayo kimsingi unaona kabisa ya kwamba kuna ukosefu wa umakini wa hali ya juu katika suala zima la utunzi wa *regulation*. Niiombe Serikali, kupitia Ofisi ya TAMISEMI, kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, toeni semina kwa maafisa ili watu wanapofanya kazi zinazoletwa kwenye Bunge tuweze kuona kwamba Mhimili wa Serikali uko *serious* katika kuandaa *regulation* ambazo zinatumiwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, niiombe Serikali kwa umakini mkubwa kabisa, ni muda muafaka sasa *regulation* zetu kabla hazijakuwa *gazette*, kwa sababu nyingi sisi kama Wabunge ambao tunasimama kwa niaba ya wananchi zinaweza kuleta madhara makubwa kwa wananchi, tuiombe

Serikali kabla hawaja- *gazetted regulation* na kanuni zozote wazilete kwenye Bunge tuweze kuziridhia ndipo ziende zikawe *gazetted* kwa ajili ya maslahi ya wapiga kura wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja nina imani Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wamesikia na nina imani Ofisi ya TAMISEMI pia wamesikia. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kingu tunaendelea na Mheshimiwa Aida Khenani baadae Mheshimiwa Halima Mdee ajandae. (*Kicheko*)

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, lakini pia ninampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo kwa kuendelea kulisaidia Taifa hili kwa kupitia taaluma yake na uzoefu wake ndani ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba hata kuna baadhi ya Wabunge hawajui majukumu ya Kamati ya Sheria Ndogo na hata kutamka hili neno unakuta mtu anasema sheria ndogo ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge linatunga sheria, lakini sheria inapotungwa na Bunge haiwezi kwenda kutumika bila kutungwa kanuni. Kanuni hizo zimekasimishwa kwenye taasisi kuanzia kwenye Halmashauri hasa kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Tunapotunga sheria, sheria nyingine zinakuja zinapitishwa kwa haraka sana lakini kanuni zinachelewa zaidi na pamoja na kuchelewa zinakuja na makosa mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo kanuni zikitungwa zikawa kinyume na sheria mama na tunaamini sheria mama ndiyo dira yetu ndiyo katiba tunayoitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lililopita nilichangia hapa kuhusu suala la sheria ndogo kwenda kinyume na sheria mama na nikaomba Wizara ya TAMISEMI ambayo iko chini

ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ndiyo inayoongoza kwa makosa na madudu mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwa sehemu wamefanyia kazi lakini ningependa wajue kwamba tunapozungumza haya mambo tumefanya utafiti. Yawezekana suala la kubana matumizi limepelekea hasara kubwa sana. Hawa watu hawapewi semina elekezi na inapotokea sheria hizi zikawa zimeshaanza kutumika ndiyo tunakuja kugundua Kamati ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Sheria Ndogo sisi sio watunzi wa sheria, lakini makosa yanayokuja yanaanzia kwenye utunzi wa kanuni yenyewe na inakuwa tayari imeshaanza kutumika. Makosa haya mengine yanafanyika kwa makusudi na hili jambo limeongezeka zaidi kwenye awamu ya tano kwenye suala la ukusanyaji wa mapato, ile tamaa ya kukusanya mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo wanatunga kanuni mpaka wanakwenda kinyume na sheria mama. Sasa ningependa kuishauri Serikali, ni vyema, hasa Wizara ya TAMISEMI na Wizara ya Fedha waende kufanya utafiti upya. Aidha, wanasheria wetu uwezo wao ni mdogo au kuna watu wanawaendesha ina maana wanaacha taaluma zao wanafuata maagizo ya kutunga hizi kanuni ambazo zinakwenda kuwaathiri Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria Ndogo kuwa na makosa ya kiundishi hii Sheria Ndogo mpaka ije ipite inakuwa imepitia kwenye hatua mbalimbali, hatuamini kwamba mpaka inaanza kutumika hawa watu wote hawajaona. Tungeomba Ofisi ya Mwasherika Mkuu wa Serikali ifuatilie kwa kina, aidha, kuna kuna upungufu mkubwa wa waandishi wa sheria au hatuna kabisa au hakuna vigezo sahihi mnavyovitumia kuwapata hao waandishi wa sheria. Kama na huko mtaingiza siasa ndiyo hali inakuwa ngumu zaidi kwa sababu hizi sheria zinakwenda kuwaathiri Watanzania wa chini kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria Ndogo kutorejea kanuni sahihi; bado wanarudia makosa yale yale, kwa sababu mpaka ianze kutumika imepita hatua kadhaa; hawa watu wako wapi? Mbona hatujaona hatua kadhaa zikichukuliwa kama watu wengine wanavyochukuliwa makosa ambayo yanakuwa yanafanyika ni ya kawaida kabisa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kutorejea jedwali sahihi, yaani hawa watu, inapita kwa mtu wa kwanza, mtu wa pili mpaka inaanza kutumika jedwali tu kwamba anarejea jedwali ambalo si sahihi na kile kitu anachokizungumzia. Hivi ni suala la kuja kujadili ndani ya Bunge, hayo ni mambo ambayo tunayafanya Sheria Ndogo sisi tunajeuka kuwa waandishi wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sijasoma *law* nimesoma *Community Development* inabidi utumie akili nyingi kufikiri. Sasa Mwanasheria Mkuu utuambie, aidha na wewe umeshindwa kutimiza wajibu wako au ofisi yako inapwaya. Kwa sababu hizi sheria tunaposema hatuzungumzii kwa sababu Waziri kama sheria imepita hapa ndani ya Bunge yeye ana mamlaka ya kutunga kanuni; unatunga kanuni ambayo inakupa mamlaka zaidi na mpaka inaanza kutumika ina makosa mpaka tunarudi ndani ya Bunge tunazungumza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri ni vema sasa kwa kuwa Bunge limekasimu mamlaka yake kwenye Kamati, kabla sheria hizi hazijaanza kutumika, hazijawa *gazetted*, sheria ikishatungwa kanuni ziletwe hapa mara moja baada ya kwamba sheria zimepita ili tuweze kupitia kanuni hizo kama zina usahihi na baadae ndiyo ziwe *gazetted* zianze kutumika kwa Watanzania kwa sababu zimewathiri Watanzania wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sioni kama kuna uharaka kiasi hicho, yaani manaleta tayari zimeshaathiri watu, kwa hiyo tunataka ziletwe kabla hazijaanza kutumika tuziangalie kama zimekwenda sawa sawa na sheria mama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la kanuni la Baraza la Sanaa la Taifa. Mheshimiwa Mwakyembe nafikiri hili jambo uliangalie vizuri. Hawa wasanii mnakuja kuwaangalia wakiwa wameshatumia nyingi ndiyo mnatunga kanuni ambazo wala hazieleweki. Wakati mwingine hili jambo linakuwa gumu kwa sababu ushirikishwaji wa wadau unakuwa mdogo na mkiwashirikisha mnawatafuta wale makada makada wale ambao wakija wanapitisha tu halafu baadae zikianza kuwaathiri ndiyo wanaanza kulalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu msanii ili afahamike kwamba ni msanii anatumia nguvu zake za ziada sana na hakuna mkakati wowote ambao wizara mmeuweka wasanii wale wa chini, ila ninyi kazi yenu ni kuandaa kanuni ambazo zinawafanya ninyi mkusanye pesa. Ni jinsi gani mnawasaidia hamna utaratibu wala mkakati wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Wizara ya Habari kama nia yao ni kuinua vipaji na michezo vya watanzania, wasijikite kwenye kukusanya pesa na kuweka adhabu ambazo zitawazuia wao kukuza na kuondoa vipaji vyao kwa sababu kuna wakati mwingine tumeshuhudia huyu Diamond ni msanii mkubwa, kuna kanuni nyingine mnatunga kwamba anavyoenda kwenye tangazo alipie milioni tano. Kuna msanii wa hali ya chini kabisa, hiyo milioni tano anaitoa wapi ina maana mnamzuia yeye mnakwenda kumtafuta mtu ambaye tayari ameshafahamika na hao ndiyo watakuwa wanaendelea kukua kila siku, wale wa chini kabisa ni vigumu sana kuweza kuonesha vipaji vyao kwamba wao wanafahamika wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri tena Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali tumieni ofisi yenu vizuri. Kama shida ni fedha za kuwapa semina elekezi watendaji wenu huko chini, hali ilivyo kwenye Halmashauri ni mbaya sana. Kama Rais alikuja kuzungumza ndani ya Bunge kuhusu tozo, zile tozo kama hamjui tunawaambia tena kanuni zilizotungwa huko chini zinakwenda kinyume kabisa na yale aliyozungumza hapa ndani na wanaoathirika ni watanzania wa hali ya chini kabisa. Kwa hiyo, ni vyema mkafuatilia yale

mnayoyazungumza na siyo kuzungumza kwa ajili ya kujiridhisha wenyewe.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Aida.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Tunaendelea Mheshimiwa Halima Mdee, baadae Mheshimiwa Ester Mmasi ajiandae.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Niseme kwamba ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo na wakati Kamati zinapangwa watu tuliopangwa Sheria Ndogo tulionekana kama vile watoto yatima kwa sababu inaonekana kama madaraja ya Kamati. Nimhakikishie Mheshimiwa Spika anayepanga Kamati kwamba nimepata nafasi ya kujifunza vitu vingi sana na ninamshukuru sana na kama Mungu atajalia niendeleo kupangwa Kamati hii milele na milele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili wamezungumza Wabunge hapa, la kwanza ambalo ni muhimu kwa Serikali, taasisi na vyombo mbalimbali kujua kwa mujibu wa Katiba na ninataka nirudie ili lieleweke. Bunge ndiyo lina jukumu la kutunga sheria kwa mujibu wa Ibara ya 64 ya Katiba. Kwa sababu Bunge tunakutana mara nne kwa mwaka na kwa sababu tuna majukumu mengine mengi zaidi ya kutunga sheria ndiyo maana Ibara ya 97(5) ya Katiba tumefanya *delegation* kwa mamlaka mbalimbali kutunga sheria ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni muhimu Mawaziri, Halmashauri na Mahakama zetu kupitia *Chief Justice* zifahamu kwamba kazi hii tumeishusha. Vilevile kupitia Kamati hii ndogo baada ya hizo sheria ndogo kuwa *gazetted* tuna wajibu wa kuja kuziangalia kama zimeenda kinyume tuna wajibu na haki ya kuzirekebisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana mkaelewa kwamba sheria hizi ndogo zinapuuzwa kwa sababu ya jina

lake sheria ndogo. Sheria hizi ndogo ndiyo zinagusa maisha ya wananchi wetu mmoja mmoja kule chini kila siku. Kwa hiyo, kama kuna kanuni, *by law*, miongozo, kanuni za mahakama, amri, taarifa na tangazo maalum lolote lile linalohusu watanzania, wawekezaji na taasisi mbalimbali hizo zote ni sheria ndogo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana watu walikuwa wanasema ooh, mnaenda kutunga sheria za mbuzi na ng'ombe sijui, hapana. Ndiyo maana ningependa hicho kitu kinachoitwa semina hata Wabunge wapewe kwa sababu kazi tunayoifanya hapa tunafanya nusu, halafu ile nusu nyingine wanaenda kufanya watu wengine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumza Mwenyekiti wetu wa kamati hapa kwamba kuna tatizo la Mawaziri wakipewa dhamana ya kwenda kutengeneza sheria ndogo wanatengeneza sheria ndogo ambazo zinakinzana na sheria mama. Juzi nimeshtuka sana wakati Kamati ya Katiba na Sheria ilipoleta suala la kuanzishwa mahakama (*mobile courts*) Waziri akalazimika kuliondoa kwa sababu Kamati ilikuwa haiungi mkono. Waziri anakuja anasema kwamba eti kifungu cha 4 cha JALA na kifungu cha 10 cha *Magistrates' Courts Act* kinampa mamlaka Jaji Mkuu kuunda mahakama, jambo ambalo ni la uongo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 4 cha JALA kama ambavyo nimesema Jaji Mkuu ana uwezo wa kutengeneza *rules* za jinsi mahakama zinavyotakiwa ziendeshwe, lakini siyo kuunda chombo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia *Magistrates' Court Act*, JALA na Sheria ya Tafsiri inayotoa tafsiri ya *Magistrate* hakuna popote ambapo Jaji Mkuu amepewa ruhusa ya kuunda mahakama nyingine, lakini ana uwezo wa kusema hii Mahakama ya Wilaya ikajisogeze iende sehemu fulani ambayo haina Mahakama ya Wilaya ili wananchi wasogezewe huduma. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira kama haya tukahoji hizi shilingi bilioni 48 mmezitumia mkanunua hayo mabasi kwa ajili ya *mobile courts/special courts* zinaenda kufanya nini? Tunajibiwa eti Jaji Mkuu anaweza kuunda mahakama mpya. Sasa vitu kama hivi vinatisha na vinaogopesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumza Mheshimiwa Aida hapa, Sheria Ndogo za BASATA. Mwenyekiti wangu wa Kamati yaani ingekuwa ni amri yangu azimio hili la leo liseme kanuni hizi zisiende kutekelezwa mpaka Waziri alete marekebisho mengine. Kanuni hizi zinaua wasanii wetu, kanuni hizi hazijengi wasanii wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, naomba nikisome kifungu cha 64 na Wabunge mnisikilize, kinasema; makosa na adhabu; haya makosa yote ninayosoma hapa ndiyo msanii anaweza akatozwa yote siyo moja moja.

Moja, Msajiliwa wa Baraza au mtu yeyote atakayebainika kuvunja au kukiuka masharti ya kifungu chochote cha kanuni hizi atakuwa anafanya kosa na atachukuliwa hatua zifuatazo;-

(i) Atatozwa faini ya papo kwa papo isiyopungua shilingi milioni moja;

(ii) Kufungiwa kazi husika na kutozwa faini ya papo kwa papo isiyopungua shilingi milioni tatu;

(iii) Kufutiwa usajili;

(iv) Kufungiwa kujishughulisha na kazi za sanaa kwa kipindi kisichopungua miezi sita;

(v) Kuzuiwa kujishughulisha na kazi za sanaa maisha kwa kubainika kulingana na ukubwa wa kosa;

(vi) Kutozwa faini na adhabu yoyote stahiki wakati wa utendaji wa kosa husika;

(vii) Kufungiwa kujishughulisha na kazi za sanaa kwa kipindi kisichopungua miezi sita; na

(viii) Kuzuiwa kujishughulisha na kazi za sanaa maisha kwa kubainika kulingana na ukubwa wa kosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *sub-section 2* inasema adhabu zilizotajwa hapo juu katika kanuni ya 64(1) zinaweza kutolewa moja moja au kwa pamoja kulingana na uzito wa kosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu fikiria zisipungua milioni moja, mbili na tatu. Ukiangalia sheria inayoanzisha BASATA hapa inawapa majukumu mengi ya kuweza kutafutia wasanii masoko, kuwajenga wasanii na kuwapa mafunzo, hawatekelezi kanuni hizi ila wameona wasanii wawili/watatu maskini wa Mungu wametoka, wanataka kuminya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nisisitize Mwenyekiti wetu ukija ku-*wind up*, namshukuru Mheshimiwa Mwakyembe alikuja akawa na busara ya hali ya juu akasema kamati ninaomba hii kitu niondoke nayo nikairudie upya niangalie, ni busara ya hali ya juu na kwa sababu ya busara hii azimio letu pamoja na mambo mengine lielekeze hizi kanuni batili zisitumike mpaka pale ambapo zitaletwa mpya na kamati ijiridhishe kwamba imeendana na hizi sheria... *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Halima Mdee, tunaendelea na Mheshimiwa Ester Mmasi na baadae Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete na Mheshimiwa Taska Mbogo wajiandae.

MHE. ESTER M. MMASI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba wengi wetu sisi Wabunge hapa ndani tuna mikataba na wananchi waliotutuma tuje tuwawakilishe katika Bunge lako tukufu. Ipo mikataba tuliyoingia kuna *psychological contracts* watu wana matarajio na sisi lakini haya yote yatatimilika pale ambapo siyo tu kwa kupitisha bajeti ya Serikali, lakini ni pamoja na kuangalia masharti hasi yanayotokana na sheria mbovu katika nchi hii ambayo yanaruhusu mianya mikubwa ya upotevu mkubwa wa fedha katika Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye muktadha wa wasilisho la Sheria Ndogo hasa nikijikita kwenye dhana nzima ya *local content policy*. Ninaomba nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikichukulia mfano wa Kampuni ya PUMA ambapo Serikali ina hisa asilimia 50 na wawekezaji wana hisa asilimia 50. PUMA kwa muktadha wa sheria hasi na sheria zenye vigezo vigumu visivyotekelezeka ni dhahiri kwamba PUMA anaenda kupoteza kiasi kikubwa cha mapato yake. Kwa sheria iliyopo ambayo ni sheria hasi, PUMA anapoteza lita 2,500,000 kwa mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu tukiangalia nafasi ya PUMA au umuhimu wa PUMA katika ujenzi wa uchumi wa taifa hili; juzi tu hapa nikiwa pamoja na Kamati ya PIC tunaona PUMA alitoa shilingi bilioni tisa gawio la Serikali. Ni dhahiri kwamba hatutasimama katika kuona kwamba sheria hizi zinafanyiwa marekebisho ya haraka ni dhahiri hata hili gawio pengine tunaweza tukalipoteza kwa siku zijazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha wa sheria hii ninaomba nieleze Bunge lako hili tukufu kwamba Shirika la *TIPER* ambalo Serikali ina asilimia 50. Tukija *SINOTASHIP* ambao ni Wakala wa Meli Tanzania kupitia ushirika wa Uchina na Tanzania itapoteza kazi kubwa nchini Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, ninapoongelea Benki ya NBC ambayo Serikali ina hisa asilimia 30; lakini ukija NMB ambapo Serikali ina hisa asilimia 31 ni dhahiri Serikali ama nchi kwa ujumla wake tutashindwa ku-*realise* faida ya kuwa na uwekezaji wa aina hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hitaji la *local content policy* inaongea pale siyo tu kwamba kampuni ya kizawa iwe na asilimia 51 ya uwekezaji, lakini pia kuna takwa la kisheria kuhusu rasilimali watu kwamba katika mfumo huu wa *local content policy*, asilimia 80 ya *top management* ni lazima wawe wazawa wa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Dkt. Mpango ni shahidi juzi nilimuona, lakini siyo hivyo katika mazungumzo yangu na Dkt. Mpango nikimuelezea dira na mwelekeo wa makao makuu ya nchi hapa Dodoma niliweza kumtahadharisha nikamwambia kwamba Mheshimiwa Dkt. Mpango hapa tunapoongea wapo baadhi ya Mabalazi ambao hawajajua hata ofisi wataijenga wapi Dodoma hapa, lakini tayari wameanza ku-*grab* ardhi na kupita kwenye Halmashauri zetu kutafuta *resources* za kuweza ku-*grab*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatutakuwa na mpango madhubuti wa kuweza kulinda wazawa wetu katika Taifa hili ili waweze kushiriki kupitia mpango huu wa *local content policy* kwenye lile takwa la kisheria la asilimia 80 ni dhahiri tutaenda bado kutokuwa na majibu sahihi hasa tunapoongelea ukuaji mkubwa wa ukosefu wa ajira nchini Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuongea na Mheshimiwa Mpango, lakini pia niliongea na Mstahiki Meya na yeye pia alikiri kwamba ni muhimu sana tukawa na sheria nzuri zenye tija ambazo zitaweza kumlinda mzawa wa Taifa hili ili na yeye aweze kushiriki kwenye ujenzi wa uchumi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wote wameongea na kimsingi wote tunaona umuhimu wa Serikali

kufanya mapitio ya haraka ya sheria hii. Kama tuliweza kuleta masuala mengi kwa hati ya dharura na hili hata ikibidi liende nje ya utaratibu lije kwa haraka. Hii ni kwa sababu Ofisi ya *TR* ina malalamiko makubwa, ina mzigo wa mashirika mengi ya Serikali yasiyokuwa na tija katika Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na unyenyekevu ninaomba sasa nimalizie kwa kuomba kwamba Serikali kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Wizara husika iweze kutendea haki suala hili ambalo Wabunge wengi wamechangia na kuguswa kwa aina yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.
(*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mmasi tunaendelea na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete.

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kupata japo dakika chache kuzungumza juu ya mchango uliotolewa hapa na Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Sheria Ndogo, Mheshimiwa Mtemi Chenge. Kwa hakika nampongeza sana hasa kwa jinsi anavyotungoza sisi, lakini pia yeye amekuwa mwenye msaada mkubwa kwa sisi wanasheria kuendelea kutusaidia kuelewa nini maana ya sheria katika uhalisia wake.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu waliotangulia wameeleza mengi na kwenye taarifa yetu ya Kamati tumeeleza mengi. Nataka nijikite katika mambo makuu mawili kama siyo matatu kama muda utaniruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza kabisa ni mahitaji ya kuwa na rasilimali watu ya kutosha katika Ofisi ya *Attorney General*. Haya yote yanayolalamikiwa hapa kama umesikiliza vizuri wengi wao wamejikita sana katika hoja kubwa ya uandishi wa sheria. Yapo maeneo mengi, tukitaka kuyaelezea hapa unaweza ukachukua muda wote uliobakia.

Naomba nizungumze kwa uchache zaidi, kwa mfano ukifungua ukurasa wa 7 na wa 17 kuna tatizo kubwa sana la uandishi unaojichanganya. Waandishi wetu wa sheria wanapenda kufanya *reference* ya vitu ambavyo havifanani na hizo sheria zenyewe, wameeleza hapa waliotangulia. Kwa mfano mmoja kwamba kuna mtu ameandika ana-*refer* Sheria ya *Traffic* ambayo ukiangalia sheria yenyewe kinachotambulishwa sicho ambacho kimeelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, majedwali mbalimbali ambayo wameyaweke kwa mfano katika ukurasa wa kwanza kwenye ile Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Gesi (*Oil and Gas*) unaona kabisa kwamba Waziri wa Fedha anapewa mamlaka ambayo mamlaka yale kwa utaratibu wake yalivyo hayatambuliki katika sheria inayoelezea juu ya usimamizi wa makusanyo ya mapato yanayotokana na *oil and gas*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunachosema ni kwamba hapa hakuna mtu anayetaka kupambana na Serikali au kuivuta Serikali, lakini basi waandishi wetu mnapofanya nukuu hizo muwe makini katika kitu gani ambacho mnaki-*refer*, isije kuwa baadaye mkaonekana kama vile kwamba ni watu makanjanja ambao hamjui hata mnalolitenda. Ndani ya ukurasa wa 10 katika Sheria Ndogo ya *Mining Local Content* nayo pia kosa hilo linajitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo mengi sana ya kueleza, lakini siyo hilo tu pia iko shida nyingine ya kutotekeleza kwa yale ambayo tumekuwa kila siku tunaeleza. Siyo mara ya kwanza Kamati inaleta mbele yako mapendekezo juu ya kazi ambayo imekwishafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unakumbuka katika taarifa yetu iliyotolewa miezi sita iliyopita tulieleza juu ya watu wetu kutokuwa makini juu ya uchapishaji wa sheria hizi ndogo. Kama unakumbuka vizuri tulieleza hapa iko sheria ambayo inaeleza kwamba watu wa Kahama katika barabara zao au katika nyumba zao mbele waweke *pavement blocks*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulieleza kwa masikitiko makubwa kwamba ziko sheria ambazo zimetungwa Dar es Salaam, wakafanya *copy and paste* wakazipeleka katika maeneo mengine, lakini matatizo hayo yanaonekana yanaendelea kujitokeza na bado shida imekuwa kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sheria ya *Electronic and Postal Communication Act* lughua ambayo imeelezwa mle ndani ambayo watu wengi hata kwenye kamati tulijadili sana juu ya kitu kinachoitwa *sim swap*, lakini unavyoona mpaka leo hii mambo bado yameendelea kuwa vilevile. Tunachokiomba ni kwamba Wizara au Serikali ichukulie mawazo yale kama ni mawazo sahihi na kama kuna maeneo ambayo wanatakiwa kuyaweka sawa basi ni vyema tukaelezana katika mikutano ya Kamati inapokutana na Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hayo, yako mambo mengine ambayo nayaona ni kwamba kwa tafsiri yangu ni mambo ya kutozingatia weledi tu, yako mambo ambayo yanaweza yakarekebishwa hata ndani ya ofisi. Ameeleza hapa Mheshimiwa Halima Mdee, lakini pia wameeleza waliotangulia hasa juu ya uandishi mbovu wa kutojua kupangilia vipengele na vifungu vya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi yangu naiomba sana Serikali iendeele kuamini kwamba wanao muda wa kutulia na kujipanga vizuri na wakatengeneza kitu ambacho kitakapokuja kwetu sisi tuwe na sehemu ndogo ya kuongezea nyama na siyo kufikia sehemu ya kuonesha kabisa kwamba hakuna kitu kilichofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeeleza mwanzo, mengi yameelezwa na wenzangu, lakini pia katika hotuba yetu ya Kamati tumejaribu kuchambua kwa undani zaidi na kueleza yale ambayo tumeweza kuyafikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nitumie nafasi hii kupongeza tena Kamati yetu, lakini pia kuendelea kuwatia

moyo Serikali waendeleo kuchukua yale ambayo Kamati inafanya kazi kwa sababu sisi Kamati inafanya kazi kwa niaba ya Bunge na unaposema kwa niaba ya Bunge tunamaanisha kwa niaba ya wananchi wote wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja tuliyotoa, lakini pia naendelea kuunga mkono hoja zote zinazotolewa. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ridhiwani. Tunaendelea na Mheshimiwa Taska Mbogo na baadae Mheshimiwa Peter Msigwa ajiandae.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, ametujalia afya njema na uhai tuko hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niipongeze kwanza Kamati ya Sheria Ndogo, ambayo ni Kamati yangu kwa kazi nzuri inayoifanya chini ya Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Mtemi Chenge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Wajumbe wa Kamati hii kwa sababu moja Kamati ya Sheria Ndogo mtu mwingine/mwananchi au Mbunge anaweza akasema kwamba Kamati ya Sheria Ndogo ni ndogo. Lakini niwaambie wananchi wa Tanzania pamoja na Wabunge mliomo humu ndani, Kamati ya Sheria Ndogo siyo ndogo kwa namna hiyo, kwanza ilipaswa iitwe Kamati ya Sheria Kubwa kwa sababu Kamati hiyo inapitia kanuni zote za Halmashauri zote nchini ambazo zinakwenda kumuathiri mwananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maana kwamba kanuni zote zinazotungwa na Halmashauri nchini Tanzania zinapita kwenye Kamati ya Sheria Ndogo na kanuni hizo zinakwenda kumuathiri mwananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano, unaweza ukaenda miji mingine unakuta Halmashauri imetunga sheria

kwamba ukitupa hata gamba la *big G* chini unalipa shilingi 50,000; ni nani anaathirika, si mwananchi wa kawaida? Ndiyo maana nikasema hizi kanuni zinamuathiri na zinatumika na mwananchi wa kawaida, anaishi nazo kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda nichangie mawili/matatu kuhusu kanuni ambazi zinaletwa kwenye Kamati yetu. Kanuni zinaletwa kwenye Kamati yetu wakati ambapo zinakuwa zimeshakuwa *gazetted* kwenye Gazeti la Serikali na zinakuwa zimeshaanza kutumika na wananchi moja kwa moja wanakuwa wameshaathirika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa zinapokuja pia kurekebishwa, tunapokuja kukaa sisi pale kwenye Kamati tunazirekebisha, zinapokwenda tena kuchapwa na kwenda kutumika tena lakini utakuta *damage* inakuwa ni kubwa mwananchi wa kawaida anakuwa ameshakuwa *damaged*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyochangia wachangiaji waliopita, niombe tu utaratibu utumike kwamba inapotungwa sheria, zile kanuni zinapotungwa zije kwanza kwenye Kamati ya Sheria Ndogo tuzipitie, tuzirekebisha kabla hazijakwenda kuwa *gazetted* kwenye Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine ambao ninapenda kuutoa ambao naona kwamba kanuni na sheria ndogo zinamuathiri mwananchi wa kawaida, ni matamko ya viongozi. Kwa mfano tamko la Waziri, tamko la Mkuu wa Mkoa, tamko la Mkuu wa Wilaya, moja kwa moja linamuathiri mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano, Mkuu wa Wilaya anaweza akatamka kwamba kila Jumamosi ni siku ya usafi maduka yasifunguliwe mpaka itakapofika saa nne asubuhi, anayeathirika hapa ni mwananchi wa kawaida. Kwa maana hiyo ni kwamba kwa mfano mwananchi akifungua lile duka au hoteli yake kabla ya ile saa nne asubuhi, atalipa faini labda ya shilingi 500,000. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi niombe tu yale matamko tunapoyatamka sisi viongozi, awe ni Waziri, Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya, tuyaangalie yasiwe na athari kwa mwananchi wa chini ambaye anakwenda kuishi na yale matamko yetu kwa maisha yake ya kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kutoa pendekezo lingine kwa Serikali, niombe hizo kanuni ziwe zimepita kwenye Kamati ya Sheria Ndogo tuzirekebishe, lakini pia niombe wale watendaji wanapotunga zile kanuni ambazo zinakwenda kutumika kwa wananchi waziangalie zile kanuni ziwe zinaendana na sheria mama. Kwa mfano kanuni haiwezi ikazidi sheria mama, zile kanuni zinatakiwa ziwe chini ya sheria mama au zifuate ile sheria mama inasemaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapotunga kanuni ambayo inakuwa ni kinyume na ile sheria mama ina maana unakwenda nje ya ile sheria, ina maana wewe hapo unatunga sheria nyingine. Kwa hiyo, basi niombe tu wale watendaji wa Serikali wawe wanazisoma vizuri zile sheria na watunge kanuni ambazo zinaendana na ile sheria mama iliyopo ambayo imewafanya watunge kanuni hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninapenda kulitoa kama ombi, Halmashauri zetu nchini Tanzania zinapotunga zile sheria ndogo zijaribu kuzichapa na kuweka kwenye *notice board* ili wananchi wanapopita waangalie kwamba katika mji wetu kuna sheria fulani ambayo tunatakiwa tusiifuate. Ukitunga kanuni ukazikalia ofisini ukaweka kwenye *draw* hizo kanuni zinakuwa hazina faida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano tu niseme unaweza ukawa umetunga kanuni kwamba *parking* eneo hili hairuhusiwi, lakini hujaweka *notice board* na hujaweka kwenye mbao za matangazo kwamba hilo eneo halitakiwi mtu ku-*park* gari, mtu anapokuja ku-*park* unampiga faini ina maana hapo inakuwa si sahihi. Niombe Halmashauri kanuni zao ziwe zinawekwa kwenye mbao za matangazo na pia matamko ya Mawaziri yawe na *limit*, kwa mfano akitoa

tamko liwe na *duration period* kama ni tamko la mwezi mmoja au mwaka mmoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwaombe sisi Wabunge tujaribu kununua yale magazeti yanayokuwa *gazetted*, zile kanuni zinapotolewa kwenye Gazeti la Serikali sisi Wabunge tunatakiwa tununue tuzisome na tukawaeleze wananchi wetu.

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja na mambo yote yaliyoandikwa kwenye Kamati ya Sheria Ndogo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Taska Mbongo, tunaendelea na Mheshimiwa Peter Msigwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru, kwanza kabisa naunga mkono maoni ya Kamati na niwapongeze sana kwa kufanya kazi nzuri sana ambayo kimsingi imekuja wakati muafaka jinsi ambavyo tunaona watu wengi wanaoumia huku chini ni wananchi wanyonge ambao Serikali ya Awamu ya Tano imesema inashughulika nao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ipo kwa ajili ya kumfanya binadamu awe bora, haipo kwa ajili ya kumkandamiza binadamu. Ukiangalia hizi sheria nyingi, hata kwenye Halmashauri zetu ni sheria ambazo zimekuwa kandamizi na zinazidi kuleta ugumu kwenye maisha ya huyu Mtanzania. Kwa hiyo, niseme Mheshimiwa Chenge pamoja na Kamati yako nikushukuru sana kwa kazi kubwa mliyofanya ya uchambuzi ambayo tukienda kwa kina kama wabunge tutaweza kuwasaidia watu wetu wasiteseke sana huko chini ambako kimsingi ndiko wanakoumia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia sheria mama kwa mfano ya BASATA ambayo ilisainiwa na Baba yetu wa Taifa, Mwalimu Julius K. Nyerere mwaka 1985, kifungu cha pili

kimeorodhesha kabisa ni nini sanaa, imefafanua nini ni sanaa, lakini kwenye kanuni alizotuletea Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe hapa ukisoma ukurasa wa 59 ameingiza pamoja na ukumbi nayo ni sanaa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unashangaa ukumbi unakuaje nao ni sanaa, hata ukimuuliza mtoto wa darasa la pili; nina mtoto wangu anaitwa Simon, mtoto wa darasa la pili, ukisema taja kitu ambacho hakihusiani na sanaa azungushie pale, nadhani ukumbi ukiweka miongoni mwake atasema hakipo, sasa sielewi Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe amewekaje. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia sasa kwenye mambo aliyoyataja yanayohusiana na ukumbi. Anasema gharama za kibali kwa kumbi za maonesho sanaa na burudani zenye ukubwa wa kukaa watu wasiozidi 350 yaani unapokwenda kufanya maonesho hayo ukalipe shilingi 350,000 unapeleka BASATA, siyo unalipia ukumbi, unapeleka BASATA, bado ukumbi hujalipia, watu 350 unalipa shilingi 550,000 unapeleka BASATA. Ukumbi unahusianaje na sanaa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikizingalia hizi kanuni za Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe zinakwenda kinyume kabisa na hii sheria mama ambayo Baba wa Taifa aliisaini. Hii inaonesha jinsi ambavyo Serikali ya Awamu ya Tano iko *desperate*, inatafuta hela kwa gharama yoyote ambazo hazihusiani kabisa na masuala ya sanaa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kumbi zenye ukubwa wa watu 750 na kuendelea mtu analipa 1,050,000 kupeleka BASATA, *what is this?* Hapo bado hujalipia ukumbi. Sasa hizi ni sheria kandamizi ndiyo maana narudia tena kwamba niwapongeze sana Kamati, mmefanya kazi kubwa kuangalia sheria kama hizi. Bado kuna kodi mbalimbali na siyo ukumbi tu, sasa haya ni mambo ya kuwanyonya na kuwakatisha tamaa hawa wanyonge. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na kwamba Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe ame-*withdraw* hiki kitu, lakini

bado nasema hii sheria tungetoa maamuzi kwamba isifanye kazi, isimame kwanza kwa sababu ina mapungufu mengi, BASATA bado wanaitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ni sheria hii hii ilimzuia msanii ambaye amejaribu kuiweka Tanzania kwenye ramani, Diamond, wamemzuia anataka kwenda nje, vijana hawa wako *talented*, wanajaribu kutafuta pesa lakini kwa sheria mbovu kama hii tumemzuia asiende kutafuta pesa. Bado hata wasanii wadogo ambao wanajitahidi wanaambiwa wanapotaka kwenda kwenye matangazo watoe shilingi milioni tano, huku ni kuwakandamiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye maelezo yenu yote mmesema mnataka mkuze vipaji, tutakuzaje vipaji kwa kanuni kama hizi. Kwa hiyo, niseme tu kwamba sheria kama hizi zinakandamiza wananchi, zinaonea wananchi, ni wakati muafaka kwamba tufafanue kwa pamoja na ni vizuri sheria kama hizi zisiwe zinaanza kufanya kazi kabla hazijaja tukazipitia humu na wataalam vizuri ili ziwe zinafanya kazi, itasaidia kupunguza matatizo kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo linaendana na hili, kuna wakati mwingine kuna sheria hizi ndogo ambazo zimeainishwa kabisa kwa mujibu wa sheria. Kwa mfano tuna sheria za Serikali za Mitaa, nikichukulia mfano wa kesi ya Mheshimiwa Haonga. Mheshimiwa Haonga alifanya makosa kwenye kikao cha Halmashauri kwa mujibu wa mashtaka aliyopelekewa Mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa bahati mbaya Maafisa wa Mahakama wamekwenda kumshtaki kwa sheria nyingine tofauti na mahakama ambayo mpaka hakimumu anasema mmemleta kwenye mashtaka haya wakati huyu makosa yake alitakiwa ahukumiwe na sheria ndogo ya ndani ya Manispaa. Kwa hiyo, maafisa wanapotosha, badala ya kuisadia mahakama kufafanua vizuri hizi sheria ndogo zinavyotumika, wanajikuta wanapotosha umma, wanatumia sheria nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sawa na hapa Bungeni. Hapa tukikoseana kwa makosa ya kimaadili hauwezi kuchukuliwa hapa ukapelekwa mahakamani kule, ndiyo maana kuna Kamati ya Maadili hapa inakuita inakuonya. Lakini matokeo yake huko mitaani kwenye Halmashauri zetu watu wakifanya makosa ya kimaadili utakuta watu wanatumia madaraka yao vibaya wanawapeleka mahakamani kwa sheria zile mnaita *criminal procedure*, si ndiyo? Sheria za Makosa ya Jinai, wakati watu wamekosea. Kwa hiyo, hata hizo sheria ndogo zipo haziheshimiwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba wale maafisa wa Serikali tusaidiane tuwaelimishe wananchi, tusaidiane kuelimisha mahakama tuiongoze mahakama vizuri kwa sababu wao ni Maafisa wa Mahakama.

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Kwa hiyo, Mheshimiwa Chengo na Kamati yako nikupongeze sana kwa kazi nzuri ambayo kwa pamoja tutakwenda kuwasaidia wananchi wetu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mche. Peter Msigwa. Sasa namkaribisha Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo aweze kuhitimisha hoja.

MHE. ANDREW J. CHENGE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi niweze kuhitimisha hoja yangu iliyo mbele ya Bunge lako. Nitajitahidi niongee kwa kifupi sana kwa sababu ya muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kumi waliopata nafasi ya kuchangia kwa kuongea humu Bungeni na Waheshimiwa Wabunge wawili waliochangia kwa maandishi, niwashukuru sana. Mmeelewa hoja na mmeleza vizuri changamoto ambazo zipo katika shughuli za sheria ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na moja la jumla, Waheshimiwa Wabunge ndiyo maana Serikali inapoleta miswada tujitahidi sana tunapoiunga mkono Serikali, maana shughuli za Serikali lazima ziende, lakini tuwe makini sana wanapowaambia kwamba masuala haya tutakwenda kuyaweka kwenye *regulations*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli muswada hauwezi ukafafanua kila *aspect* lakini ile misingi na mipaka ya utekelezaji wake unataka uione, iwe katika sheria mama na mkifanya hivyo usimamizi wenu kama Bunge, *oversight, control, supervision* ya sheria ndogo utakuwa na maana sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona zipo kanuni, sheria ndogo ukiziona unajiuliza hivi..., lakini kwa sababu ni sheria za nchi zinatumika, lakini tukianza vizuri kuwa makini na kile ambacho tunakikasimu *then* tutakuwa *on a good footage*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, limesemewa vizuri sana, kwa nini hizi sheria ndogo zisianze kutumika mpaka hapo utaratibu fulani unapofanyika? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu hivi, katika nchi za Madola, tuna mifumo ya aina mbili ya kusimamia madaraka ambayo Bunge limekasimu kwa vyombo vingine. Mfumo wa kwanza unaitwa *affirmative resolution procedure* yaani unaleta hizo rasimu zako za sheria ndogo unaziweka mezani kabla hazijaanza kutumika na Wabunge ndiyo wanapata nafasi ya kuona kinacholetwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua hiyo wanaweza wakasema *no*, kanuni hizi na hizi au kanuni hii hapana, kwa hiyo, wanakwenda kuirekebisha huko halafu ndiyo inakwenda kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali ianze kutumika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna utaratibu wa pili ambao unaitwa *negative resolution procedure* ambao sisi

Tanzania ndiyo tunaangukia humo, kwamba ukiisoma Sheria yetu ya Tafsiri ya Sheria, na ndiyo maana taarifa ya Kamati inasema udhibiti wa Bunge siyo wa moja kwa moja, unasubiri kwanza ichapishwe kwenye Gazeti la Serikali ili iwe sheria ndogo halafu iwasilishwe Bungeni. Lakini ikishachapishwa imeshaanza kutumika, ndiyo tofauti ile ya *affirmative* na hii ya *negative*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mmelisema vizuri Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Rashid Abdallah, Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa Zainab na wengine Mheshimiwa Kingu na Mheshimiwa Aida, kila mmoja karibu amegusia Mheshimiwa Ridhiwani wameyagusia, mimi nasema yote haya jamani yanazungumzika, hizi ni sheria zilitungwa na Bunge hili. Tukiona kwamba utaratibu wa *negative resolution procedure* haujakaa vizuri tunajenga hoja, tunashauriana na Serikali tukielewana tunafanya marekebisha, tu-*adopt the negative* ni nani *affirmative relation procedure*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naelewa Mheshimiwa Mdee amelisema vizuri sana Bunge letu halikai kila siku. Lakini unaweza kwa sababu tunajua lini mikutano yetu ya Bunge inapaswa kufanyika. Mnaweza mkajipanga na sheria ikasema wazi *except* kwa aina fulani ya sheria ndogo za dharura zile maana dharura ni dharura hauwezi ukasema isubiri sijui nini. Unaweza utaratibu ambao unawezesha Bunge kupitia Kamati husika kuweza kuyaangalia haya, mimi nadhani tutakapokuja kuelewana kwa hivyo tutaenda vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru sana mlioiona maana hizi ni sheria wala usiseme Sheria Ndogo kwa sababu ni *subsidiary*, lakini zitatumika na wanachi na zingine *is very hash* ikikosewa tu kidogo unamuumiza mtu; na hapa nichukue nafasi kumshukuru sana Mheshimiwa kwa kuona busara aliyोजना kwamba turejeshe utaratibu huu na Taarifa za Kamati ziwe zinawasilishwa mara mbili kwa mwaka maana ni sheria zinatumika, tusiruhusu wananchi wanaendelea na vyombo vingine wanaendelea kuumia kwa

sababu tu sheria hazijapitiwa na Bunge kupitia Kamati husika.
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge kundi la sheria ndogo limetajwa kwenye Sheria ya Tafsiri *subsidiary legislation means any order, proclamation, rule of court, regulation, notice, by law or instrument made, narudia made under any act or other lawful authority.* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huo ndiyo msingi ni vema tunapoyaangalia haya tuzingatie, sheria ndogo haiwezi ikavika ukuu ambayo haina katika sheria mama. Hiyo misngi ya kutunga sheria na tafsiri haiwezi ikajibika ukuu ambao haina katika sheria mama. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa vile Serikali ipo najua nilivyosema kwenye taarifa tunafanya kazi karibu sana na Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Mheshimiwa Jenista Mhagama kama *coordinator* wa shughuli za Serikali na *Chief Whip* wa Serikali Bungeni katika shughuli hizi na hili la BASATA niseme namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwakyembe kwa sababu alipofika kwenye Kamati aliliona na akasema kiungwana tu jamani nipeni muda na mtu muungwana akimwambia hivyo lazima na wewe uoneshe uungwana, ndio maana tukasema sisi tutasema tu kwamba ilipaswa ije lakini kwa sababu haijaka vizuri tumekubaliana itakuja katika Mkutano mwingine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kwa sababu lazima sasa baadae Bunge litaamua nisome sasa maazimio haya ili Bunge litakapohojiwa lijue linaamua nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kwanza inahusu dosari ya uandishi wa majedwali ikilinganishwa na vifungu vya sheria.

KWA KUWA katika uchambuzi wa Kamati imebainika kuwa baadhi ya sheria ndogo zinadosari mbalimbali katika majedwari kuhusu vifungu vinavyoanzisha majedwali husika.

NA KWA KUWA kwa mujibu wa kifungu cha 25(2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinabainisha kwamba majedwali ni sehemu ya sheria;

KWA HIYO BASI Bunge linaazimia kwamba Wizara ambazo sheria ndogo zake zimebainika kuwa na dosari katika majedwali zifanyanyiwe marekebisho ili kuondoa dosari hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, azimio la pili linahusu kukinzana na masharti ya sheria mama au sheria nyingine za nchi.

KWA KUWA baadhi ya sheria ndogo zilizofanyiwa uchambuzi na Kamati zimebainika kuwa na vifungu vinavyokinzana na masharti ya sheria mama au sheria nyingine za nchi.

NA KWA KUWA kukinzana huko ni kwenda kinyume na masharti ya kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinachotoa sharti kuwa sheria ndogo kutokwenda kinyume na masharti ya sheria mama.

NA KWA KUWA kukinzana huko kuna ifanya kanuni husika kuwa ni batili kwa kiwango kilichokinzana.

KWA HIYO BASI Bunge linaazimia kwamba Wizara zinazohusika kufanya marekebisho katika sheria ndogo hizo ili kuondoa vifungu vinavyokwenda kinyume na masharti ya sheria mama au sheria nyingine za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.
(Makofi)

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mtemi Chengo hoja yako imeungwa mkono. Sasa kabla bado

sijalihoji Bunge nampa fursa Mwanasheria Mkuu kwa dakika tano na baadae *Chief Whip* ili tuweze kumaliza.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, kwanza nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Chenge Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kwa mawasilisho yake na kwa hoja alizotoa na wote tunamfahamu nakumkiri Mheshimiwa Chenge katika umahiri wake wa sheria. Kwa mimi binafsi nimtangulizi wangu, ni kaka yangu amekuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa hiyo, huwa napata pia mawazo na ushauri mwingi kutoka kwake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika masuala la sheria siku zote kuna mambo mawili makuu ambayo hata Mheshimiwa Chenge anayafahamu vizuri sana. Kuna masuala ya misingi yaani *principles* na kuna masuala ya utaratibu yaani *procedure* au *enabling procedures*. Tunapokuja suala la udhibiti wa Bunge katika suala la utungaji wa Sheria Ndogo na tukaja kwenye *principles* hakuna ubishani, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ile Ibara ya 97(5) imeeleza vizuri. Hata hii *Interpretation of Laws Act* nadhani ni kifungu cha nne haina ubishi. Lakini pia misingi hii kwa wanasheria wanajua iko kwenye *principles* za *Administrative Law*, sijui kwa Kiswahili tunaweza kusema Sheria ya Utawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *principles* hakuna shida na tunakubaliana Serikali na Kamati na kila mtu. Kuna changamoto kunapokuja kwenye utaratibu na ndiyo maana Mheshimiwa Chenge mwenyewe katika taarifa hii na ameirudia wakati anahitimisha kwamba waliona na ninapenda tena kurudia kusoma hii sehemu ukurasa wa nne wa ripoti hii kwamba; hata hivyo udhibiti huo yaani udhibiti wa Bunge katika utungaji wa sheria ndogo siyo wa moja kwa moja kwa sababu Bunge halina mamlaka ya kuingilia mchakato wa kutungwa kwa sheria ndogo yoyote mpaka sheria ndogo inapotangazwa katika Gazeti la Serikali na kuwasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ametueleza vizuri sana Mheshimiwa Chenge vizuri ametuelimisha taratibu zinazotumika katika Mabunge ya Jumuiya ya Madola. Lakini kwa nini sentensi hii iliwekwa ni kwa sababu ya ile *concept* hii ni *delegated legislation*. Kwa hiyo, Bunge kimsingi haiwezi tena likaja na kuanza kujadili zile sheria ndogo kwa sababu litakuwa limefuta ile *concept* ya *delegated legislation* na ndio hiyo changamoto pekee iliyopo na ndiyo maana akaeleza juu ya taratibu hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nilitaka niseme, hata ukienda kwenye kanuni zetu za Bunge Toleo sasa la Januari 2016 ukiangalia ile Kanuni 80 mpaka ya 93 zinahusu utungaji wa sheria unaofanywa na Bunge, hakuna kanuni inayozungumzia Bunge litakavyofanya kazi dhidi ya sheria ndogo ambazo zimeshatungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tungekuwa tunatumia huu mfumo wa kwanza aliutaja wa *affirmative resolution procedure* tungekuwa na kanuni hizo kwenye Bunge letu zitatuongoza tunapotunga sheria tunazoziiita kubwa huu ni utaratibu, tukija tunaposhughulika na sheria ndogo huo ni utaratibu hatuna huo utaratibu ni kwa sababu tunatumia ile aina ya pili aliyoizungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme na nikumbushe na Mheshimiwa Chenge ni mahiri sana katika hili; katika mfumo sasa wa *Common Law* siyo wa *Commonwealth Parliament*, wa *Common Law* sheria ndogo ndogo kama zina matatizo nini utaratibu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu siku zote umekuwa kupitia kitu kinaitwa *judicial review* na hiyo inafanyika *judicial review* moja wapo ya misingi ya *judicial review* ni kama ile sheria iko *ultra vires* yaani inapingana au imejipa ukuu zaidi ya ile sheria mama ambacho Mwenyekiti alikuwa anakieleza hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, upo utaratibu katika mfumo wa sheria wa *Common Law*. Sasa nilitaka tu

ku-*share* hilo na kuonyesha shida kidogo. Naomba dadika moja kuna kitu cha muhimu nimalizie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa yamezungumzwa mapungufu katika uandishi wa sheria. Tunayakiri haya kwamba yametokea mapungufu mara kadhaa katika uandishi wa sheria ni mojawapo ya changamoto ambazo Afisa Mwanasheria Mkuu wa Serikali imekuwa nazo na ndiyo maana mwaka huu Mheshimiwa Rais akaamua kutoa maelekezo ya kuunda.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, na kuusuka upya Ofisi...

MWENYEKITI: Mheshimiwa naomba ukae muache amalizie Mwanasheria Mkuu. (*Kicheko*)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: ...ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kwa hiyo zile changamoto zilizozunguzwa za uandishi za upungufu wa watu na kadhalika...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo zitashughulikiwa na zinaendelea kushughulikiwa tunavyoongea, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, Mheshimiwa Jenista dakika tano.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti,

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Waheshimiwa naomba make tumalizie tumefikia mwisho.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana utaratibu lazima ufuatwe.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jenista naomba uendelee.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wanachofanya nini basi toa nafasi na huku.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ester naomba utulie tuendelee Mheshimiwa Jenista.

MBUNGE FULANI: Heshimu kiti.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasimama hapa kwa mujibu wa kanuni na wewe unajua na Mheshimiwa...

WABUNGE FULANI: Hoja ya Kamati.

MWENYEKITI: Waheshimiwa naomba tutulie Mheshimiwa Jenista malizia.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mujibu wa kanuni ina jukumu na kwa mujibu wa sheria tulizonazo inajukumu la kuleta mbele ya meza yako sheria ndogo zote ambazo zimekwisha kutangawa kwenye Gazeti la Serikali na inawekwa mbele ya meza yako tukufu na baada ya Kamati ndogo Kamati ya Sheria Ndogo kumaliza kazi yake hii yote nzuri kama ilivyofanywa leo. Ofisi ya Waziri Mkuu inajukumu la kupokea maoni yaliyotolewa na Kamati ndogo na ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge wawe watulivu wajue tunachotaka kusema. Na wakati mwingine utaratibu wa kelele kelele siyo wa Kibunge. *(Makofi)*

WABUNGE FULANI: Aaah, hapana.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu ina jukumu la kupokea maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Sheria Ndogo na kuyawasilisha kwa Wizara zote husika kwa jinsi yalivyochambuliwa na Kamati ya Sheria Ndogo. Hata Mheshimiwa Halima anajua, nimekuwa nikienda mpaka kwenye Kamati kupokea majedwali hayo kwa niaba ya Wizara zote.

Ninasimama hapa kusema yafuatayo, kwanza ninampongeza Mwenyekiti kwa kazi yake nzuri; pili, ninawapongeza Wajumbe kwa kazi yao nzuri; na tatu ninatambua yale yaliyojiri kwenye taarifa ya Kamati ndogo na yamewekwa vizuri sana na *summary* ya Mheshimiwa Mwenyekiti wakati akihitimisha hoja yake. Ni yapi? (*Makofi*)

Kwa mujibu wa sehemu ya tatu ya Kamati za Kisekta Mtambuka ambayo kifungu kidogo cha (c) kinaitambua Kamati yetu ya sheria na kifungu cha 11 kimeelezwa vizuri na Mwenyekiti wakati akihitimisha hoja yake, wajibu wa Kamati Ndogo wameutekeleza Kamati inayoshughulikia Sheria Ndogo wametokeleza vizuri mambo makubwa yaliyojiri ambayo ninatokanayo na nitayawasilisha kwenye Wizara husika kama yalivyowekwa mezani na Mwenyekiti wa Kamati Sheria Ndogo ni pamoja na hayo mawili aliyoyazungumza kuhusu majedwali yanayoenda na sheria mama. Lakini vilevile makosa madogo madogo ambayo yamekuwa yakijitokeza na kujirudia katika sheria ndogo zina zotungwa yanayoendana kinyume na sheria mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo limejitokeza suala la Watendaji wetu wanaosimamia ama wanaoshughulikia sheria hizi ndogo kutokuwa na umakini katika kufanya kazi yao. Jambo hilo ninaomba nilichukue pia na liweze kufanyiwa kazi ya kutosha na Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile amesema ziko Wizara ambazo zimejitokeza kwa nguvu kidogo kwenye taarifa ambazo zimekuwa zikichambuliwa na Kamati yetu

Kamati ya sheria ndogo, nazo tutazifikishia majedwali hayo ili yaweze kufanyiwa kazi sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulihakikishia Bunge lako tukufu kadri tunavyofanya kazi na Kamati ya Sheria Ndogo tumekuwa na mabadiliko makubwa na tunaishukuru sana Kamati ya Sheria Ndogo imekuwa ni msaada mkubwa sana kwa uandishi wa sheria ndogo ndani ya Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo na sisi kama Serikali tutaendelea kufanya nao kazi kwa karibu ni kwa maslahi ya Taifa na nchi yetu na si kwa maslahi ya mtu mwingine yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa niaba ya Serikali tutayatekeleza hayo yote. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Jenista pamoja na Mwanasheria Mkuu.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Sasa nalihoji Bunge.

*(Hoja Ilitolewa lamuliwe)
(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

(Taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuhusu uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge ilipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Kwa hiyo, taarifa maoni na mapendekezo ya Kamati yetu ya Sheria Ndogo imepitishwa kuwa maazimio ya Bunge rasmi na kama ambavyo Serikali imeahidi itaenda kuyafanyia kazi na inaendelea kuyafanyia kazi. Niwashukuru niwapongeze wote hasa Mwenyekiti wa Kamati kwa kazi kubwa unayoifanya na timu yake yote. Pia niwashukuru Serikali kwa kupokea na kuahidi kwamba watayafanyia kazi.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Baada ya kusema hayo tumekamilisha shughuli zetu za leo na naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

(Saa 07.00 mchana Bunge liliahirishwa hadi siku ya Ijumaa Tarehe 14 Septemba, 2018 Saa Tatu Asubuhi)